

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Hamsini na Mbili – Tarehe 16 Juni, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatuh Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa tuketi.

Katibu!

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Swali letu la kwanza Ofisi ya Raisi, TAMISEMI, Mheshimiwa Nicodemus Henry Magonga, Mbunge wa Mbogwe.

MHE. NICODEMUS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, sio Nicodemus Magunga ni Nicodemus Henry Maganga, ahsante kwa kunipa...

MWENYEKITI: Basi kaa chini sio wewe.

MHE. NICODEMUS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mimi umeisema vibaya.

MWENYEKITI: Basi sema!

Na. 430

Kutengeneza Barabara za Jimbo la Mbogwe

MHE. NICODEMUS H. MAGANGA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara zote mbovu zilizopo katika Jimbo la Mbogwe?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbogwe lipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe lina mtandao wa barabara wenyewe urefu wa kilomita 1,344.3. Serikali imekuwa ikifanya matengenezo ya barabara mbovu, pamoja na matengenezo ya kawaida kwa barabara zenye hali nzuri kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe iliidhinishiwa shilingi bilioni 1.30 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometra 78.6, makalvati mistari 27, boksi kalvati moja pamoja na ujenzi wa barabara ya Mang'ombe – Magetini mpaka Kona nne, yenye urefu wa kilometra 1.2. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, jumla ya shilingi bilioni 1.64 ziliidhinishwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometra 46.6, makalvati mistari 18 pamoja na ujenzi wa barabara ya Masumbwe – Iponya yenye urefu wa kilometra moja kwa kiwango cha lami na barabara ya Mang'ombe, Magetini – Kona nne, yenye urefu wa kilomita 0.8 kwa kiwango cha lami, ujenzi wa barabara hizo umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.14 kwa ajili ya matengenezo ya barabara yenyе urefu wa kilometa 74.96, Mtaro wa mawe kilometa 1.2 na ujenzi wa barabara yenyе urefu wa kilometa moja kwa kiwango cha lami katika Mji wa Masumbwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matengenezo yaliyofanyika katika mwaka wa fedha 2019/2020 na 2020/2021, yamejumuisha barabara muhimu zilizokuwa mbovu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, zikiwemo barabara ya Shenda - Mwabomba yenyе urefu wa kilometa 17, barabara ya Isebya-Lwamgas yenyе urefu wa kilometa 10. Barabara ya Ushirika-Kadoke-Ntono yenyе urefu wa kilomita 5.5, barabara ya Ikunguigazi – Isabya - Nyashinge yenyе urefu wa kilometa 15, barabara ya kanegere – Prison-Nyakasaluma-Bunyihuna yenyе urefu wa kilometa 19.46, barabara ya Ishigamva-Busabaga-Ilolangu yenyе urefu wa kilometa 15 na barabara ya Ilolangu -Kisumo-Bukombe boda yenyе urefu wa kilomita 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, ili kuhakikisha zinapitika katika majira yote ya mwaka na kuwezesha huduma za usafiri na usafirishaji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maganga.

MHE. NICODEMUS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, nakushkuru Mheshimiwa Waziri, uzuri umejibu halafu umefanya ziara kwangu, hizo barabara zote ulizozisema ni mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza ambayo ni hatarishi sana, daraja la Budoda halipitiki toka kwenye kampeni. Je, Serikali haina mfuko wa dharura kwenda kurekebisha madaraja ambayo yanawafanya wananchi kupoteza Maisha? Kuna Kata ya

Ngemo, Mtanya pamoja na Ludembela, kuna madaraja mpaka sasa hivi hayapitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa wewe Mheshimiwa Naibu Waziri, ulifika kwenye jimbo langu na ukajionea na tulizama mara tatu. Je, kwa sasa hivi na bunge linakwenda kuisha, nikawaambieje wananchi kulingana na ubovu wa barabara hizi ambazo hazipitiki?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nicodemus Maganga, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ameuliza kwamba daraja la Budoda halipitiki kwa muda mrefu tangu kipindi cha kampeni, kwa hiyo akseliza kama hakuna fedha za dharura. Niseme tu Mheshimiwa mbunge nimelipokea jambo lako na ninalikabidhi kwa *TARURA* Makao Makuu, ili waende wakafanya tathmini hiyo na watuletee taarifa ili tutafute fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la Pili ameuliza atawaambi nini wananchi, kwa kuwa bunge linakwisha na barabara zake bado hazipittiki. Nenda kawaeleze tu kwamba Serikali tumejipanga kuhakikisha kwamba tunamaliza matatizo ya barabara maeneo mengi nchini. Na katika hatua ya awali ambayo tulioichukuwa ni kupeleka fedha milioni 500 kwenye kila Jimbo, ambazo zitakwenda kujenga barabara za lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili waeleze wananchi wako kwamba, mara baada ya bajeti ya Serikali kupita, kikiwemo kile kifungu maalum cha kuongeza fedha za *TARURA*, tutaongeza fedha katika Jimbo lako ambazo zitasaidi zaidi zile barabara ambazo ni mbovu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Zaytun Seif Swai.

Na. 431

Uwiano Sawa wa Mikopo ya 10% kwa Halmashauri Zote

MHE. ZAYTUN S. SWAI aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka uwiano sawa wa mikopo ya asilimia 10 inayotokana na mapato ya ndani bila kujali mapato ya halmashauri husika ili kusaidia wanufaika wa mikopo wanaoishi nje ya miji wapate fursa sawa na wanufaika wa mijini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura ya 290 kifungu cha 37(a) na Kanuni zake za mwaka 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Sheria ya mikopo ya asilimia 10 ya wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ni asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri baada ya kuondoa mapato lindwa. Hivyo kiwango cha mikopo kinatokana na uwezo wa makusanyo ya halmashauri husika. Halmashauri zimeelekezwa kutoa fursa sawa za mikopo kwa vikundi vyote vilivyokidhi vigezo vilivyopo ndani ya halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo hii ni sehemu tu ya mifuko mbalimbali ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi iliyopo nchini, na Serikali itaendelea kuboresha kadri itakavyohitajika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zaytun.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushkuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza mawali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, wakati Mheshimiwa Rais, mama Samia Suluhu Hassan, anahutubia wanawake wiki iliyopita, aliaota maelekezo kwenye halmshauri zetu, waweze kutoa mikopo mikubwa kwa vikundi ili kuongeza tija ya mikopo hii. Je, lini halmashauri zetu zitaanza kutekeleza maagizo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wanawake wa Mkoa wa Arusha wamenituma, pmoja na makundi mengine tajwa ya vijana na walemavu, kumekuwa na urasimu mkubwa sana kupata mikopo ya halmashauri. Wanufaika hawa wanatembea umbali mrefu, kufatilia mikopo hii Halmashauri bila ya mafanikio, naomba kusikia kauli ya Serikali juu ya jambo hili, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa viti maalim kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, ni jambo la msingi sana, Mheshimiwa Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan, ameelekeza na ameweka msisitizo kuhakikisha kwamba, mamlaka za Serikali za Mitaa zinatoa mikopo yenye tija kwenye vikundi vya wajasirimali, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Ni kweli kwamba mikopo hii ambayo

imekuwa inatolewa, imekuwa inatolewa kwa kiwango kidogo, ambacho hakiwakwamui wajasiriamali kutoka hatua moja kwend hatua nyengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais TAMISEMI, tumekwishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa mamlaka ya Serikali za Mitaa, kuhakikisha wanatoa mikopo hiyo yenye tija, ya kuwawezesha sajasiriamali hao kujikwamua. Kwa hiyo naomba nimuhakikishie Mheshimiwa mbunge kwamba Serikali tayari inatekeleza maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais, na tumeshtaoa maelekezo kwa Wakurugenzi na kazi hiyo inaendelea kuhakikisha mikopo ile inatolewa kwa kiwango kinachokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kweli kwamba kwa jografia ya halmashauri zetu nydingi, kuna umbali mkubwa kati ya maeneo ambayo wajasiriamali wanafanya shughuli zao, na Makao Makuu ambapo wanahitaji kupata huduma hizi za mikopo.

Mheshimiwa mwenyekiti, tumendelea kuboresha pia maafisa mikopo katika Halmashauri, maafisa wa maendeleo ya jamii kuwafikia wajasiriamali katika maeneo yao, kuwawezesha na kuwarahisishia uwezekano wa kupata mikopo hii. Na Serikali itaendelea kuboresha mbinu hizi ili kuendelea kurahisisha upatikanaji wa mikopo.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa naibu Waziri kwa majibu mazuri sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Nape.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushkuru kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa pamekuwa na tatizo la matumizi ya hizi fedha za mikopo kwa maeneo mengi, na hasa maeneo mengine zimekuwa zikipelekwa kutumika kwenye maeneo yasiyo kusudiwa baada ya kukopwa.

Je, Serikali haioni wakati umefika sasa badala ya kutoa fedha, tutoe vifaa vinanyoendana na biashara husika au shughuli husika ambaao inakopewa. Kwa sababu hivi vifaa tunahakika vitakwenda kufanya shughuli iliyokusudiwa, mfano, matrektu au vifaa vya uzalishaji badala ya kutoa fedha kama fedha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Nape Moses Nnauye Mbunge wa Mtama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Serikali inatambua kuna mikopo ambayo inatolewa kwa maada ya fedha taslim kwenye vikundi, pia kuna mikopo ambayo sasa tumeboresha utaratibu wa kutoa vifaa vitakavyowawezesha wajasiriamali kutekeleza shughuli zao; Kwa hivyo wazo lake ni zuri sana. Na sisi kama Serikali tumelichukua tumeanza kulifanya kazi, kuna vikundi ambavyo kimsingi vinahitaji vifaa, na kuna vikundi ambayo vitahitaji fedha kwa ajili ya aina ya shughuli zake, na hili nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kulitekeleza. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Tunaendelea, Ofisi ya Makao wa Rais, Muungano Mazingira, Mheshimiwa Soud Mhommed Jumah.

Na. 432

Fedha za Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH aliuliza: -

Je, Taasisis ngapi zimeweza kujisajili hadi sasa na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund*) nchini, na miradi mingapi imeshaombewa kupitiwa mfuko huo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). Naomba kujibu swalı la Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge Jimbo la Donge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund*) ulianzishwa mwaka 2010 na kuanza kufanya kazi mwaka 2015. Taasisi inayotaka kuomba fedha kutoka katika Mfuko huu, ni lazima iwe imesajiliwa au kupata *ithibati* chini ya Mfuko huu. Ithibati au usajili hutolewa baada ya taasisi husika kutimiza vigezo stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko wa mabadiliko ya Tabianchi unaruhusu taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa, kusajiliwa ili kuweza kuomba fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya mabadiliko ya tabianchi. Hadi kufikia mwezi Machi 2021, mfuko huu ulikuwa umesajili jumla ya taasisi 74 ulimwenguni kote. Hapa nchini, taasisi iliopata usajili ni moja tu, ambayo ni Benki ya CRDB. Tunaipongeza Benki ya CRDB kwa kuweza kupata ithibati ya mfuko huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa usajili wa taasisi katika mfuko huu wa mabadiliko ya Tabianchi hauna ukomo. Serikali inaendelea kuhamasisha taasisi nyingine za hapa nchini kujisajili na mfuko huu, ili kuwa na uwezo wa kupata fedha na kutekeleza miradi mbalimbali ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi, hadi sasa jumla ya miradi sita imeombewa fedha kutoka Mfuko huu kupitia taasisi mbalimbali. Hata hivyo, ni miradi miwili tu ambayo fedha yake imeidhinishwa. Miradi hiyo ni Pamoja na mradi wa Maji kwa Kuwezesha uhimili katika Mkoa wa Simiyu (Dola za Marekani millioni 120), na mradi wa

pili, ni mradi wa kuandaa Uwezo wa CRDB (Dola za Marekani 560,000) ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Soud Mohammed.

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa MwenyeKITI, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kuna taasisi tatu hapa nchini za *NEMC*, Wizara ya fedha pamoja na *TAMISEMI*, zimeanza mchakato karibu miaka sita mapaka kumi iliyopita, na mpaka leo hazijaweza kukamilisha utaratibu wa kuweza *accredited*.

Je, Wizara au Ofisi Makamo wa Rais Mazingira, ina mpango gani wa kuweza kuzihamasisha na kuzijengea uwezo taasisi hizi ziweze kukamilisha mchakato huu na kuweza kufaidika na fedha hizi?

Mheshimiwa MwenyeKITI, la pili, kwa vile Zanzibar hakuna taasisi hata moja ambayo imeanza mchakato huu. Je, kuna utaratibu gani au mikakati gani ambayo imepangwa na Ofisi ya Makamo wa Rais Mazingira, kuweza kuzijengea uwezo taasisi za Zanzibar na kuzihamasisha ziweze kuanzisha mchakato wa kuijunga na mfuko huu wa taibanchi. Ahsant sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, wamjibu kwa kifupi sana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa MwenyeKITI, naomba kujibu swali na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa mwenyeKITI, ni kweli katika hizi fedha za mifuko hii miwili ya *Adaptation na Green fund*, hizi mara nyingi sana tushindwa kuzi – *access* kwa muda mrefu, hata hivyo Ofisi ya Makamo wa Rais Muungano na Mazingira, imeweza kuhakikisha kwamba katika kipindi cha hivi karibuni imejitahidi kufanya kazi yake kubwa vya kutosha, na tushukuru sasa hivi, kwa mfano, *NEMC* imefanikiwa kupata fedha kutoka mfuko

wa *Adaptation Funds*, ambao ni wastani wa shilingi billion 6 ambazo hizi tupo katika mchakato na Wizara ya fedha kuweza kuzi – *access* vizuri ili ziweze kufanyakazi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunaendelea kuzijengea uwezo taasisi hizo. Tunafahamu kwamba TAMISEMI walianza mchakato takriban miaka mitatu, na bado kuna suala la *capacity* tunaendelea kulifanya kazi. Kwa upande huu wa Zanzibar, juzi tulikuwa na ziara kule Zanzibar (Unguja na Pemba) na jana tulimaliza. Miiongoni mwa jambo kubwa sana tulokubaliana nalo ni suala zima la kuangalia jinsi gani tutafanya kazi kwa pamoja katika upande wa kimazingira, kwa sababu jambo la mazingira linakata maeneo yote mawili.

Mheshimiwa mwenyekiti, hili naomba nikuhakikishie Mheshimiwa mbunge, mimi na dada yangu kule Mheshimiwa Saada Mkuya, ambae anahusiana na upande wa Mazingira kwa upande wa Zanzibar, tutafanya kila liwezekanalo kwa umoja wetu. Na hivi sasa Mkurugenzi wetu wa Mazingira anaitwa Dkt. Andrew Komba hivi muda huu ninayozungumza yuko Zanzibar akifanya kikao na wakuu wa Mikoa kule Pemba, katika *ajenda* kubwa ya kuangalia jinsi gani tutafanya ajenda ya pamoja ya mazingira ndani ya nchi yetu.

MWENYEKITI: Majibu hayo yametosha Mheshimiwa. Tunaendelea na Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Halima James Mdee kwa niaba yake Mheshimiwa Shally.

Na. 433

Biotech Products Limited Kusaidia Mapambano ya malaria

MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE
aliuliza:-

Je, uwepo wa Kiwanda cha kuua mazalia ya Mbu (*Tanzania Biotech Product Limited*) umesaidia vipi mapambano dhidi ya Malaria nchini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu. Wanaume mpo. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Wanaume mpo?

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE

NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hawapo, inakuwa shida sana kuwaona mpaka uvae miwani ya *x-ray*. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii lilikuwa linauliza je, uwepo wa kiwanda cha kuua mazalia ya mbu kimesaidia vipi mapambano dhidi ya malaria nchini? Tangu Kiwanda cha Tanzania *Biotech Product Limited* kuanza uzalishaji mnamo mwaka 2016, jumla ya lita 340,520 za viuadudu zimenunuliwa na Serikali kwa gharama ya shilingi bilioni 4.5 ambazo ni wastani wa shilingi 13,200/= kwa lita. Lita hizi za viuadudu zilisambazwa katika Mikoa 28 na kuzifikia Halmashauri zote 185 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudii hizi ziliungana pamoja na utekelezaji wa afua zingine za udhibiti wa malaria zikiwemo matumizi ya vyandarua, kupulizia viatilifu - ukoko ndani ya nyumba hasa kwenye maeneo yenye kiasi kikubwa cha maambukizi ya malaria na uwepo wa vipimo na dawa zenye ubora kwenye kutibu wagonjwa watakaothibitika kuwa na malaria. Hivyo, matokeo ya juhudii hizi ni kuwa, zimefanikisha kupungua kwa idadi ya Mikoa yenye hatari kubwa ya maambukizi ya malaria kutoka Mikoa 11 mwaka 2017 hadi Mikoa Saba mwaka 2020. Aidha visa vipyaa vya malaria vimepungua kwa asilimia 35 kutoka wagonjwa 162 kwa kila watu 1000 mwaka 2015 hadi wagonjwa 106 kwa watu 1000 mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumthhibitishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa Serikali

itaendelea kutumia bidhaa za Kiwanda chetu cha Kibaha kwa ajili ya kuchangia jithada za Serikali kufikia kumaliza Malaria (*elimination*) ambapo tumedhamiria kuwa ifikapo 2025 kiwango cha malaria kiwe kimepungua hadi kufikia asilimia 3.5 kutoka asilimia 7.5 ya mwaka 2017. Aidha, Serikali itahakikisha kila Halmashauri inaendelea kuwajibika kwenye kuhakikisha kuwa inatenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya utekelezaji na hapa wanafanya vizuri. Mwaka huu wa fedha tunaoenda kuanza mpya wametenga bilioni 2.7 lakini ilikuwa milioni 600 mwaka 2020/2021. Kwa hiyo tunaenda vizuri. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shally.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Kwa kuwa, azma nzima ya kuondoa malaria siyo kupunguza bali ni kumaliza kabisa na Zanzibar wamefanikiwa. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kugawa viuadudu hivyo wakati wa *weekend* zote za kufanya usafi majumbani kwa watu? (*Makofii*)

Swali la pili, kwa kuwa Kamati ya Bunge ilipotembelea kwenye kiwanda hicho ilikuta bado Halmashauri nyingi hazijalipa mikopo ambayo walichukua. Ni lini sasa Serikali italipa ili kiwanda kile kiweze kuendelea vizuri. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, ni lini. Jiandae Mheshimiwa Tunza.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunaelekea kwenye *elimination* na ndiyo mkakati wa Serikali na tumejipanga pamoja na wadau wetu kwamba tunapata fedha kwa ajili ya kufanya haya masuala ya kununua hivi viuadudu endelevu kwa ajili ya kuelekea kwenye *elimination*. Kwa mfano, Serikali ya Uswiss kwenye mpango wake wa Miaka Nne, 2021- 2024 kuna bilioni 4.4 zimetengwa ambapo bilioni 3.7 zitatumika kununua lita 284,810 kwa ajili ya utekelezaji huo. Sasa hivi tunaandika andiko ambalo

litagharimu bilioni 294 kwenye Mwaka wa Fedha ujao tutalileta kwa wastani wa bilioni 59 kila mwaka tuweze kuwa na utaratibu wa kuwa tunapuliza haya mazalia mpaka kila kitu kishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haya masuala ya Halmashauri kutokulipa kama nilivyo sema kwenye jibu la msingi zimetengwa bilioni 2.7 tutasimamia walipe yale madeni lakini waendelee kuchukua na kupewa viuadudu vingine vya ziada. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Tunza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa Mikoa ambayo inaongoza kwa maambukizi ya malaria ni pamoja na Mkoa wa Mtwara. Nataka kujua mkakati wa Serikali kuhakikisha Mkoa ule unaondoka katika janga hilo la ugonjwa wa malaria. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri. Ahsante.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mkoa wa Mtwara ni kati ya Mikoa ambayo ina maambukizi makubwa ya malaria, tunalitambua hilo, iko Mikoa ya Lindi, Katavi na mingine mingi. Tunaipa kipaumbele kwa hizi rasilimali tulizonazo hatutazitumia tu hivi *randomly*. Kwa mfano Arusha, Manyara, pamoja na Moshi wenyewe wameshakwenda kwenye *elimination*. Kwa hiyo tutaongeza nguvu sana *ku-adress* haya masuala ya Mikoa ambayo bado maambukizi yapo juu. Tutashirikiana pia na Wizara ya Mazingira kwa sababu suala hili ni mtambuka kuhakikisha kwamba tunaifikia hii Mikoa tushushe kama Manyara, Arusha na Moshi. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kaa hapo hapo. Sasa hivi kuna mtindo watu wanapita majumbani wanamwaga

dawa kwa barua za Halmashauri asilimia kubwa ya dawa hizo ni maji. Hilo nalo mlidhibiti.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nimepokea na nawatumia salamu huko walipo. Tunaanza kuafuatilia leo hii tujue walitumwa na nani na kiwango cha ubora wa hizo dawa wanazomwaga. Nasema waache maana Serikali iko kazini. Ahsante.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa Mbunge wa Igunga.

Na. 434

Kukamilika kwa Chuo cha VETA – Igunga

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha VETA Igunga?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Igunga kama ifuatavyo: -

Chuo cha Ufundisi Stadi cha Wilaya ya Igunga ni mionganii mwa vyuo 29 ambavyo vinaendelea kujengwa. Ujenzi wa Chuo hiki unaendelea vizuri na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai, 2021. Aidha, mchakato wa ununuzi wa mitambo na zana za kufundishia unaendelea sambamba na ukamilishwaji wa chuo hiki. Ujenzi wa chuo hiki utakapokamilika udahili wa wanafunzi wa kozi fupi utaanza mara moja wakati ule wa kozi ndefu unatarajia kutafanyika ifikapo Januari, 2022. Ahsante.

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza niipongeze Wizara, Waziri na Naibu wake wanafanya vizuri. Mwezi Januari Naibu Waziri alipita pale alifanya ziara na akatoa maelekezo mwezi wa tatu chuo kikamilike lakini nimefanya ziara Jumamosi tarehe 12 changamoto imekuwa ni kwamba fedha zinakwenda kidogo katika kukamilisha huu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment* ya Serikali katika kukamilisha fedha ambazo zitaenda kukamilisha huu mradi na kuanza udahili. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ngassa kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa na kusuasua kidogo katika kupeleka fedha zile za awamu ya mwisho kuhakikisha kwamba tunakwenda kukamilisha ujenzi katika maeneo haya. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, fedha awamu ya mwisho zaidi ya Shilingi milioni 560 tayari zimeshapelekwa katika chuo hiki kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi huo na tutahakikisha kwamba tunasimamia vyema kuhakikisha ujenzi huo unakamilika ifikapo Julai ili vijana wetu wawezee kuanza mafunzo katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa hapo taja jina lako.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naitwa Aloyce Kamamba, Mbunge wa Buyungu.

MWENYEKITI: Haya karibu.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, uhitaji wa Chuo cha Ufundi VETA ambao unawakabili wananchi wa Wilaya ya Igunga unafanana sana na uhitaji wa chuo hicho katika Wilaya ya Kakonko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini Serikali itajenga chuo cha ufundi VETA katika Wilaya ya Kakonko? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kamamba Mbunge wa Buyungu kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuwa na Chuo cha VETA katika kila Wilaya hapa nchini. Kwa hiyo, nilmhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko makini, kwa hivi sasa tunakamilisha ujenzi wa vyuo hivi 29 katika Wilaya hizi 29 nchini.

Baada ya awamu hii kukamilika Serikali tutajipanga vema kulingana na upatikanaji wa fedha tutahakikisha kwamba tunakwenda kujenga chuo katika kila Wilaya hapa nchini. Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila Mbunge wa Kyela.

Na. 435

Ujenzi wa Barabara ya Katumbasongwe - lleje

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE aliuliza: -

Je, ni lini barabara ya kutoka Katumbasongwe hadi lleje kilometra 90.7 itaanza kujengwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ally Anyigulile Mlaghila, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Katumbasongwe – lleje ni barabara ya Mkoa yenye urefu wa kilometra 114.51 inayounganisha Mkoa wa Mbeya na Songwe kuititia Wilaya ya Kyela na Wilaya ya lleje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Katumbasongwe - Kasumulu – Ngana – lleje ipo katika taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina taratibu za ujenzi zitaanza. Aidha, Serikali inaendelea kuihudumia barabara hii kwa kuifanya matengenezo mbalimbali ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka wakati taratibu za ujenzi wa kiwango cha lami zikiendelea. Katika mwaka wa fedha huu wa 2021/22 barabara hii imetengewa Shilingi milioni 141.45 za matengenezo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlangila.

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni barabara muhimu sana kwa ulinzi wa nchi yetu hasa kwa upande wa Tanzania na Malawi, pamoja na hayo kuna barabara muhimu sana ambayo kwa uchumi wa Kyela inafaa ijengwe mara moja.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini barabara ya Ibanda – Itungi – Poti itaanza kujengwa rasmi?

Swali la pili, wakati wa ujenzi wa barabara ya Kikusya – Matema kuna madaraja ya chuma yaliyokuwepo kwenye Mto Lufilyo Nambaka yalitolewa. Je, Mheshimiwa Waziri, kwa sababu ya uhaba wa madaraja na watu wanaotembea kilometra nyingi kufuata daraja lilipo, Serikali haioni kwamba

ni muhimu sasa madaraja yale yarudishwe Kyela ili yapelekwe sehemu zeny e uhitaji za llondo, Ipande na sehemu za pale Ngorwa? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Anyigulile Mlaghila, Mbunge wa Kyela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya lbanda – Itungi – Poti imetengewa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami na naamimi tayari maandalizi yako ili iweze kutangazwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Kyela waiamini Serikali na hata akienda kwenye vitabu vyetu vya bajeti tumeonesha fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili haya madaraja ambayo anayasema. Madaraja haya ya chuma ni madaraja ambayo yanatumika kwa ajili ya kutumika pale panapotokea dharura. Kwa hiyo, madaraja anayoyasema ni kweli yalikuwepo lakini yalishapelekwa Katavi kwa ajili ya koa changamoto ambayo ilitokea. Kwa hiyo, kuititia Bunge lako Tukufu nimuagize Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Mbeya aende akafanye tathmini halafu tuone kama tutapata madaraja sehemu nyingine tuweze kurejesha mawasiliano ili kuwapunguzia adha wananchi amba wanakwenda mbali kwa ajili ya kupata huduma ya usafiri. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tofauti kubwa kati ya miradi ya upembuzi yakinifu wa barabara zetu ukilinganisha na ujenzi, kwa sababu zipo barabara ambazo

zimefanyiwa upembuzi yakinifu tangu mwaka 2012 na bado hazijajengwa.

Je, Serikali haioni kwamba ipunguze miradi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili barabara ambazo zimeshafanyiwa upembuzi yakinifu kwanza zijengwe, kwa sababu haiwezekani mwaka 2012 ifanyiwe upembuzi halafu uje kuijenga 2025 useme kwamba utaijengwa kwa *data* zile zile, ni lazima itabidi ujenge kwa *data* zingine.

Je, huoni kama Serikali inapoteza fedha nyngi?
(*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana nae kwamba tukifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa muda inakuwa ni gharama kwa sabbau itabidi tuje turudie, lakini azma ya Serikali wakati tunafanya upembuzi na usanifu wa kina inakuwa ni kuijenga barabara kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyosema kinachosumbua wakati mwingine ni upatikanaji wa fedha kwa kipindi hicho lakini ni muhimu tukafanya usanifu ili mara tunapopata fedha basi barabara hizo ziendelee kujengwa. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya usanifu na kutafuta fedha. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Iddi.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kwa kuwa tatizo liliopo Kyela ni sawasawa na tatizo liliopo katika Wilaya ya Halmashauri ya Msalala. Je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa barabara inayotoka Busisi – Ngoma,

Ngoma – Nyang’hwale, Nyang’hwale – Chela, Chela – Busangi – Kahama? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi Kassim, Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara anayoisema ya kutoka Busisi – Nyang’hwale na kupita kwenye Jimbo lake ni barabara ambayo tayari imeshafanyiwa usanifu na kinachosubiri ni upatikanaji wa fedha ili barabara hiyo iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi kwa kipindi cha miaka mitano nina uhakika zitajengwa kwa kiwango cha lami kadri fedha itakavyoendelea kapatikana. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 436

Ujenzi wa Barabara ya Tarime - Serengeti

MHE. GHATI Z. CHOMETE aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa barabara ya Tarime hadi Serengeti kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Tarime – Mugumu (Serengeti) ina jumla ya urefu wa kilometa 87.14 ambapo sehemu ya barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 10.7 tayari imejengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 76.44 zilizobaki zimejengwa kwa kiwango cha changarawe. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa daraja la Mara lililopo katika barabara hii lenye urefu wa meta 94 na barabara za maingiliano za daraja hilo zenye urefu wa kilometa 1.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kilometa 25 nje ya kilometa 76.44 zisizokuwa na lami za barabara hiyo imetangazwa tarehe 4 Juni 2021. Taratibu za manunuzi zikikamilika kazi za ujenzi zitaanza mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara hii kwa sehemu itakayobaki kadri ya upatikanaji wa fedha utakavyopatikana.

MHE. GHATI Z. CHOMETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali madogo tu ya nyongeza:

(a) Serikali imetangaza tarehe 4 Juni zabuni je, ni lini sasa kilometa 76 zilizobaki zitafanyiwa kazi? (*Makofi*)

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha barabara hii inaendelea kuitika wakati wote. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Zephania Ghati Mbunge wa Viti Maalum mkoa wa Mara kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwamba ametoa kibali barabara hii imetangazwa inajengwa kwa awamu, kwa kuanzia na kilometa 25 tuna bilioni Sita za kulipa *advance payment* baada ya kumpata mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia swali lake la pili kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mkoa wa Mara kuititia *TANROADS* imetenga shilingi milioni 411 kwa ajili ya kuendelea kufanya maboresho barabara hii hadi hapo itakapokuwa imekamilika. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, sera ya Serikali ni kuunganisha kwa kiwango cha lami barabara za Mikoa na Wilaya na kwa kuwa barabara ya Idete – Iringa ni barabara ambayo inaunganisha Majimbo matatu, Iringa Mjini, Jimbo la Kalenga na Jimbo la Kilolo.

Je, ni lini sasa Serikali itaijenga kwa kiwango cha lami barabara hii kwa sababu kwanza ni ya kiuchumi?

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sera ya Serikali ni kuunganisha kwa kiwango cha lami barabara za mikoa na wilaya. Na kwa kuwa, Barabara ya Idete – Iringa ni barabara ambayo inaunganisha Majimbo matatu, Iringa Mjini, Jimbo la Kalenga na Jimbo la Kilolo. Je, Serikali ni lini sasa itajenga kwa kiasi cha lami hii barabara kwa sababu, kwanza ni ya kiuchumi?

MWENYEKITI: Ahsante umeeleweka. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum maarufu wa Mkoa wa Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara aliyoitaja ni muhimu sana, na mpango wa Serikali ni kuunganisha mkoa na mkoa na wilaya na wilaya.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa niaba ya Serikali, kwamba fedha zikipatikana wakati wowote barabara hizi zote muhimu zitajengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sophia.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itaikumbuka Barabara ya Bujera – Masukulu mpaka Matwebe katika Wilaya ya Rungwe kuweza kutujengea? Mheshimiwa Waziri naomba jibu la Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Mkoa wa Mbeya, wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Rungwe mimi nimefika, na maeneo ya Mbeya kwa ujumla wake; na tumekubaliana kwamba tunapotaka kujenga barabara za eneo hili usanifu wa kina lazima ufanyike kwa sababu ya miundombinu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mbheshimiwa Sophia kwamba, pesa ikipatikana wakati wowote, barabara hii itajengwa kiwango ulioitaja muhimu sana kwa watu wa Rungwe cha lami. Ahsante.

MWENYEKITI: Tuendelee Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma.

Na. 437

Kulinda Haki na Maslahi ya Watumiaji Nchini

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO aliuliza: -

Mihimili muhimu ya uchumi wa soko ni Mamlaka za Udhhibit, Tume ya Ushindani na Mamlaka ya kulinda haki na maslahi ya Watumiaji: -

(a) Je, ni lini Serikali itaunda mamlaka yenyeye nguvu ya kulinda haki na maslahi ya watumiaji nchini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutunga Sheria ya kuwalinda Watumiaji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kumlinda Mlaji/Mtumiaji na inatekeleza jukumu hilo kupitia Sheria ya Ushindani Namba 8 ya Mwaka 2003 (*The Fair Competition Act*). Sheria hiyo ndiyo iliyounda Tume ya Ushindani (*Fair Competition Commission – FCC*) ambayo ndiyo mamlaka ya kuwalinda walaji/watumiaji wa bidhaa na huduma nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Sheria hii, Serikali imekamilisha uundaji wa Baraza la Kumtetea na Kumlinda Mlaji (*National Consumer Advocacy Council*) ambalo litakuwa na jukumu la kisheria kusimamia haki za mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha

taratibu za kuhakikisha Baraza hilo linaanzishwa ili liweze kujitegemea nje ya FCC, ili liweze kufanya kazi zake kwa ufasaha.

Aidha, Serikali inakamilisha maandalizi ya Sera ya Ubora ambayo pia ni muhimu katika kulinda haki za walaji/watumiaji.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inazo sheria mbalimbali za kumlinda mlaji. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Ushindani Namba 8 ya Mwaka 2003, Sheria ya Viwango ya Mwaka 1975, Sheria ya Vipimo ya Mwaka 1982, Sheria ya Usalama Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003, Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Sheria ya Chakula, Madawa na Vipodozi ya mwaka 2003. Chini ya sheria hizo walaji mbalimbali hulindwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Dkt. Ishengoma.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tume ya Ushindani, kama zilivyo mamlaka zote za udhibiti hapa nchini, zina mamlaka ya kimahakama *quasi-judicial organs*. Je, Serikali haioni kuunganisha ushindani na kumlinda mtumiaji zinafifisha dhana nzima ya ushindani na inafifisha dhana nzima ya kumlinda mtumiaji wa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Dhana ya mtumiaji hapa nchini inaanisiwa kwenye sheria mbalimbali ambazo hazina dhana nzima ya kumlinsda mtumiaji na kuakisi haki nane za mtumiaji kama zilizvyoainishwa na Umoja wa Mataifa. Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kutunga sheria, *a standalone law* ya kumlinda mtumiaji wa Kitanzani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli *FCC* au Tume ya Ushindani inasimama kama tume ambayo inahusika kama ya kimahakama, kwa maana ya *quasi-judicial organ* na ndiyo maana katika majukumu yake yale mawili ya kulinda ushindani pamoja na ya kumlinda mlaji tumeamua sasa ile *National Consumer Advocacy Council* ambayo ilikuwa ni sehemu, kama *section* katika taasisi hii ikae sasa *independent* ili sasa tuwe na uhakika kwamba, mlaji anasimamiwa ipasavyo badala ya kuwa chini ya Tume hii ya Ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mionganoni mwa majukumu ambayo tunaenda kufanya, sasa tunataka tuanze kutunga sera ya kumlinda mlaji; na ndani ya sera hiyo sasa tutatengeneza pia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, kama nillivyosema, pia ili kumlinda mlaji maana yake sasa tunataka tuwe na sheria ambayo yenye moja kwa moja itahakikisha inasimamia kumlinda mlaji tu ikiwa nje ya *FCC* ambayo inafanya majukumu mawili ya kusimamia ushindani, lakini pia na kumlinda mlaji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri hapohapo, Mheshimiwa Waziri, hebu tumeni watu wenu kwenye *supermarkets* kubwa, *dettol* sabuni za kuogea zote *fake*. Watu wanalipa pesa nydingi wanatumia vitu visivyo halali na pesa wanazolipa. Chunguzeni *supermarkets* zote, katazame *dettol*. Ukiitia maji *dettol* inakuwa nyeupe, leo ukiitia maji *dettol* inakuwa nyeusi, pamoja na sababu ambazo zimeandikwa majina makubwa, lakini ni *fake*.

Tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwin'juma.

Na. 438

Usafirishaji wa Vipepeo Nje ya Nchi

MHE. HAMIS M. MWINJUMA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaruhusu tena usafirishaji wa vipepeo nje ya nchi ili kuongeza vipato vya wananchi wa Muheza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwin'juma, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 17/03/2016, Serikali ilisitisha biashara ya kusafirisha wanyamapori hai nje ya nchi. Tatizo kubwa liliosababisha maamuzi hayo lilikuwa ni ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu za kufanya biashara hiyo, ikiwa ni pamoja na kutokea wimbi kubwa la utoroshaji wa wanyamapori hai. Vilevile Serikali iligundua matokeo hasi yanayoendelea kujitokeza kwa kuendelea kufanya biashara hiyo ikiwemo kuhamisha rasilimali ya wanyamapori nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali inafanya tathmini ya kina ili kubaini faida na hasara ya usafirishaji wa wanyamapori hai nje ya nchi kwa ajili ya kujiridhisha na biashara hiyo. Baada ya tathmini hiyo Serikali itatoa tamko kwa wadau wa biashara hiyo kuhusu uamuzi uliofikiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwin'juma.

MHE. HAMIS M. MWINJUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, na nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kwamba, kwa vile imeshathibitika kwamba jambo hili halina madhara yoyote kimazingira na kwenye idadi ya vipepeo, na kwamba kwanza ukiachilia mbali kuongeza vipato vya wananchi lilikuwa linasaidia kwenye idadi ya vipepeo kwa vile kwa kawaida kipepeo anayetaga mayai mpaka 500 kwa njia

zake za kwaida huweza kuzalisha vipepeo wawili, lakini kwa njia hii ya msaada wa wananchi huweza kuzalisha mpaka vipepeo 300.

Je, Serikali haioni kwamba, ilishauriwa tu vibaya kwenye suala hili kwa kutengenisha katika wanyama wakubwa kama chui, twiga na swala na hawa vipepeo wetu na kwamba inatakiwa kurudi nyuma na kutengenisha sasa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa vile ni nchi chache sana duniani ambazo zinaweza kuzalisha vipepeo kama sisi, na ni biashara na utalii mkubwa duniani; Serikali haioni haja sasa ya kuwekeza kwenye kuanzisha utalii wa vipepeo, ili kuongeza vivutio vya utalii nchini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hamis Mwin'juma, Maarufu kama "Mwana FA", kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Hamis Mwin'juma, lakini pia nimpongeze sana kwa kuendelea kusimamia eneo hili la wanyamapori hai, lakini nimpongeze pia kwa kuendelea kupigania wananchi wa Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo ameshauri Mheshimiwa Mwinjuma, kwamba Serikali inawezekana ilishauriwa vibaya. Nimtoe wasiwi kwamba Serikali iko makini na Serikali iko kazini na ina wataalamu wa kutosha. Suala hili limekuwa likichunguzwa na wataalamu mbalimbali. Muhimu ni kuangalia kipi faida na hasara ambayo inaweza ikapata Serikali. Tunapoendelea kuhamisha wanyama mbalimbali kutoka ndani ya nchi kupeleka nje ya nchi ina maana tunazidi kuuwa utalii wa hapa Tanzania. Hata hivyo nimtoe wasiwasi,

kwamba suala hili tunaendelea kulifanyia tathmini, tutachakata kuangalia faida na hasara ya eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze pia, kwa kuendelea kuhamasisha utalii kuitipia vipepeo ambavyo amevitamka yeye mwenyewe. Kwa hiyo, kama kweli tutaanzisha utalii wa vipepeo haina haja sasa hata kuendelea kuvitoa hivi vipepeo viende nje ya nchi kwa sababu tunapoendelea kuvitoa tunauwa soko la utalii wa ndani.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jesca.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niulize swali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia wazawa katika kukuza utalii wetu hasa *cultural tourism*? Kwa mfano kutumia wazee wa kimila kama wazee wa kihehe ambaao walianza kutunza Mbuga ya Ruaha wakati wa *Chief Mkwawa* na kutumia wazee wengine kama Wamasai, ili kuhakikisha kwamba utalii wetu unakua, kwa kuwa wao wenyewe wanakuwa tayari ni kivutio?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jesca, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sasa hivi Serikali ina mpango wa kutumia watu maarufu, wazee wa kimila kama ambavyo amewaaishwa Mheshimiwa Mbunge na watu maarufu wakiwemo wasanii ambaao tutawatumia kama mabalozi wa hiyari. Kwa hiyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, suala hili Serikali inalishughulikia; na tulishukuru sana Bunge hili limetupitishia bajeti nzuri ambayo sasa mwaka wa fedha 2021/22 tunaenda kutekeleza maeneo yote haya. Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Katani Ahmad Katani.

Na. 439

**Hitaji la Kituo cha Uhamiaji – Kijiji cha Chikongo,
Tandahimba**

MHE. KATANI A. KATANI aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Uhamiaji katika Kijiji cha Chikongo kilichopo Kata ya Moreha Wilayani Tandahimba ambacho huduma ya *Visa* kwa Watanzania waendao Msumbiji hutolewa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA K.n.y.
WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Katani Ahmed Katani, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chikongo ni eneo lilioko pembezoni mwa Mto Ruvuma katika Wilaya ya Tandahimba ambayo kwa upande wa Msumbiji inapakana na Wilaya ya Nangale. Kwa sasa huduma za uhamiaji katika Kijiji cha Chikongo zinapatikana kuititia ofisi ya Uhamiaji ya Wilaya ya Tandahimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuititia Idara ya Uhamiaji itafanya mashauriano na nchi ya Msumbiji kuanzisha kituo cha uhamiaji katika eneo la Kijiji cha Chikongo kilichopo katika Wilaya ya Tandahimba ili kuendelea kutoa huduma kwa Watanzania waendao nchini Msumbiji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Katani.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Serikali nadhani haielewi Swali langu la Msingi. Chikongo tunaposema upande wa pili wa Msumbiji, wenzetu tayari wanacho kituo cha uhamiaji, upande wa Tanzania ndio hatuna kituo cha uhamiaji: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali languni kwamba, ni lini Serikali itapeleka kituo cha uhamiaji upande huu wa Tanzania? Si suala la mashauriano na Msumbiji kwa sababu, Msumbiji wao tayari wanacho kituo cha uhamiaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili. Je, wenzetu wa Msumbiji tunapopeleka bidhaa kule wana *custom* pale, wana shughuli zote pale. Upande wa Tanzania wananchi wetu wakileta bidhaa wanapata shida kwa sababu hawana *custom* hapo, *TRA* hawapo pale. Tupe kauli ya Serikali, ni lini mtajenga kituo cha uhamiaji pale na kupeleka huduma nyingine zote za msingi ili Watanzania wapate huduma kwa urahisi pale?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Katani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Katani kwa kazi nzuri anayoifanya; na ndiyo maana wananchi wa Tandahimba walimuamini na kumpa nafasi ya kuwawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwa ujumla wake kwamba lengo la Serikali ni kudhibiti maeneo yote ya mipaka yetu, ikiwemo uingiaji wa wageni na utokaji pia wa wananchi wetu. Pia kudhibiti mapato kupitia *TRA*, yako pia masuala ya afya pamoja na masuala ya usalama kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kuhusu maswali yake yote mawili kwa

ujumla. Ni kwamba niwatoe hofu tu wananchi wa Tandahimba, tunaona uko umuhimu. Kituo cha uhamiaji ambacho tunacho kiko makao makuu ya wilaya, ni mbali kidogo na sehemu ambapo wananchi wanavuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Katani, kwamba suala hili tumelichukua. Nitumie nafasi hii tu kumuelekeza Kamishna wa Uhamiaji atume wataalam pale. Kwa sababu wananchi kama wanagonga *passport* zao ng'ambo wanapoingia; ni muhimu wananchi pia wa Tanzania waweze kupata huduma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hili nalielekeza tu lifanyiwe kazi mara moja na sisi tutaendelea kusimamia kama Serikali kuona wananchi hawapati shida na tunapata manufaa makubwa sana kutoka kwa nchi za majirani kupitia biashara na mambo mengine ambayo yanahusiana na mambo ya mipakani. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kimei.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi ninauliza swali moja ambalo ni, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi kwenye Soko la Kimataifa la Mwika ambalo liko mbali sana kutoka Himo ambako ndiko kwenye kituo cha polisi?

Mheshimiwa Mwneyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjibu Mheshimiwa Kimei, swali lake la nyongeza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kimei, kama ulivyosema, na niseme tu kwamba uko umuhimu wa kuwa na kituo cha polisi. Si maeneo tu haya ya Mwika, lakini maeneo mengi ambayo yanaweza yakawa yanajihusisha na biashara kama ilivyo eneo la Mwika. Nilichukue suala hili ili

tuone upande wa Serikali kulifanyia kazi haraka ili tuweze kuleta manufaa makubwa. Ili biashara iweze kushamiri vizuri tunahitaji kwa kweli kuwa na ulinzi wa kutosha katika maeneo haya. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa maswali yetu yote yamekwisha, sasa ni kipindi cha wageni.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni waliopo Jukwa la Spika; wageni 29 wa Mheshimiwa Spika ambao ni walimu kutoka Mlali - Kongwa, Mkoani Dodoma wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani Richard Mugurumi. Karibuni sana. (*Makofî*)

Wageni 81 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni wanafunzi wanasoma Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*), wakiongozwa na Waziri Mkuu wa Serikali ya Wanafunzi wa chuo hicho Ndugu James Mwijjande. Karibuni sana. (*Makofî*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kutoka *Rahabu Ulcers Herbal Clinic*. Wanatoa matibabu ya vidonda vya turbo, wakiongozwa na Dkt. Rahabu Rugabo. (*Makofî*)

Wageni 24 wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni Madiwani, Wenyeviti na Makatibu wa CCM Wilaya ya Rufiji, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Ndugu Rajabu Mbonde. Karibuni. (*Makofî*)

Wageni 14 wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ambao ni Watumishi wa Mungu kutoka Ushetu, Mkoani Shinyanga, wakiongozwa na Askofu Simon Nkwabi. Karibuni. (*Makofî*)

Wageni watano Mheshimiwa Hussein Bashe Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni wataalam wa Sekta ya Pamba kutoka Mkoani Mwanza wakiongozwa na Balozi wa pamba

nchini Balozi Aggrey Mwanri. Karibu Mzee Aggrey Mwanri, Mzee wa Toronto karibu. (*Makofii*)

Mgeni wa Mheshimiwa Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishati ambaye ni mshindi wa shindano la ubunifu la *NSSF* kutoka Bukoba Mkoani Kagera ndugu Christopher Kaijage, karibu. (*Makofii*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Mary Masanja, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambaao ni jamaa zake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mratibu wa *Miss East Africa* ndugu Mariam Ikoaa, karibuni sana Dodoma. (*Makofii*)

Wageni 32 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambaao ni Machifu Watwale wa Tanzania wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Machifu Tanzania ambaye pia ni Chifu wa Unyanyembe Tabora, Chifu Msagata Fundikira, karibuni. (*Makofii*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Neema Lugangira ambaao ni wadau wa lishe *Shishi Food*, kutoka Jijiji Dar es Salaam ndugu Zuwena Yusuph (Shilole) na ndugu Rajab Nyangama, karibuni. (*Makofii*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Kassim Hassan ambaao ni ndugu zake kutoka Zanzibar, Ndugu Abdulkarim Ali, Ndugu Soud Haji na ndugu Ahmada Dau. (*Makofii*)

Wageni 21 wa Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ambaao ni wanawake wajasiriamali wauza mbogamboga kutoka Tabora Mjini wakiongozwa na Ndugu Zena Mazinge. (*Makofii*)

Wageni 26 wa Mheshimiwa Dorothy Kilave ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu Dodoma wanaotoka Temeke Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Clepina Robert. (*Makofii*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Jacqueline Kainja ambaao ni Wafamasia wa sekta binafsi kutoka jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Gervas Mwala, karibuni. (*Makofii*)

Wageni 18 wa Mheshimiwa Muhamramy Mkenge amba ni Madiwani wa Halmashauri ya Bagamoyo Mkoani Pwani wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri, Mheshimiwa Mohamed Usinga. (*Makof*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Kassim Haji amba ni ndugu zake kutoka Zanzibar; Abdulkarim Ali, ndugu Soud Haji na Ndugu Ahmad Dau, hawa nafikiri walishatangazwa.

Wageni 25 wa Mheshimiwa Samwelii Hhayuma amba ni wafanyabiashara kutoka Hanang Mkoani Manyara wakiongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Clementine Fiso. (*Makof*)

Wageni Wawili wa Mheshimiwa Joseph Tadayo amba ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam, Mke wake Ndugu Elita Joseph na binti yake Ndugu Rebecca Tadayo, karibuni. (*Makof*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Nashon Bidyanguze amba ni wapiga kura wake kutoka Kigoma Kusini wakiongozwa na Mwenyekiti wa UV-CCM ndugu Elias Raphael. (*Makof*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Charles Kajege amba ni Watendaji Wakuu wa Shirika la *Project Concern International*/kutoka Musoma Mkoani Mara wakiongozwa na Ndugu Nicolas Ford. Karibuni. (*Makof*)

Wageni 20 wa Mheshimiwa John Sallu amba ni Wanachama wa Mkata *Fitness club* kutoka Handeni Vijijiini wakiongozwa na Hussein Saguti. (*Makof*)

Wageni saba wa Mheshimiwa David Kihenzile amba ni Mameneja wa *CRDB* kanda zote nchini wakiongozwa na Meneja wa *CRDB* kanda ya kusini ndugu Dennis Mwaloka. (*Makof*)

Waheshimiwa tuna wageni hapa kutoka Benki ya *CRDB* amba ni Mameneja kanda, tunae Boniventure Paul

Kiungo, Chabu Mishwaro, Badru Idd Luganzila, Said Pamuyi, Lusingi Sitta, Chiku Issa, Dennis Moleka, Jenipher Tondi, mmesikia juzi Rais amesema mpunguze riba. (*Makof!*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Maimuna Mtanda ambao ni wadogo zake kutoka Newala Mtwara wakiongozwa na Ndugu Chihindi Juma. (*Makof!*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Kenneth Nollo ambao ni rafiki zake kutoka Bahi Jijini Dodoma, Ndugu Job Mwakalambo na Ndugu Costancia Maduma. (*Makof!*)

Katibu!

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Mapendekazo ya Serikali kuhusu Makadiryo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano ya Bajeti tunaanza na Mheshimiwa Vuma Augustine Holle, jiandae Mheshimiwa Riziki Said Lulida.

MHE. VUMA A. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza kabisa kwa uzito wake, nipende kuchukua fursa hii, Mwenyekiti jana Mkoani Mwanza kulitokea tukio zuri la kihistoria na la kuenziwa. Mheshimiwa Rais wetu mpendwa alipata muda wa kukaa na vijana wa nchi hii kutoka maeneo mbalimbali Mkoani Mwanza, akaongea nao kwa kirefu sana, lakini alitumia muda wake mwingi kuwaeleza imani kubwa aliyonayo kwa vijana

wa nchi hii, lakini fursa ambazo zipo Serikalini, akatutia moyo vijana wa nchi hii lakini akatuhakikishia ulinzi katika harakati zetu zautafuta maisha na kujenga nchi kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kadi nyekundu ilitoka jana pale pale kwa watu ambao walionekana kwamba wanabeza juhudzi za vijana za utafutaji. Sasa kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais lakini nashawishika kuwaomba vijana wenzangu Tanzania kote, kwamba ni wakati muafaka sasa kama ambavyo tulikuwa tunafanya kuhakikisha kwamba tunamlinda Mheshimiwa Rais wetu na kumtetea katika maeneo yote. Kwenye mitandao, kwenye matukio mbalimbali, tuhakikishe kwamba tunamlinda na kumtetea Rais wetu kwa kuwa anayo maono makubwa sana kuhusu vijana wa nchi hii.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa

MWENYEKITI: Taarifa.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe Mheshimiwa taarifa sio ombi ni amri kwa vijana. (*Makof*)

MHE. VUMA A. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa naipokea. Vile vile nipende kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan wiki iliyopita nilipata taarifa kwamba ametupatia Jimbo la Kasulu Vijijini shilingi Milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za vijijini. Fedha ambazo nimeshajadiliana na meneja wangu wa TARURA kwamba tutachonga barabara ya kutoka Kata ya Kigembe kwenda mpaka Kata ya Rungwe mpya kwenda kufungua maana yake Tarafa ya Buyonga na Tarafa ya Heruchini. Kwa kweli tunamshukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hili ninamshukuru sana pia kwa shilingi milioni 600 za Ujenzi wa shule ya sekondari ambazo anatupatia Kasulu Vijijini fedha ambazo tumekubaliana tunakwenda kujenga kwenye Kata ya Karela, kata ambayo ina shule tatu za msingi sasa tunataka kuwapa

shule ya sekondari ambayo ni zawadi kutoka kwa Mama Samia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Mwigulu na timu yake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya kuandaa bajeti. Ni bajeti ambayo imeonesha vyanzo mbadala vyataga mapato ukiachilia mbali ambavyo tumekuwa tukiendelea kubana walipa kodi kwa maana ya watumishi na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshauri au kumwongezea yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la watengenezaji wa matrela ya malori haya, mwanzo au miaka ya nyuma kidogo tulikuwa na watengenezaji zaidi ya 10 nchi hii, lakini leo hii wamepungua wamebakira watatu, kama sikosei tunao *Super doll, AM* sijui na mwingine yupi, lakini ziko kama tatu. Kwa nini wanapungua na hawa wanaweza wakafunga viwanda vyao ni kwa sababu zipo nchi ambazo watu wanaenda kununua huko matrela na kwa nini wanaenda huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakwenda huko kwa sababu *manufactures* wa huko wa China nadhani kama kama sijakosea na Uturuki, wanapewa *export levy* na nchi zao asilimia 20 ya *FOB*. Sasa wanakuwa na uwezo wa kuuza matrela kwa bei ndogo sana, sasa mtu akinunua kule akija kwa bei ndogo, akija hapa Tanzania analipa *import duty* yaani asilimia 10. Sasa ukiangalia mtu akinunua gari za kutembelea *IST* kwa mfano, akija hapa Tanzania analipa *import duty* nadhani asilimia 20 sijui 25. Wakati huyo mtu hana mpinzani, hakuna mtu ambaye anatengeneza magari hapa Tanzania kwa maana *IST* na gari nyingine, lakini matrela haya ambayo wapo watengenezaji wa Tanzania wapo hapa Tanzania, unashangaa wanatozwa kidogo na hatimaye viwanda vyetu vinaendelea kupata wakati mgumu kwa sababu ushindani wa bei unakuwa ni mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, hapa kuna chanzo kingine cha fedha moja tuongeze *import duty* kwenye matrela haya iende kuwa sawasawa na gari zingine tu za kawaida za kutembelea angalau asilimia 20. Hii italinda viwanda vyetu na hawa watengenezaji wa ndani na lazima wataongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio ya kwetu tu yapo mengine mengi matrela ambayo yanapita hapa kwetu kwenda kwenye *land locked countries* na wenyewe wanalipa asilimia 10 hapo *import duty*. Kwa hiyo tunayo nafasi ya kungeza fedha, tunayo nafasi ya kulinda viwanda vyetu, tunayo nafasi ya kufanya jambo hili ili kuongeza fedha katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mwanya mwingine nataka nimshauri Mheshimiwa Mwigulu na timu yake, Kasulu sisi tunao walipa kodi wachache kwa maana ya watumishi ni wachache lakini na wafanyabiashara ni wachache. Hata hivyo, ipo fursa, tulianzisha miaka mitano iliyopita. Sisi kule kwetu baada ya Tanzania kuingia kwenye uchumi wa kat, Watanzania wa Kasulu wale wananchi wa Kasulu hawaendi tena kufanya kazi za mashambani, wanaofanya kazi za vibarua vya mashambani idadi yao imepungua. Sasa pale mara nyingi wanatumia watu kutoka nchi ya jirani ya Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu hakuna utaratibu ambao ni rafiki wale watu wanaotoka Burundi wanakuja na ni maarufu wako Kasulu. Ukitafuta *data* kutoka kwa watu wa *Immigration* Kasulu watakambia. Yako maelfu ya watu wanatoka Burundi kuja kufanya kazi za mashambani. Sisi baada ya kuingia uchumi wa kat, lakini pia shule za kata zikajengwa, watu wa Kasulu awanaenda kusoma shule na wakimaliza shule wanaajiriwa, wengine wanajajiri, wengine wanaenda mikoani kutafuta Maisha. Kwa hiyo ule utaratibu wa watu wa Kasulu kwenda kufanya kazi ya vibarua mashambani umepungua. Kwa hiyo *manpower* ambayo tunaitegemea sasa hivi ni nchi ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulianzisha utaratibu, ilikuwa miaka mitatu iliyopita, tukamshauri Waziri wa Mambo ya Ndani tuanzishe kituo kinachoitwa *season immigrant pass* ambayo akija hapa mtu wa Burundi atawenza kulipia Sh.30,000, aliyemleta atalipa Sh.60,000. Hawa watu ni wengi kuliko wafanyabiashara na watumishi wa Kasulu, hapa kuna fedha nyngi kuliko kodi ambayo tunaikusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana sana Serikali ilitazame hili kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani. Mchakato ulishaanza nadhani Mheshimiwa Kangi Lugora aliusaini wakati ule, naomba tuuendeleze, kuna fedha nyngi sana hapa kuliko ambazo wanawabana wafanyabiashara. Juzi nimesikia, mpaka wafanyabiashara wamegoma kwa sababu wanakamuliwa Kasulu pale mpaka inakuwa ni *too much*, wamegoma. Akaenda Kamishna wa *TRA* kurekebisha mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, hapa kuna chanzo kingine cha fedha, nyngi sana mamilioni ya shilingi kutoka Wilaya ya Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe jambo moja tu iko miradi inaendelea kwetu Mradi wa Barabara kutoka Buhigwe-Kasulu, Kasulu kwenda mpaka Nyakanazi. Ule mradi *speed* yake tunashukuru ipo vizuri, lakini iko miradi ya *bonus* ambayo tuliambiwa inakuja na hiyo barabara. Kwangu pale tuliahidiwa kujenga hospitali lakini na gari la wagonjwa ambayo ni zaidi ya bilioni mbili na milioni 400.

Ukienda Buhigwe, ukienda Kasulu Mjini wana ya kwao, ukienda Kakonko kwa ndugu yangu Mheshimiwa Kamamba yapo, ukienda Kibondo kwa dada yangu yapo, tunataka hii miradi sasa ianze kuletewa fedha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iletwe hela kwa sababu tuliambiwa kwamba utekelezaji wa ujenzi wa barabara utaendana na miradi hii ni mabilioni ya shilingi ambayo kama fedha zikitolewa kwa wakati Mkoa wetu wa Kigoma unakwenda kunufaika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, Mheshimiwa Seif Gulamali kiongozi wa Klabu ya Yanga kutokana na mabadiliko ya Rasimu ya Katiba ya Klabu ya Yanga leo anawaomba washabiki, wapenzi wa Klabu ya Yanga muda wa saa mbili usiku wakutane hoteli ya Chako ni Chako kwenda kujadili mabadiliko hayo. *Sorry siyo Chako ni Chako ni Morena, wakutane Morena Hoteli saa mbili na Viongozi Wakuu wa Yanga watakuwepo.*

Mheshimiwa Riziki Lulida, jiandae Mheshimiwa Polepole.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipatia hii nafasi. Vile vile nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametujalia sisi hapa angalau kupata uhai na afya njema, tunasema ahsante Mungu. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi anayoifanya kama mama mwenye upendo kwa kuhakikisha maendeleo ya Tanzania yanapatikana na juhudi kubwa anazozifanya na sasa hivi hata sisi akinamama tunapata nguvu kuwa tunaye Jemedari wetu ambaye anapambana na uchumi wa nchi yetu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitazungumzia upandw wa Bandari, katika njia kuu nne za uchumi mojawapo ni bandari. Toka enzi ya ukoloni walifanya utafiti mkubwa sana wa kuona mafanikio ya bandari zetu hasa Bandari ya Mtwara, Bandari ya Tanga na Bandari ya Dar es Salaam; nitajikita katika Bandari ya Tanga na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona leo hizi bandari zikiwa zimeachwa hazina kazi ya kufanya wakati tunahangaika na mizigo katika bandari hii ili kuleta pato na kodi kubwa katika uchumi wa nchi yetu tutaanzia na bandari wa Mtwara, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutoa tamko kuwa Korosho zote zinazotoka Mikoa ya Mtwara na Lindi zinakwenda katika Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mafanikio makubwa sana kuifanya ile Bandari itakuwa inafanya kazi lakini vile vile sio zao la korosho tu tunataka hata kahawa ya Mbeya, kahawa ya Ruvuma yote iende katika Bandari ya Mtwara. Nilikuwa naangalia *kilometers* za kutoka Ruvuma mpaka Bandari ya Mtwara. Kutoka Ruvuma-Songea mpaka Mtwara ni saa 8.53 na kutoka Ruvuma au Songea mpaka Dar es Salaam ni saa 14.53 ina maana ni masaa 15 ukiachilia mbali foleni za Dar es Salaam lakini utashangaa kahawa ya Mbinga badala ya kuipeleka Mtwara inapelekwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijaauliza urasimu huu unatokana na nini kuifanya nchi inadumaa kibashara? Si hivyo tu Mkoa wa Mtwara, Mkoa wa Ruvuma tunapakana na nchi jirani zikiwemo Malawi, Zambia pamoja na Kongo *DRC*. Mizigo ya Kongo *DRC* imehama kutoka katika Bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya urasimu, lakini tujulize kwa nini kuwepo kwa urasimu wakati kuna eneo ambalo ni karibu Bandari ya Mtwara ambayo katika miaka ya nyuma ilikuwa inafanya kazi kubwa sana na ilikuwa inaheshimika kwa watu, ilikuwa iko *busy*, lakini kwa urasimu uliokuwepo Dar es Salaam, kwa sintofahamu iliyokuwepo Dar es Salaam wameifanya bandari ya Mtwara kuwa *dormant*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ufuta unatoka Nanjilini, ufuta unatoka Newala unakuja Dar es Salaam, lakini yote ni bishara tu kutaka kuleta *mileage* na kumkandamiza mkulima katika zao la korosho zao la ufuta, zao la kahawa zao la *cocoa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hayati Rais Mkapa alianzisha *Mtwara Corridor* kuhakikisha kuwa mazao yote ya Mkoa wa Katavi, Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Lindi na Mtwara yote inatumia Bandari ya Mtwara. Kumetokea kidudu gani? Ameturoga nani mpaka kuifanya hii bandari isifanye kazi? Kutokana na urasimu, tunaona leo nchi zote za jirani zimekimbia Beira Mozambique. Beira ukiangalia inapakana na *South Africa*. Hivi jamani ifikie mahali tubadilike Watanzania, tusiendelee kulalamika. Tunahitaji mifumo ambayo watu wanataka kuileta Tanzania yenye maendeleo

ili maendeleo haya yaonekane. Wenzetu wale waliokwenda kule, hawakwenda hivi hivi, kuna vitu tumewafanya ambavyo havikuwafurahisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaona mkonge unatoka Tanga unapelekwa Dar es Salaam; kahawa ya Kilimanjaro inapelekwa Dar es Salaam; mazao ya Babati Mkoa wa Manyara yanapelekwa Dar es Salaam; Tanga iko wapi? Hivi leo tunazungumza Bandari ya Tanga haina mapato, siyo kwa kuwa haina mapato, Dar es Salaam pana ubadhirifu mkubwa, pana urasimu mkubwa mpaka umeifanya Bandari ya Dar es Salaam kuonekana kama ni bandari ambayo haina hadhi na heshima kwa nchi hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri wa Fedha akae na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, tujilize maswali mengi, kwa nini inatokea hiyo hali? Tuna Kamati zetu za Bunge; Kamati ya Miundombinu, Kamati ya Bajeti, tuachane na masuala ya kukaa mezani, twende kwenye *site*. Unda tume itakayoonyesha kuwa inataka kuisaidia bandari. Leo bila kuwa na uchumi haiwezekani. Tunapata aibu kubwa, wenzetu wanatujadili katika Bunge letu, wanasikiliza maoni yetu, wanayafanya kazi. Sisi tunakaa humu ndani tunaongea sana, tunatoa mawazo makubwa sana Wabunge, mawazo yetu hayafanyiwi kazi, matokeo yake ni urasimu. Urasimu huu umetufanya tuwe katika uchumi wa kat, lakini ilibidi tuwe katika uchumi mkubwa sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungukwa na nchi ambazo wakiitumia bandari hizi nyiningine, tutatoka kiuchumi, lakini tuko wapi? Tunadhalilika, tunaaibika kwa ajili yetu wenyewe kwa sababu hatujipangi. Huwa nafika mahali najuliza, hivi watendaji hawa wa bandari hawaoni bandari ya Mtwara kama ni bandari nzuri? Bandari ambayo ina kina? Nataka nijue kwa nini tunapata hasara na bandari? Mtwara tunakosa ajira kwa sababu hakuna kazi inayofanyika Mtwara. Ajira hamna. Tunakosa ajira Tanga; tungelufua uchumi mkubwa sana katika mikoa hiyo miwili; Tanga na Mtwara na majirani zao wote wangeondoka kiuchumi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Mheshimiwa Waziri atakapotaka ku-*wind* aniambie kama majibu hayana maana nataka nichukue shilingi mnijibu hapa kuna nini? Wanasema sababu za msingi kwamba hakuna makasha. Hivi kweli tumebinafisha *section* ya *container terminal* tumewapa *TICTS*, kwa nini *TICTS* anaing'ang'ania Dar es Salaam? Kama kazi imemshinda kwa nini asije kutuambia? Tunajikuta tumekaa, makontena yamefika pale yanatolewa, rushwa zote ziko katika Bandari ya Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda muafaka sasa hivi, tukitoka hapa tuwe na muda maalum maana yake hatuna *time frame* kuwa tukitoka hapa tuiangalie Bandari ya Mtwara, tuiangalie bandari ya Lindi na Kamati zote mbili hizi ziende katika eneo. Mimi sitoi amri maana amri anayo kit, lakini naona kabisa tuko katika muflisi mkubwa na tukiendelea hivi wageni wetu wote majirani zetu watahama katika bandari hizi na uchumi wa bandari yetu utatokomea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye *issue* yangu ya pili ya viwanda. Tumevifunga viwanda kwa muda mrefu, hakuna maneno yanayozungumzwa humu ndani. Leo tunangojea kuletewa mafuta kutoka nje. Jiulize mbegu za pamba zinazolimwa katika mikoa ya kanda ya ziwa zinafanya kazi gani? Vile viwanda kwa nini mnavifunga mpaka leo? Kwa nini havifunguliwi? Tunajikuta tunaenda kukaa bandarini, kungojea mafuta kutoka nje, aibu hii kwa nchi hii itaisha lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Mtaka ameonyesha uzalendo wa hali ya juu sana kutaka kufufua zao la Alizeti. Nami kama mwanamke na wanawake wote Tanzania nzima tumuunge mkono Mheshimiwa Mtaka, wanawake wote Tanzania nzima tulime angalau eka mbili za alizeti ili kuhakikisha aibu hii ya kuagizia mafuta nje itokomee kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ni-*declare interest*, mimi mwenyewe ni mlimaji wa alizeti. Nalima alizeti, Lindi inastawi alizeti, tukitoka hapa ni kwenda Lindi kumuunga

mkono Mheshimiwa Rais. Baada ya miaka miwili Tanzania hii hakuna tena kuagizia mafuta ya chakula kutoka nje. Mafuta ya chakula yatoke hapa hapa, kila Mbunge atoke hapa akiwa na neno moja; tunakwenda kulima Alizeti. Hakuna tena Mbunge kwenda kule, hapana; aonyeshe mfano; hawa Wabunge wote waonyeshe mfano, kila mmoja awe na eka tano tano katika eneo lake, alime Alizeti. Hii isiwe hoja ya Mheshimiwa Riziki, iwe hoja ya Kitaifa ili tukitoka hapa tuwe na *legacy*.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. RUZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Polepole halafu ujiandae Mheshimiwa Chaurembo.

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Nami naomba niungane kwanza na Wabunge wenzangu kuunga mkono kazi nzuri ambayo inafanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kupeleka maendeleo kwa watu wetu wa Tanzania.

Kwa upekee mkubwa sana, napenda kumpongeza kwa dhati mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa matukio makubwa ya kihistoria ambayo ameyafanya katika ziara yake ya Mwanza kwa siku tatu mfululizo. Hapa napenda kuweka misisitizo katika uzinduzi na ufuatilaji wa miradi mikubwa ya kimkakati itakayokwenda kubadilisha maisha ya watu wetu Watanzania na hasa katika kanda ya ziwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameshuhudia utiwaji saini mikataba mitano ya ujenzi wa meli kubwa katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na bahari ya hindi. Meli hizi, katika uchumi kuna njia kama tatu za usafiri;

ya kwanza ni usafiri wa maji; pili ni usafiri wa reli; tatu ni usafiri wa barabara; nne ni usafiri wa ndege. Zimepangika hivyo kwa maana ya unafuu wa njia za usafiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira njema ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuwekeza zaidi katika usafiri wa kwenye maji, unadhihirisha mwelekeo mzuri wa kusafirisha mizigo mikubwa kwa bei nafuu; na hapa ninaangazia soko lote la Afrika Mashariki. Tutaweka *wagon ferry* pale yenyewe kubeba tani 2,800 maana yake hiyo ni sawasawa na kuingiza treni kama tatu hivi za mizigo zitakazotoka Tanzania kwenda Kenya au kwenda Uganda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile itajengwa meli ya kubeba uzito hivyo hivyo wa tani zaidi ya 2,800 ambayo sasa ninaona makaa ya mawe kutoka kusini mwa Tanzania mpaka bandari ya Mtwara kama alivyosema pacha wangu pale, yatatemebea kwa maji kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam na mpaka *Tanga Cement* badala ya kutumia usafiri wa barabara ambao unaghanimu nchi yetu fedha nyingi kwa kufanya *routine maintenance*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuweka jive la msingi la kuzindua ujenzi wa reli ya kutoka Mwanza mpaka Isaka, reli ya kiwango cha Kimataifa, *Standard Gauge Railway*. Hapa nataka nimtie moyo kwamba akifika Isaka atusaidie kutafuta fedha akamilishe kipande kutoka Isaka mpaka huku Dodoma; na tutoke Dodoma mpaka Tabora - Kaliua hiyo mpaka Kigoma na tukitoka Kaliua twende mpaka Mpanda, tukitoka Mpanda twende mpaka Kalema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kupeleka meli mpaka Kalema ni kwasababu tayari ameshaweka meli pale, itaanza kujengwa hivi karibuni na tutapitisha kwenye bajeti hii. Maana yake, meli itakayokuwa inabeba mizigo katika Ziwa Tanganyika yenyewe zaidi ya tani 2,800 itatoka Bandari ya Kalema itakwenda Bandari ya Kalemii upande wa *DRC* Kongo na huko ndugu zetu wale ambao hawana masoko sasa hivi, watatumia masoko yetu ya dhahabu katika eneo

la Kalema na mizigo ya mbao. Kwa hiyo, meli italeta hapo Kalema tutabeba na *Standard Gauge Railway* na italetwa mpaka Dar es Salaam kwa kwa ajili ya kupeleka ng'ambo ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda ifahamike kwamba reli tunayoitumia sasa hivi ni *narrow gauge*, inaweza kubeba ujazi kama wa tani 1,200 hivi. Pia reli ya *TAZARA* nayo inabeba kama 1,200 mpaka 1,400 hivi. Kipindi fulani tumezungumza na balozi ya nchi ya kimaghari sitamtaja hapa, alisema "*The East Africa sub-region is too small to support two standard gauge railways,*" akimaanisha Afrika Mashariki uchumi wake ni mdogo sana ku-support *Standard Gauge Railway* mbili kwa maana ile ya Kenya na hii inayojengwa hapa Tanzania. Yule hakuwa na dhamira njema na alikuwa muongo. Kwa sababu sijamtaja nina hakika sijakosea sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukiwa na mzigzo wa tani 50 Mbeya au Kapirimposhi, Zambia unataka kuuleta Dar es Salaam, itakuchukua zaidi ya miezi sita kuusafirisha na wakati huo utakuwa umeshakosa masoko huko mbele ya safari. Kwa hiyo, kujenga *Standard Gauge Railway*, ndio njia muafaka ya kuchagiza na kuchochaea ukuaji wa kiuchumi katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia kazi kubwa ameifanya alipotembelea daraja la Kigongo, Busisi. Jana Mheshimiwa Kanyasu alisema vizuri sana kwamba wale ambao wamekuwepo pale wanaweza wakaelewa tatizo lillolokuwepo sasa hivi la kutumia vivuko vya maji. Wakati mwingine foleni pale ni masaa matatu kuvuka, lakini sasa tunabadilisha maisha ya watu kwa kuvuka kwa dakika nne tu. Hilo ni jambo kubwa sana katika ustawi wa maisha ya watu wetu wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ningependa kusema baada ya pongezi, niendelee kumpongeza pia Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan ambaye alikuwa Makamu wa Rais wa Awamu ya Tano. Yapo

mambo yaliyofanyika mwaka jana 2020 ambayo ni vizuri tukayafahamu ya kwamba mama yetu ndiye alikuwa ndiye mshauri mkuu wa Rais wa Awamu ya Tano. Mafanikio yale hatuwezi kumtenganisha nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nieleze jambo moja. Mwaka 2020 dunia ilikumbwa na janga la *Corona* na Tanzania iliamua kutoka na suluhisho lake la ndani la kukabiliana na *Corona*. Nakumbuka Serikali ilitoa maelekezo kwamba tufanye mambo makubwa matatu; moja, tumwombe Mungu; pili, tuzingatie ushauri wa wataalamu wa afya na Serikali; na tatu, tuendelee kuchapa kazi. Hakufungiwa mtu ndani hapa, wala hatukuweka *measures* ambazo ni gandamizi na zinarudisha watu wetu nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda ieleweke kwamba Ndugu Bashiru yuko hapa, Katibu Mkuu Mstaafu, mwaka jana, 2020 alitoa maelekezo kwamba humu ndani msitoke, mwendelee kujadili mpaka mpitishe bajeti, hakuna cha *Corona*; na mlipitisha na wengine tumewakuta kipindi hiki. Hakuna sababu ya kuogopa jambo hili. Mwaka 2020, kwa mbinu tulizotumia hapa nyumbani, wakiwemo ndugu yangu hapa, alitoka na ile dawa moja inaitwa Bosnia na nyingine nyingi tu; na Covid-19 na akina nani, zimefanya maisha yamekwenda vizuri kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusisitiza ni kwamba nchi nyingine zote walitumia mbinu zilizolekezwa na ndugu zetu wa Magharibi. Nikwambie, wote walitumia mbinu za Magharibi waliharibikiwa vibaya mno. Hizi taarifa siyo longo longo, ni taarifa za kiutafiti na ziko. Nitatoa mfano ambao ni halisi. Nchi zinazotuzunguka, ninyi mnafahamu, zilitumia mbinu za kimagharibi kukabiliana na ugonjwa wa *Corona*. Wote wali-experience negative growth mwaka 2020 by end of December. Ni Tanzania peke yake iliyotumia local solutions iliobaki na uchumi chanya, kwa takwimu za Benki ya Dunia na kwa takwimu zetu za NBS. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali, yako mambo tulifanikiwa sana mwaka 2020, msyaache, tuyatumie

mwaka huu pia kupiga hatua kwa maana hiyo. Bajeti ambayo tunakwenda kuipitisha hapa ilioletwa na ndugu yetu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa maelekezo ya mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, imepokelewa vizuri sana na Umma kwa sababu inakwenda kufanya mkate mdogo kuu-share na watu wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu, tunapo-share mkate, ni vizuri tukajiwekea utaratibu mzuri wa kusimamia nidhamu ya makusanyo na matumizi. Tusipofanya hivyo, tutaumaliza mkate na tusiweze kuwekeza mkate mwingine na kuifanya dhamira njema ya mama yetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan isifike. Sisi tuko hapa kama askari wake wa mwamvuli kuhakikisha ya kwamba tunafika huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haraka haraka nitoe rai pia kwa Wizara ya Fedha, hawa wanaoitwa *micro, small and medium enterprises* ulimwenguni ndiyo wana-constitute asilimia 90 ya chumi zote. Hapa Tanzania tuwawezeshe zaidi, ndiyo walipa kodi. Mpaka takwimu za mwaka 2010 ambazo ndiyo tunazo, ziko zaidi ya *micro, small and medium enterprises* kama milioni tatu na zinamilikiwa na watu 2.7 million.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa hapa walipa kodi ni milioni tano, kama tukiwajengea mazingira mazuri ya kuweza kupata fedha, mitaji na mikopo nafuu; nami nakumbuka kulikuwa kuna maelekezo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nina uhakika katika majumuisho litawekwa sawa, kwamba ile mifuko yote ambayo inatoa fedha hapa nchini inakaribia 20 haisomani, haitambuani na hairipoti kwa wakati mmoja. Ijumuishwe ili hilo fuko lote la fedha tulisukume kwa wajasiriamali wadogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali, unajua wakati mwingine wala siyo tunachohitaji ni benki hapa. Hapa tunahitaji fuko moja kubwa la fedha ambalo litawenza kusukuma kazi za wajasiriamali wadogo ama kwa kuwapatia fedha au kwa kuwapatia *guarantee* kwa maana hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie jambo moja hapa. Sasa tupo katikati ya kipindi kingine tunaambiya *Corona* inaendelea. Rai yangu ni kwamba Wizara ya Afya; hapa mimi ningepeleka Wizara ya Afya zaidi na Wizara ya Fedha. Ilani ya uchaguzi imeeleza katika fungu la 84 kwamba lazima tutengeneze kiwanda cha kimkakati cha kuchakata mimea dawa. Hatujatenga fedha vya kutosha. Ilani inasema kuanzisha kituo kikubwa cha utafiti na uchunguzi wa mimea dawa na kuanzisha kiwanda cha kimkakati cha kuzalisha dawa zitokanazo na mimea yetu. Mbona tunatibiwa, tutapona na hizi mimea dawa? Rai yangu, hiki kiwanda msikiweke huku uraiani, mkakifiche sehemu fulani kwenye Kambi ya Jeshi ambako hakuna mtu anaweza kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni vita, wakijua mnatengeneza dawa hapa za kupambana na UVIKO watakuja kutuhujumu, lakini tukikificha sehemu mahsus, hakuna mtu anaweza kufika, tutatengeneza dawa, tutatengeneza tiba, watu wetu watakaoonekana wamepata tatizo, watapewa dawa hizo na hakuna mtu atakuja kutuzingua hapo baadaye. Ila tusipokuwa makini, umeshasikia wakubwa jana wamesema tupewe chanjo billioni moja, tuje kudungwa hapa.

Mheshimwia Mwenyekiti, nilikuwa natoa rai, tuwekeze vya kwetu, *local solutions, for local problem.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chaurembo, halafu ujiandae Mheshimiwa Khadija Hassan Abood

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika Wizara yetu hii. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya toka achukue madaraka haya ya Urais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejadili na kuitisha bajeti mbalimbali za Wizara hapa na michango mbalimbali tumechangia. Ni dhahiri bajeti hii ambayo tunataka tuipitishe hapa imetokana na Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa maana yale yote ambayo tumeyajadili ndiyo yamekuja kujumuishwa katika bajeti ya Wizara hii ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumza sana suala zima la *TARURA* iongezewe fedha. Tumeona katika Bajeti ya Wizara ya Fedha kila Jimbo limepewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya kwenda kukarabati miundombinu ya barabara. Tumechangia kuhusiana na namna gani ambavyo tunaweza tukaongeza fedha kwa ajili ya kuzipeleka *TARURA*. Tumetoa michango mbalimbali, wapo waliogusia kuhusiana na ongezeko la fedha katika mafuta, wapo waliochangia katika miundombinu ya mawasiliano na bajeti iliyosomwa na Waziri wa Fedha, vyote hivyo vimejumuishwa. Tafsiri yangu ni kwamba bajeti hii iliyoletwa hapa imezingatia michango ya Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno mengine bajeti hii ni bajeti yetu, ninachotaka kusema tunazo kazi za kufanya, zipo kazi kwanza kwa sisi Wabunge, kwa sababu yaliyoletwa ndiyo tuliyoyataka, kazi yetu ya kwanza kama Wabunge tunatakiwa twende tukawaelimishe wananchi wetu, twende tukawaelimishe wananchi wetu ili bajeti hii iweze kutekelezeka. Ipo sheria ile ya *property tax*, ambayo ni wajibu wa kila mwenye jengo kuilipia kodi ya majengo, tumekuwa zamani huko tukikusanya kwa kuititia halmashauri zetu, tukaenda *TRA*, lakini ufanisi ukawa mdogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumekuja na mbinu mbadala ya kukusanya kuititia mita za LUKU. Tutakapoenda kuwaelimisha wananchi wetu, nini kinachoenda kutendeka hatutapata tabu kwenye ukusanyaji wa hizi fedha za *property tax*. Madhalani mwenye nyumba anayepangisha nyumba kwa mwezi shilingi 300,000/= tukiweka utaratibu mwananchi akajua kwamba kwenye 300,000/= hii kwa kila mwezi 1,000 ni

kodi ya majengo, kwa hiyo, ni rahisi unaenda kulipa 299,000/
= (*Makofi*)

Mheshimiwa mwenyekiti, ni kama vile kwenye majumba haya yaliyopangishwa yapo mashimo ambayo yanabeba maji taka, maji taka yale ni jukumu la mwenye nyumba kuyanyonya pale yanapojaa. Sasa kwenye mikataba ni namna ya kukubaliana tu. Aidha, kwenye kodi yangu utakata kiasi kadhaa ili shimo likijaa uwezekunyonya au nipe kodi yangu shimo likijaa nitakuja kunyonya, kwa hiyo, kubwa hapa kinachoitajika ni elimu kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bajeti hii sisi ndiyo tumechangia kwa kiasi kikubwa mpaka hapa tulipofikia, ninaamini bajeti hii pia ni yawananchi, kwa sababu Wabunge tuliochangia hapa tumewawakilisha wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa upande wa pili kwa Mawaziri, tunaenda kuwahamasisha wananchi wetu ili waweze kulipa kodi, boda boda wapunguze makosa na mambo mengine, lakini pale fedha zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo tuwaombe sasa na ninyi Mawaziri mchukue wajibu wenu kupeleka fedha hizi katika hii miradi kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ile miradi michango yetu na elimu yetu tunayoenda kuitoa kwa wananchi tutawaambia, gharama hizi za simu zinaenda kupelekea tupate fedha kwa ajili ya kukarabati barabara, kwa ajili ya kumalizia miradi mikubwa ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninyi mawaziri msipopeleka fedha katika hiyo miradi maana yake sasa pamoja na elimu tulioitoa kwa wananchi mnaenda kutupalia makaa kwa wananchi wale, kwa hiyo upande wa mawaziri kwa maana ya Serikali na ninyi tunawaomba mtimize wajibu wenu kuhakikisha miradi ile yote iliyotengewa fedha inaenda kutekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe ushauri mambo machache katika masuala mazima ya barabara hasa barabara zile zinazomilikiwa na *TARURA*. Huko nyuma halmashauri nyingi hasa zile za Dar es Salaam zilikua zinatenga fedha kwa ajili ya barabara zaidi ya bilioni 4 nakumbuka halmashauri ya jiji la Ilala na Temeke zilishawahi kutenga katika miaka mbalimbali. Hebu sasa tuangalie Serikali kama halmashauri hizi huko nyuma zilikuwa zinauweozo wa kutenga hizo fedha hebu angalieni Serikali namna ya kuzikopesha halmashauri hizi fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano; halmashauri ya Temeke Ilala na hizi nyinginezo zikakopeshwa labda bilioni 20 kila moja kwa ajili ya kwenda kukarabati barabara, halafu kila mwaka mkawahambia muwe mnalipa labda bilioni tatu tatu, naaminii baada ya miaka mitano barabara zitakuwa zimetengenezwa na fedha zitakuwa zimerudi katika mfuko mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ulizungumza katika hotuba yako kwamba majadiliano yanaendelea kuhusiana na mradi huu wa DNDP, kwa Dar es Salaam mradi wa *DMDP* ni muhimu kweli kweli. Tunaomba sana muharakishe mazungumzo katika mradi huo wa *DMDP*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho posho la wenyeviti wa Mitaa na madiwani, Mheshimiwa Waziri umezungumza halmashauri zile 16 zitaendelea kulipa kwa mapato yake ya ndani. Sisi tuwaombe sana Dar es Salaam tuna mizigo mikubwa sana na sisi Dar es Salaam mchukue gherama hizi Serikali Kuu muweze kulipa ili fedha hizi sasa ambazo wamekua wakilipwa sasa hivi madiwani ziende zikalipe wenyeviti wetu wa Serikali za Mitaa ambaa kiukweli wamekuwa na hali mbaya sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kumpongeza Waziri wetu wa TAMISEMI, dada yangu Mheshimiwa Ummu Mwalimu ameonyesha kwa kiasi kikubwa ushirikiano mkubwa na Waheshimiwa Wabunge. Kila Mbunge hapa ameandikiwa

barua na Mheshimiwa barua na Mheshimiwa Waziri aeleze vipaumbele vyake katika ujenzi wa shule za Sekondari, Wabunge wote tumeandika na zimemfikia waziri naamini ile migongano ya kugombania Sekondari ikajengwe wapi itakuwa imekwisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe na mawaziri mwingine wote tuunge sasa juhudhi alizozifanya Waziri wetu Mheshimiwa Ummy Mwalimu na sisi kwa kufanya hivyo naamini mambo mbalimbali yataenda kubadilika katika hal mashauri zetu, barabara zitajengwa, mashule yatajengwa, zahanati zitajengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, jiandae Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

MHE. KADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuamsha asubuhi ya leo tukawa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuipongeza hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hotuba ya bajeti ya Serikali na mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa mama Samia Suluhu Hassan, kwa juhudhi mbalimbali anazozifanya katika kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele kukuwa katika uchumi pamoja na kuinua maisha ya mwananchi mmoja mmoja katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Ally Mwinyi, kwa juhudhi zake mbalimbali anazofanya katika kuhakikisha Zanzibar inakwenda mbele na inasonga mbele kiuchumi na

kimaendeleo pamoja kunyanya hali za wananchi wa Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha Naibu wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya na mashirikiano ya pamoja hadi kufikia kutuletea bajeti nzuri ambayo inaenda kutatua changamoto za wananchi mbalimbali, changamoto za wakulima, wavuvi, wafanyabiashara na wananchi kwa jumla nawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wizara yake kwa kututambua sisi asasi zisizo za kiserikali - *NGOs* akatuweka katika bajeti yake kwamba na sisi tumechangia katika uchumi wa Taifa kwa kweli taasisi zisizo za kiserikali nazo zinafanya kazi kubwa katika kunyanya maisha ya mwananchi, kutatua changamoto za wananchi, kutatua changamoto za ajira, lakini kuinua uchumi wa nchi ni vyema sasa michango yetu nayo ikatambuliwa na dhamani gani tumewekeza katika mazingira yote, katika maeneo yote ya sekta zote za uchumi maendeleo ya jamii na kadhalika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza bajeti hii kwa kuondoa ushuru katika mazao ya Kilimo, Ufugaji, Viwanda na Biashara. pamoja na kuondoa ushuru huu wa forodha, tuisahau kuzingatia mazingira katika bajeti zetu zote tuhakikishe kwamba pamoja na mambo yote tunayoyafanya kuilinda nchi yetu na mazingira na mabadiliko ya tabia nchi, na katika bajeti imo, Mheshimiwa umetenga fedha kwa ajili ya mazingira, ni vizuri sana tukawa na fedha zetu za ndani za kuwekeza katika kuhifadhi mazingira yetu ya nchi na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili napenda kuchangia kwamba pamoja na mambo yote tunayoyafanya ya kuwekeza lakini tutenge ardhi katika maeneo muhimu ikiwemo uhifadhi wa misitu, uhifadhi wa uoto wa asili, uhifadhi

maeneo tengefu kwa ajili ya kulinda mazingira ya nchi na kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili napongeza Serikali kwa kuondosha ushuru katika uwekezaji wa mbolea na viwanda vya mbolea ni kweli itasaidia kutatua changamoto za mbolea katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nashauri katika uwekezaji huo huo wa mbolea tuisahau mbolea zetu za asili kwa maana ya kuhifadhi ardhi yetu iendelee kudumu na kutumika milele na vizazi vijavyo. Naamasisha pia katika mipango inayokuja tuwekeze pia katika kilimo hifadhi na kilimo hai, kilimo hifadhi na Kilimo hai kitakwenda kulinda afya ya mimea yetu na mazao tunayozalisha hayatakuwa hayana *chemical*, lakini pia tutahifadhi ardhi na udogo wa nchi yetu kwamba usiendelee kuharibiwa na *chemical* za viwandani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea katika hicho hicho kilimo, kuna kilimo cha mazao ya bustani na mboga mboga, kilimo hiki kimetokea kuwa na soko kubwa duniani na tunaingiza fedha nyngi za kigeni kupitia kilimo hiki cha bustani na mboga mboga.

Narudia kusitiza kwamba Kilimo hiki kuna baadhi ya maeneo wanakata miti mikubwa wanaondosha uoto wa asili badala yake tunakwenda kupanda bustani na mazao ya mboga mboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tulitizame kwa upana wake pia na ndiyo nikasisitiza kwamba tuweke na maeneo ya kuhifadhi uoto wa asili na misitu kwa maana kila bidhaa zikiwa nyngi huko duniani na sisi kilimo tutaongeza kupanua maeneo, tukipanua maeneo tunakata miti ya asili, tunakata na misitu, lakini tunapanda mboga mboga, naomba hili tuliweke angalizo katika mipango yetu ya maendeleo kwa kila mwaka, na hii nakuja pale kusitiza kwamba kupima maeneo yapi ya Kilimo, yapi ya ufugaji, yapi ya viwanda, na yapi ya uhifadhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea naipongeza Serikali kwa kuondoa ushuru wa ongezeko la thamani katika taa za *solar*, pamoja na vifaa vya kutengenezea *solar*, lakini katika hapa nilikuwa nauliza Serikali injibju kwamba katika kusamehe hizi tozo na kodi inaunganisha na ile mitambo ya kusukuma maji katika visima vyetu kama hicho hakipo nashauri Serikali mitambo ya kusukuma maji katika visima vyetu viondolewe kodi. kwa sababu uwekezaji wa visima vya maji kwa kutumia *diesel/na petro/tumegundua* kwamba ni gharama kubwa ya uendeshaji na hivyo mzigo unamwelemea mwananchi anayetumia maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali yetu, ni ya Rais wetu ni kuhakikisha mwanamama anamtua ndoo kichwani lakini wananchi kwa ujumla wanapata maji safi na salama. Kwa hivyo tukipunguza kodi kwenye vifaa vya kusukumia maji katika visima vya maji itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa visima vya maji na maji yatapatikana kwa bei nafuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kwenye Sekta ya uvuvi naipongeza Serikali sana, sasa tumejipanga katika uvuvi, uvuvi wa bahari kuu na Serikali ina mpango wa kununua meli za uvuvi. Ushauri wangu pamoja na kujilingiza kwenye uvuvi huo mkubwa kwa kununua meli uvuvi wa Bahari Kuu, uvuvi wa Kisasa tuisahau wavuvi wetu wadogo wadogo, wavuvi wetu wadogo wadogo na wao waende sambamba na ukuaiji huo wa uchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu bado zana zao ni duni, zana zao hafifu mvivu anapokwenda baharini anajua kwenda lakini uhakika wa kurudi hana kwa sababu atakachokutana nacho baharini hajui kama ni mawimbi makali au ni dhuruba, au atapata samaki au hapati, kwa hivyo uchumi huu mkubwa tuwachukue wavuvi wetu wadogo wadogo ambao wametusaidia mpaka kufika hapa kwamba uvuvi bado Tanzania upo tuwawezeshe kwa zana za kisasa ili na wao tuwainue kiuchumi lakini pia waongeze mapato ya Taifa na waweze kujilajiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia nasema hivi naipongeza sana Serikali tumuunge mkono Rais wetu atuletee maendeleo nampongeza Makamu wa Rais, nampongeza Waziri Mkuu, nampongeza Rais wa Zanzibar kwa juhudhi kubwa anazofanya katika kuwaletea wananchi maendeleo na sisi wananchi tuko bega kwa bega kuhakikisha maendeleo haya tunayapata yanawafikia wananchi wetu, yanatufikia na sisi wenyewe na vizazi vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ahsante sana, nakushukuru naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Olelekaita Mbunge wa Kiteto anapenda kuwatangazia wageni wake ambao wameingia Bungeni sasa hivi mnakaribishwa Bungeni karibuni, karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Asha Abdullah, ajiandae Mheshimiwa Tunza.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii kwa siku hii ya leo. Awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa nguvu kuweza kusimama hapa kwa heshima ya kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani na pongezi zangu za dhati kwa Rais wetu, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kazi endelee Jemedari mkuu Mheshimiwa Mama Samia kwa jinsi anavyosimamia kuendesha Serikali yetu hii na leo hii bajeti yake katika Awamu hii ya Sita. Bajeti ambayo imegusa wananchi wote na bajeti ambayo imeakisi na kulenga mambo muhimu yote ya maendeleo ya kila mtu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubali kwamba lazima tuwe na mbinu yoyote ya kupata kodi ili kuendesha Serikali na kuendesha nchi. Kwa hivyo kuna sehemu itaumauma lakini hakuna nchi inayoendeshwa bila kukusanya kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu leo nataka niunganishe pale Mheshimiwa Rais Jemedari Mkuu Mama Samia alipokwenda kufungua tawi la Benki kuu Tanzania na kuonyesha jinsi nchi yetu inavyotarajiwa kufanya kwa kutumia sekta hii ya kifedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo ambalo limekua likisemwa humu bungeni kwa muda mrefu nalo ni la benki ya *Federal Bank of Middle East*. Tokea tarehe 8 Mei, 2017, *FBME* benki ili wekwa chini ya ufilisi kwa *DLB deposit insurance board* na Benki Kuu ya Tanzania. Leo ni miaka minne na mwezi moja hakuna majibu ya utatuzi kwa suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wateja wa benki hii hawajapata amana zao Zaidi ya kulipwa shilingi milioni moja na laki tano licha ya ramana yao kuwa kubwa. Uwe na milioni mia mbili, uwe na milioni mia tatu kwa mujibu *regulation* uwe unalipwa 1500, wafanyakazi licha ya kuwachishwa kazi hawajapata stahiki zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki wenye amana mauti imewakuta bila kupata haki zao na familia zao zinaendelea kuteseka. Kwa ruhusa yako naomba niwataje baadhi ya hao waathirika ili Serikali na watu wengine wote wapate kuona jambo na uzito wake; mfano Marehemu Ally Juma Shamuhuna, aliyekuwa Waziri na Naibu waziri kiongozi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme hili jambo nina *interest* nalo mimi nausika nalo sana pia. Marehemu Dkt. Maliki Abdallah Juma, alikuwa mkurugenzi mkuu wa wizara ya afya, marehemu Mohamed Toll Suleiman, Marehemu Shaibu na wengine kadhaa na baadhi wengine walio hai sasa hivi wameshafika kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako niwataje; Mzee Buruani Sadati ambaye alikuwa Waziri na mshauri katika Ofisi ya Rais ya Dkt. Shein, Dkt. Mohamed Sale Jidawi, Dkt Nafisa Dkt. Mwatima na wengine kadhaa ambao

hao wa sasa na wenzao wengi wamestaafu wanategemea amana yao hiyo waliyoweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wa Bunge liliopita 2018 walisemea jambo hili mara kadhaa halikupata majibu, Mawaziri, Naibu Mawaziri mpaka Mwanasheria Mkuu lakini bado jambo hili limekwama. Ushauri wangu kwa vile Benki Kuu ndiyo *custodian* na ndiyo *guarantor* basi waone namna ya kulimaliza jambo hili. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Mwanasheria wakutane na makundi ya wadau husika bila kubagua na mbili kutafuta njia bora kuhakiki haki za wadau hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu chini ya jemedari wetu Samia Suluhu Hassan iweje kulitatua jambo hili, hichi ni kilio akisikie Mheshimiwa Rais kuitia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu lingine ninalotaka kulizungumzia hapa ni hili la suala ya VATkwenye bidhaa, natoa shukrani sana kwa Serikali kulifanya kazi jambo hili, kuamua mfumo wa marejesho kama ilivyokuwa zamani. Ombi marejesho yafanywe moja kwa moja baina ya TRA na ZRB kwa sababu wanayo mifumo ya risiti kila mmoja anamuona mwezake, zoezi likifanywa na Hazina patakuwa na urasimu na Hazina zetu Hazina mifumo wanayoonana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nimelifurahia na kweli limetia moyo vijana wetu ni hili la biashara za bodaboda. Ni ukweli usiopingika biashara hii inafanywa na vijana wetu wengi na inawasaidia sana lakini wamekuwa wakipata mkwamo mkubwa katika kufuatia tozo za faini kubwa ya elfu 30, lakini Serikali yetu sikivu imeona na imeweka kiwango kizuri cha Shilingi elfu kumi huu ni uamuzi wa kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu lingine ninataka kulisema hapa ni mkopo nafuu kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, Bunge la Kumi na Moja lilitunga sheria kuzitaka Halmashauri zote nchini kutenga

asilimia 10 ya mapato kwa ajili ya mikopo nafuu kwa vijana wanawake na watu wenyewe ulemavu. Ni ukweli usiopingika utaratibu umepunguza kwa kiasi kikubwa changamoto za ukosefu wa ajira hivyo kuyawezesha makundi haya kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Halmashauri zote ziongeze usimamizi na udhibiti wa makusanyo na migawanyo yake ili kuhakikisha fedha za mikopo zinawafikia makundi stahiki na mikopo itolewe bila upendeleo. Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI wakae pamoja kuona namna bora ya uratibu wa mikopo hiyo ya makundi maalum lengo la kuhakikisha makundi yanajiendeza kiuchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu lingine ni nafasi ya taasisi ya *OSHA* kuchochea uchumi wa viwanda nchini. Kupitia Kamati yetu ya Katiba na Sheria nimeona usimamizi wa afya mahali pa kazi (*OSHA*) chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu na chini ya jemedari anayeendalea kusogea mbele Mheshimiwa Jenista anapambana kweli kweli kazi hapa inafanyika vizuri, mazingira yamekuwa mazuri sana kutokana na ufanisi wa shughuli zao kusimamia mazingira rafiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na michango mizuri ya taasisi ya *OSHA* bado narudia hoja yangu kwamba kumekuwepo na tatizo la kuwakaimisha watumishi kwa muda mrefu, kwa hivyo niombe ofisi hii ilifanyie kazi watu wasikaimu kwa muda mrefu ili wapate kufanya motisha na ninaamini kwa uhodari wako Mheshimiwa Jenista jambo hilo kwako siyo tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi wa mfuko wa fidia kwa wafanyakazi *WCF* mfuko huu uliopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kipindi cha miaka mitano tangu ulipoanzishwa 2015 umekuwa mfuko wenyewe tija kubwa kiuchumi na ustawi wa waajirriwa katika sekta binafsi na sekta ya umma. Mfuko umeonyesha uwezo wa kuijendesha kwa kuendelea kukua kiuchumi kimfumo mwaka hadi mwaka kiasi

kwamba mfuko umeipatia Serikali kodi ya Shilingi bilioni 10 kwa mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya kazi ushauri wa muda mrefu wa Kamati na Wabunge kuhusu michango, mwaka wa fedha inakwenda kupungua endapo waajiri wataanza kuchangia

MWENYEKITI: Ahsante

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, waajiri wataanza kuchangia 0.6 kwa msingi huo naomba kuunga mkono hoja, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na wote waliochangia katika hotuba hii. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mbunge wa Jimbo la Lupa Masache Kasaka anapenda kuwatangazia wageni wake Mchungaji Jackson Mkakami Ndugu Mashaka Sompö, Ndugu Joshua Mlambabala, Ndugu Laurent Nzingirwa karibuni sana. Mheshimiwa Tunza, jiandae Mheshimiwa Eng. Ezro John

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya siku ya leo, nianze mchango wangu kwa kutoa shukrani za dhati kabisa kutokana na ile kauli ya Waziri Mkuu aliyosema msimu huu wa korosho korosho zote zitasafiri kupitia bandari ya Mtwara. Watu wa Mtwara, watu wa Kusini tunajua na tunathamini mchango huo kwa sababu tunatambua ni nini kinakwenda kutokea, hicho kilikuwa ni kilio chetu cha siku nydingi ndani miaka mitano korosho zilikuwa zinasafirishwa nje ya bandari ya Mtwara hivyo kusababisha mambo mengi ya kiuchumi kusimama Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kama korosho zitasafiri kupitia bandari ya Mtwara tunategemea watu wenye maghala watakodisha pale, tunategemea

wafanyabiashara wadogo wadogo, mama lishe, wanawake wenzangu mimi Tunza, watafanya biashara pale na mambo mengine yatakwenda kuwa sawasawa. Nishauri bandari ile isiishie kutumika kwenye zao la korosho tu itumike pia kwenye mazao mengine na kwenye shughuli nyingine, kwa sababu Serikali imewekeza pesa nyingi pale ambazo ni kodi za Watanzania hivyo ikiendelea kutumika tunasema ile *value for money* itaonekana pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukrani za dhati kwa hilo na naiomba Serikali iondowe zile changamoto za makontena za tozo kubwa kubwa ili kusudi ivutie wafanyabiashara waje kuitumia bandari ya Mtwara nasi watu wa Kusini Watanzania halisi tupate kunufaika na hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwenye zao la korosho naiomba Serikali iangalie kwa undani suala la pembejeo kumekuwa na malalamiko mengi kama tunaenda kutumia bandari basi pembejeo nazo zipelekwe kwa wakati na kwa ubora na kwa uwungi unaotakiwa ili kusudi watu walime wapate korosho nyingi ili ile bandari inayokwenda kutumika sasa ipate manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungumzie kidogo *TRA*, unapotaka kupata pesa ni lazima uwekeze, usitegemee kupata pesa bila kuwekeza. Naishauri Serikali kama kuna mtu anakwenda *TRA* ukabahatika kufika na ukahudumiwa na mfumo bila kuambiwa mfumo, sijui mtandao uko chini, mtandao unasumbua, mtandao unafanya nini, ni bahati sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha hili ufanya maendeleo ni lazima upate pesa. Waliopewa dhamana kukusanya pesa ni *TRA* sasa tunaomba mboreshe mfumo wa *TRA* ili kusudi mtu ukitoka nyumbani siku hiyo, maana yake nisiwaambie kulipa kodi nako ni moyo, mtu ametoka nyumbani amebebeba pesa yake anatamani aende *TRA* akalipe kodi anafika pale anaambiwa mfumo haufanya kazi, akirudi nayo ile pesa nyumbani hatuna uhakika kama kesho atarudi tena kwenda kuufuata mfumo unafanya kazi ama haufanyi kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naiomba Serikali kwa moyo wa dhati kabisa wekezeni kwenye mifumo hii inayotumika kukusanya mapato ili kusudi mtu anapoamua kwenda kulipa akifika pale aliye aondoke. Uwe ndiyo mfanyakishara hawezi kutamani kufika *TRA* akae masaa matatu, manne matano mwisho wa siku unamwambia mfumo haufanyi kazi akirudi nyumbani ile pesa anaingiza kwenye mzunguzuko wewe Serikali unakuwa hujapata chochote. Mkaimarishe kwenye vitengo vyote hata kule *LATRA* nako pia kuna usumbufu wa mtandao ukienda inawezekana usipate huduma, mitandao yetu haijaka sawa sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wananchi watalipa kodi kwa hiyari wakiona maendeleo. Mfano watu wa Mtwara tumekuwa tukilia kila siku kuhusu ile barabara ya kutoka Mtwara Mjini inayopita Nanyamba, Tandahimba, Newala, inakwenda Masasi, kilometra 210 tu zimezungumzwa na Wabunge waliopita sisi wengine tumeingia hiki ni kipindi cha pili tunazungumza mpaka leo mmejenga kilometra hamsini, hivi kilometra 210 kwenye eneo ambalo zinatoka korosho! Korosho hizo zinazochangia Pato la Taifa la nchi hii kwa kiasi kikubwa kilometra 210 *just* kilometra 210 zinawashinda kitu gani, twendeni mkatutengenezee hizi hili na sisi tutakapokuwa tunalipa kodi tulipe kodi kwa kujivuna kabisa kwamba tunalipa kodi na maendeleo tunayaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukienda kule Mtwara katika Mikoa inayoongoza ukosefu wa maji ni pamoja na Mtwara, mkatutekelezee mradi wa maji ya kutoka Mto Ruvuma ili tunapolipa kodi tujue kodi zetu zinatumika kutuletea maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika hii miradi ya *REA* kama kuna mkoa umefanya vibaya kwenye miradi ya *REA* ni Mkoa wa Mtwara, kuna vijiji vingi havina umeme tunashukuru Mheshimiwa Waziri wa Nishati alituita sisi Wabunge wa Mtwara kutuhakikisha kwamba Wakandarasi ambao wamekwenda safari hii watakwenda kufanya vizuri. Tunaomba msituache nyuma kila kitu, ukienda maji tatizo

Mtwara, umeme Mtwara, barabara Mtwara tunaomba muende mkatutekelezee na hospitali ya Kanda ya Kusini tunaomba iende ikafunguliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani tupate huduma tukiwa kwenye Kanda zetu wala siyo lazima tufike Muhimbili, kule kukiwa kuko poa tutaishia huko huko ingawa huku kwngine tutakuja kufanya mambo mengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nishauri kwenye *issue* za fursa za mapato, mimi nimekuwa kwenye Kamati mbalimbali, Wakurugenzi wanapokuja kwenye Kamati tunawashauri mkatafute vyanzo vipyta ya mapato, mimi naishauri Serikali kuwe na kitengo maalum chenye wataalam wa kuweza kufanya utafiti, *analysis* ya kutosha kujua kwa mfano ukienda Mkoa wa Mtwara Halmashauri fulani inaweza ikawa na fursa ya mapato moja, mbili, tatu, wawashauri wale halafu yale malengo yanayowekwa yale, wale Maafisa Mipango wetu yule mtu atakayefanya vizuri basi aonekane amefanya vizuri amefikia malengo na yule ambaye ajafanya vizuri aambiwe ajafanya vizuri na pia kuwe na *training*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua mimi tatizo lingine ninaloliona sijui kwa sababu ni mwalimu huwa naona kama wafanyakazi wengi wa Serikali wakishaajiriwa hakuna mafunzo kazini, wakati mambo yanabadilika, mambo hayako vilevile watu wanatakiwa wapewe mafunzo waambibiwe sasa hivi kama nchi tunaelekea huku tunaomba mfuatilie moja mbili tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi Tunza ukiniuliza fursa ambazo zinaweza zikapatikana Mkoa wa Mtwara naweza nikakuambia tuna fursa ya gesi ule mradi wetu wa *LNG* ufanyiwe kazi, tuna fursa ya korosho lakini kwa masikitiko makubwa nakuambia hakuna kiwanda chochote cha maana kinachofanya kazi ya ubanguaji. Hizo ndiyo fursa tuna bahari hatuna bandari ya uvuvi, hatuna meli, hatuna viwanda vya samaki pesa tunazitoa wapi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliambiwa kiwanda cha mbolea mpaka leo hatukioni hizi ndio fursa za mapato ambazo mimi ukiniuliza *layman* tu ambaye sijui uchumi naweza nikakuambia, Wachumi wetu watushauri vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie jambo moja hili ni ombi kwa Serikali, katika Manispaa ya Mtwara Mikindani kuna mgogoro unaendelea kati ya wafanyabishara wadogowadogo ambao walikuwa wanafanya biashara soko la sabasaba Serikali imejenga soko zuri na soko la kisasa, wafanyabiashara walizoea kufanya biashara kwenye hilo soko la sabasaba sasa hapa pana mgogoro, wale wafanya biashara ni wafanyabiashara wadogowadogo, wengine ni wanawake wana mitaji midogo naomba Serikali iangalie suala hili kwa busara zaidi kuliko kutumia nguvu. Waone ni namna gani ya kukaa na hawa wafanyabiashara ili kusudi wafanye biashara zao kwa amani watumile lile soko letu la kisasa ambalo limejengwa lakini waangalie na huku wanawaachaachaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha nakuuliza swalilangu la mwisho ile *issue yetu ya export levy* kutoka kwenye zao la korosho unatuachaachaje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Injinia Ezra John Chiwelesa jiandae Mheshimiwa Bakari Ahmad Bakari.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi pia na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango, hasa kwenye bajeti hii kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Waziri na timu yake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya, aliongea Mheshimiwa Jerry hapa juzi kwamba umeupiga mwingu sana kama wa Morrison, nadhani na staili ya kuupiga ndiyo staili vijana wanaitumia zaidi, hata

jana Mama aliyoafanya Mwanza kule vijana wanapo-
comment wanasema Mama anaupiga mwingi sana.
(*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuseme kwa kweli kutoka ndani ya kilindi cha moyo wangu nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wako kazi mliyoifanya ni kubwa, bahati mbaya siku inasomwa bajeti sikuwepo nilikuwa na msiba kwa hiyo nikawa niko kwenye mazishi ya Babu yangu Biharamulo lakini nilipokuwa njiani narudi nikawa napitia *comments* nyingi sana kuna watu walitisha *press conference*. Ukiona mtu anaitisha *press conference* anakosa kitu cha kukosoa humu kwenye bajeti anaishia kusema bajeti hajaongelea Katiba Mpya na Tume Huru ya Uchuguzi uelewe kwamba umemaliza kila kitu. (*Makof*)

Kwa hiyo niwapongeze juu ya hilo kazi illyofanyika ni kubwa sana, pia nimpongeze Mama kwa kazi kubwa ambayo ameifanya tangu ameingiea madarakani ni muda mfupi lakini watu tunaona matokeo chanya kabisa kabisa hasa kwa niaba ya wananchi wa Biharamulo nishukuru kwa milioni 500 za ujenzi wa barabara ambazo zinaingia kuitia *TARURA* na tayari tumeshakubaliana tuongeze kilometra moja ya lami pale hili tuweze kuchochea maendeleo haraka zaidi. Hali kadhalika na suala la shule ya sekondari, kuna shule sasa tumekubaliana inaenda kujengwa pale Nyakaula pale ni eneo ambalo lilikuwa na wanafunzi wengi zaidi kwa hivyo tutaongeza shule ya pili ili maendeleo haya ambayo Mama anayasema kwa vitendo na wao wayapokee haraka zaidi ili wawewe kuunga mkono juhudii kubwa ambazo zinafanywa na Serikali ya Awamu ya Sita. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya labda lipo jambo moja ambalo mimi ningependa nijikite nalo, mimi ni mdau wa viwanda kwa hiyo nadhani mchango wangu kwa sehemu kubwa una- *base* zaidi katika masuala ya viwanda, mpango wetu wa maendeleo wa miaka mitano ijayo 2021/2022 - 2025/2026 dhima yake kubwa inasema ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi tangu nimeanza kuchangia mara nyingi sana nimekuwa ninagusa masuala ya viwanda kwa sababu ni *area* yangu ambayo nimekuwa nikitumika kwa muda mrefu kwa hiyo napenda nichangie kitu ambacho nina *experience*. Kwanza ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kwa hiyo nichukuwe pia nafasi hii sana kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo ambayo aliyatoa juzi hasa suala la Liganga na Mchuchuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye Kamati na bahati nzuri tumefanikiwa kufika *site* pale kwenye ziara ya Kamati, mradi huu ni mradi ambao unaenda kuliinua Taifa hili na kutupeleka mbele zaidi. Ukipitia ripoti zote ripoti ya *NDC* inasema, lakini pia jambo moja ambalo nimekuwa nikiliona kwa upande wangu na upande *profession* yangu tunachokikosa hapa mpaka mradi huu unachelewa ni *technologytu!* *Technology* ndiyo inayotutesa leo tungelikuwa na uwezo tuna wataalam wa Kitanzania pale tungeshatia timu na hii kazi ingekuwa inafanyika leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukiangalia ripoti *NDC*, *total investment cost* ambayo huyu Mchina anakuja kuweka pale ni *three billion US Dollars*. Sasa ukiangalia *three billion US Dollars*, tunajenga reli leo inatumia thamani kiasi gani? Wakati ule ni mradi wa kibiashara kwa sababu anaweka *three billion USD*, na *income per year* – hii ni ripoti ya *NDC* – *income per year* itakuwa ni *1.736 billion USD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani anaweka billioni tatu mtaji, baada ya mwaka mapato ni *1.736 billion USD*. Kwa hiyo baada ya miaka miwili tu alichokiwekeza pale kashakipata na kila kitu kinakwenda sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo unaweza kuona kwamba kinachotutesa pale mpaka leo ni *transfer of technology*. Ndiyo maana mimi kwenye michango yangu mingi sana nimekuwa naomba, tujaribu kusikiliza jinsi ya kulinda viwanda vyaa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojaribu kulinda viwanda nya ndani hatulindi tu kwa sababu tunazuia wale watu wasilet au wasifanye nini, tunawawezesha vijana wetu wa Kitanzania kupata *knowledge ya how they can work on these industries* ili waweze wao wenyewe kesho na kesho kutwa kutumia *experience waliyoipata kwenye viwanda watusaidie kujenga viwanda vingine hapa.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, sasa niombe, na nadhani hapa tuko sawa, kwamba kuna watu wameweza kuelezea sana suala la *importation*. Nilichangia juzi nikielezea suala la *importation of traders*, sitaki sana kurudia kule, lakini tumeona kwamba viwanda vilivyokuwepo hapa vingi vilikufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tutakapokwenda kuvinyanya viwanda hivi maana yake tuna-*transfer technology* hata kwa vijana wetu wanaosomea *mechanical engineering* katika vyuo vyetu, vijana ambao wanasona VETA, maana tunafungua vyuo nya VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unafungua vyuo nya VETA tuna-*invest billions and billions* kwenye VETA halafu hatuna viwanda, hawa watoto tunawapeleka wapi baada ya hapa? *Investment* tulioifanya kwenye vyuo nya VETA tunaipeleka wapi baada ya hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunachoomba ni kwamba tujikite zaidi kwenye kuwezesha viwanda nya ndani. Kwanza niwashukuru na kuwapongeza, kwa mfano ishu ya *tiles* tunajua wengi sana wakienda madukani wanataka *Spanish tiles*. Sasa ili kulinda viwanda hivi ambavyo vimejengwa kwenye Mkoa wa Pwani, mmeona, mmeongeza asilimia 35, kwamba sasa *import duty* iwe 35%; unampa mtu *chance* ya kuchagua *premium*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tajiri anayesema anataka akajenge kwa *Spanish tiles* maana yake anatuongezea asilimia kwenye *import duty*. Anavyoleta hapa zile *tiles* ili waweze kuzinunua hapa Serikali inapata kodi ya kufanya vitu

vingine, lakini huku tukiendelea kuvilinda viwanda hivyo ambavyo vimejengwa hapa kwa ajili ya kuwaajiri Watanzania na kutumia malighafi za Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe sambamba na hilo, ninakumbuka hata ishu ya *REA*. Nilikuwa napitia ripoti ya *REA* hapa, wakati mnaanza miaka mitano iliyopita, wakati tunaanza kufanya miradi hii ya umeme nakumbuka walio wengi walikuwa na wasiwasi kwamba je, tutapata *capacity?* Tutakuwa na uwezo wa kuzalisha hivi vitu hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unapoweka sera nzuri kinachotokea ni nini? Hili likishakuwa soko la tajiri fulani ambaye ana viwanda kule nje, anapoona soko lake halifanyi kazi, anachojaribu kukifanya lazima alifuate soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ambaye amesha-*invest* na anajua soko lake ni Tanzania, amekuwa anapata bilioni 50 au 30 kutoka Tanzania anapofanya biashara, yule mtu ukimwambia tumezia *importation* au *importation* anaona inakuwa kubwa anashindwa *ku-compete*, anachokifanya anatoka kwenye nchi yake anakuja kuwekeza hapa. Akishawekeza hapa tayari anatutengenezea biashara kwa sababu anataka alinde soko lake ambalo amelipata Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunachoomba, lazima tujaribu kuangalia, mtusaidie kwenye hili. Lakini kipindi mnatusaidia kwenye hili, kwamba sasa tujaribu kuvutia wawekezaji na kuweka *conditions* ambazo zitalinda viwanda vyा ndani, lakini vilevile twende *step* moja mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijaribu kuchangia hapa *last time* nikasema hatuwezi kujenga viwanda vyote Mkao wa Pwani. Pwani haitaenea. Maana bada ya hapa na sisi vilevile huko mikoa tunahitaji viwanda viwepo. Tunapotamka viwanda hatutatakuja kila siku tunalia viwanda vijengwe Chalinze au Dar es Salaam wakati hata mimi huko Biharamulo, Kigoma na wapi, na sisi tunataka viwanda hivi. Ili sasa mwekezaji atoke aje kuwekeza Kigoma, Biharamulo,

Arusha, Mtwara au Mbeya lazima tuoneshe kwamba kuna *incentive* fulani tunampa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, jana Mheshimiwa Mavunde kaongelea hapa suala la *income tax*. Tujaribu kuona, huyu mtu anapata *advantage* gani akija Kigoma? Maana atoe kontena Dar es Salaam, alipeleke Kigoma halafu amalize arudishe tena kuuza Dar es Salaam. Anafanya *double kwenye transportation*, hataweza kushindana na mtu aliyeleo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tujaribu kuona jinsi ya kuweza kuwasaidia. Hata kama ni *income tax*, mpe *grace period*. Mwambie labda akiwekeza Bukoba au Buharamulo mnampa *chance* ya kutokulipa *income tax* kwa miaka mitano au mingapi, au vinginevyo mpunguzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule mtu ataangalia, atapiga hesabu na benki yake *then* atajua aende akawekeze wapi. Hapo tutakuwa tunatanua uchumi na kusambaza viwanda kwa ajili ya watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa najaribu kulipitia hapa ni mazingira mazuri ya uwekezaji ili watu waweze kuwekeza. Hilo jambo mmeliahidhi, Mheshimiwa Waziri ninaomba mkalismamie maana kipindi cha nyuma killio kilikuwa kikubwa. Lakini kwa sababu bajeti yako imesema na bajeti imesema mawazo ya Wabunge kwa kweli mimi sina budi kushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hata Wabunge tunaondoka hapa kifua mbele kwa sababu miezi mitatu tuliyokaa Dodoma tunaishauri Serikali, kwa sehemu kubwa mambo mengi yametekelizwa na mambo mengi yamekuwa *incorporated* hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hata sisi tunaporudi huko nyuma, kesho na keshokutwa hata tunaporudi kwenye Bunge lingine tuna uhakika kwamba tunachokishauri hapa Serikali inasikia. Na hii ndiyo kazi yetu sisi, kuwashauri ninyi, ili

ninyi msikie wananchi waliyotutuma muende mkayafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kwa kumalizia, niliongelea suala la *trailers*, naomba hili jambo ulichukulie *serious* kwa sababu nina *experience* nalo. Tumeongea, si mimi tu, naona watu wengi, nililianzisha lakini watu wengi sana wameweza kuliongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *import duty*, unajaribu kuangalia magari yanazalishwa hapa, *trailers* hizi. Tunachojaribu kuangalia, tuvute wawekezaji waje, hata *HOWO trucks*. Tumeona *HOWO* ziko nyingi sana hapa. Ongeeni na yule mtu mwenye *HOWO* kule. Kwa sababu hii ni bandari ambayo ina-serve nchi zaidi ya tisa, tukimwambia aje awekeze hapa akaja na spea, akajenga kiwanda hapa cha kufanya *assembling*, kama leo wanavyo-*assemble* magari pale Kibaha, wana-*assemble* mabasi yameanza kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ataajiri Watanzania. Tunahitaji ajira kwa ajili ya Watanzania maana wanalipa *SDL*, wanalipa *PAYE*, wanalipa vitu vingi zaidi. Lakini chanzo kikubwa cha kutengeneza ajira milioni nane, tutazipata tutakapovutia wawekezaji wakaja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe hilo jambo uliangalia, suala la *duty* kwa ajili ya *trucks*, hizi *trailers*, tuone jinsi tunavyoweza kuzipandisha nazo ili wawe *competitive* na waweze kushindana na watu wengine hapa. Maana huna haja ya kuchajji *ISI* asilimia 25 halafu mtu anayeleta gari kubwa lenye thamani kubwa ya kutupa kodi kubwa bado anachajiwa asilimia kumi. Hili jambo naomba milaingalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze. Mimi sina jambo la kuongezea zaidi ya kushukuru kwa hotuba nzuri na yote ambayo mmeyaweka ambayo tumeyachangia hapa. Mungu awabariki sasa tunapokwenda kuyatekeleza ili sasa kwa sababu ninyi ndio wenyе pesa, kuna mambo mengine

ambayo tumeyasema hapa yanahitaji pesa, mkaweza kuzitoa hizi pesa kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kwa kumalizia; *TBS* tumewapa kazi nyngi sana. *TBS* leo ndio anayekagua magari, kazi iliyo kuwa inafanyika Japan; *TBS* leo ameacha mkataba na *SGR* ndiye anayekagua *pre-export verification* anafanya ye ye; *TBS* tumempa vinasaba ndiye anaanza kuweka vinasaba kwenye mafuta ya petroli. Kwa hiyo kwenye Bunge hili tumempa kazi nyngi sana *TBS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachoomba, ili *TBS* asituangushe kwa sababu hizi kazi ni *continuous*, atahitaji bajeti ya *manpower*, atahitaji bajeti ya kununua vifaa. Ninaomba mtenge pesa na *TBS* apatiwe hizi pesa haraka ili isije ikawepo sababu sasa kwamba *TBS* tulimpa kazi na ameshindwa kufanya kazi huku akiwa anakwamishwa na ninyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bakari Ahmad Bakari, wajiandae Mheshimiwa Aloyce Kamamba, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani na Mheshimiwa Vita Kawawa.

MHE. BAKAR HAMAD BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba hii ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingu wa rehema, aliyenipa uhai na uzima leo hii kuweza kusimama ndani ya Bunge hili la kuweza kuchangia hotuba hii nzuri ambayo ni *very participative* ambayo imeshirikisha mawazo ya Wabunge wote katika Bunge hili, wale ambao walichangia kwenye hotuba mbalimbali za kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mwananchi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba hii. Lakini pia nimpongeze Naibu Waziri wake kwa msaada mkubwa sana kwenye uwasilishaji wa hotuba hii. Sambamba na hilo niwapongeze timu yao yote; Makatibu Wakuu na Manaibu wao, kuweza kusaidiana kuweza kuiandaa na kuiwasilisha hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ni hotuba ya kwanza kwa Serikali hii ya Awamu ya Sita. Nimpongeze mama yetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama Samia Suluhu Hassan, kwa majibu mengi sana ya Watanzania, hususan wanyonge kupidia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii imejibu majibu mengi sana, changamoto nydingi sana za wananchi kwenye majimbo yetu kupidia Wabunge wengi ambao walichangia, nikiwemo mimi mwenyewe. Niliweza kuchangia suala la gharama za mizigo inayotoka Zanzibar kuja Bandari ya Dar es Salaam wakati nachangia hotuba ile ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limepatiwa ufumbuzi, na nimpongeze sana mama yetu, Samia Suluhu Hassan, tuko pamoja. Nawaomba sana wenzangu, Wabunge na wananchi tuendelee kumtakia dua, Mungu amlinde, ampe afya njema ili aendeleee kutujengea nchi yetu hii kwa uchumi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii imebeba dhima kubwa ya uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Hatuwezi kujenga uchumi shindani ambao utakuwa na viwanda na kwa faida ya maendeleo ya watu kama hatujajenga mazingira rafiki kwa wawekezaji wa ndani na wa nje kuja kuwekeza ndani ya nchi yetu. Ukiangalia sasa hivi mazingira yaliyopo hatuwezi kusema kwamba ni mazingira rafiki kwa wawekezaji kuja kuwekeza ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kuwekeza katika uchumi wa viwanda na uchumi shindani, ni lazima tupunguze suala la riba. Riba kwenye benki zetu ni kubwa, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tunampongeza na kumshukuru mama yetu Samia, juzi naye pia amelizungumza jambo hili. Lakini pia Naibu Waziri wakati una-*wind up* ile hotuba yako ya Wizara ya Fedha ulilizungumza jambo hili na ukasema kwamba mna nia ya kukutana na Benki Kuu pamoja na wadau wote wa benki kuweza kuangalia namna ya kupunguza riba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu ambao tunashindana nao wkenye viwanda riba zao ziko chini. Sisi bado riba yetu iko juu sana. Hatuwezi kwenda kushindana nao kama hatujaweza kuondoa jambo hili, kama hatujaweza kupunguza riba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la urasimu; wanapokuja *investorswaliomo* ndani au walioko nje wanaokuja hapa, bado kuna suala la urasimu, mara pale mara hapa mara huku, anapoona hivyo *investoranaondoka* na fedha zake anakwenda kuwekeza maeneo mengine, nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba sana, tunaiomba sana Serikali, tunaiomba sana Wizara iondoe suala hili. Ikiwezekana basi iweke *one stop center* ili anapokuja *investor* basi iwe ni rahisi kwake kufuata zile *procedures* za kinchi na kuweza kuwekeza. Wanapowekeza hawa wanatuletea faida nyingi sana kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la malighafi. Viwanda hivi ambavyo vinawekezwa ni lazima viwe na malighafi ya kutosha. Ni lazima twende kama Serikali tukawaelimishe na kuwashamasisha wananchi, hususan katika suala la kilimo maana malighafi nyingi zinatokana na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba sana Serikali ijiwekeze kwenye kuwawezesha na kuwajengea mazingira bora na rafiki, hususan vijana, kwenda kwenye sekta ya kilimo na kujandaa kwenye malighafi za viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uchumi wa buluu (*blue economy*). Kule Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwenye hotuba yake ile ya fedha ya mara hii, amejielekeza katika uchumi wa buluu. Na hii ndiyo agenda kubwa sana kule Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana jambo hili tulibebe kwa sababu bahari ndilo eneo kubwa sana ambalo limezunguka ndani ya nchi yetu. Naomba sana tuwe na dhamira thabiti ya kullendea suala hili la uchumi wa buluu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwenye bajeti kuna *target* ya kununua meli nne zinazokwenda kwenye *deep sea*. Naomba sana jambo hili tulianze kwa kutenga fedha zetu za ndani, tusitegemee misaada kutoka nje kuja kutuletea meli hizi, tuanze sisi. Mimi naamini kwamba kwa dhamira ya Serikali tuna uwezo wa kufanya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kununua ndege 11, tunashindwaje sisi wenyewe kununua meli za kwenda kwenye *deep sea*. Naamini kama tuna dhamira kweli ya dhati ya kwenda kwenye uchumi wa buluu, hatuwezi kushindwa kununua meli zetu sisi wenyewe na kwenda kwenye uchumi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa matumizi ya fedha; hapa tunajadili matumizi haya ya fedha, tunajadili kupitisha bajeti hizi, lakini jambo kubwa sana ambalo tunalipitisha halitaonakana na maana kama hatuendi kusimamia fedha hizi ambazo tunazipitisha hapa. Nashauri kwamba kuwe na chombo cha tathmini na ufuatiliaji, Wizara ya Fedha iwe na chombo hiki ambacho kinaifuatilia miradi

yote wakati wa utekelezwaji wake ili kuona kwamba fedha hizi tunazopitisha zinakwenda kuzingatia nidhamu ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana kuna vitu viwili tofauti; kuna nidhamu ya fedha, lakini kuna namna ya kuweza kuitumia fedha kwa mujibu wa taratibu na sheria. Watu wetu wa *procurement* walioko huko kwenye maofisi wanajaribu kutumia sheria na taratibu lakini hawazingatii nidhamu ya matumizi ya fedha. Naomba sana Serikali twende tukazingatie nidhamu ya matumizi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda kwenye maofisi unaweza ukakuta kwa mfano kitu cha kununua 500 kimenunuliwa shilingi 1,500, mara tatu au nne ya bei halisi. Tunaomba sana twende tukazingatie nidhamu ya fedha na thamani halisi ya fedha hii ambayo tunaipitisha. Tutakapofanya hivyo, naamini tutapiga maendeleo kwa hatua kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba atakapokuja Waziri hapa anipe ufanuzi kuhusu jambo la punguzo hili la *PAYE* kwa wafanyakazi. Kule Zanzibar wafanyakazi wa Muungano ambao wanafanya kazi kule mapato yale yanakwenda kwenye Serikali ya Zanzibar. Hata hivyo tunaona kwamba hakuna utofauti baina ya mwaka jana na mwaka huu; mwaka jana tulipeleka kule bilioni 21, ikiwa ni *PAYE* za wafanyakazi wa Muungano walioko kule, lakini mwaka huu pia tunaona kima ni kilekile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza, na hapa naomba pia nipate ufanuzi, kwamba je, wafanyakazi kwa maana ya watumishi wa Muungano, kule Zanzibar hawajaongezeka? Au hawapandi madaraja, au labda kima cha mshahara hakipandi? Tatizo hasa ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba mwaka jana ni bilioni 21, lakini hata mwaka huu ni bilioni zilezile 21; tatizo hapa ni kiyu gani. Je, zimebakia pale kwa sababu ya punguzo la asilimia moja au tatizo ni lipi? Naomba pia hapa atakapokuja Waziri atupe ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri sana Serikali na Wizara za Muungano na zile ambazo siyo za Muungano ziendelee kushirikiana na kufanya kazi kwa pamoja. Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamahuri ya Muungano tukifanya kazi kwa pamoja naamini tutapunguza *gap* kubwa sana la maendeleo katika maeneo yetu haya mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano yapo maeneo ambayo Tanzania Bara yako juu lakini kule Zanzibar bado wapo chini, lakini kuna maeneo ambayo kule Zanzibar tumepiga hatua lakini huku bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kule Zanzibar tuna posho za wazee, huku bado jambo lile halijatekelezaka. Kwa hiyo tukishirikiana naamini tunaweza tukapeana mawili matatu tukajua kwamba na huku tunaweza kulitekeleza jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la gharama za kuunganisha, huku ni...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Bakar kwa mchango wako mzuri.

MHE. BAKAR HAMAD BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, anaomba kutambulisha wageni wake ambao wako kwenye *practical training Benjamin Mkapa Hospital*/hana Dodoma ambao ni Ndugu Cornelius Nakalala na Magulu Barnabas; karibuni. Someni vizuri mkatibu watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Aloyce Kamamba, wajiandae Mheshimiwa Jaqueline Ngonyani pamoja na Mheshimiwa Vita Kawawa.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia kwenye Wizara hii ya Fedha; na kwanza kabisa naunga mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya ya kutuongoza Watanzania, na kwa uchapaji kazi wake; na kwa hakika anavyochukua hatua kwa haraka sana katika masuala ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, na Naibu wake, rafiki yangu Mheshimiwa *Eng.* Masauni. Kwa kweli mnachapa kazi vizuri, mnasikiliza, mnafuatilia na mwisho mmekuja kutoka na bajeti ambayo ni shirikishi. Mmewakiliza Wabunge wote mkafuatilia changamoto zinazowakabili katika maeneo yao na mwisho bajeti hii ambayo mmeitoa ni bajeti shirikishi inayojibu matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kuchangia ni mengi lakini nitachangia katika maeneo machache na yale ambayo yametolewa na wenzangu kuhusu vyanzo vya kodi na taratibu zake, ulipaji wa madeni ya posho kwa Madiwani, na yote ambayo yamechangiwa na wenzangu, naomba sana myazingatie na myafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia maeneo machache na moja nitachangia sana katika eneo la ukamilishaji wa miradi. Ipo miradi mbalimbali, miradi ya kimkakati. Wakati nachangia mara yangu ya kwanza kabisa Bungeni, hoja yangu ya kwanza ilikuwa ni ukamilishaji wa miradi ambayo imeanzishwa. Ipo miradi kama reli ya kisasa (*SGR*), ununuvi wa ndege, ufufuaji wa viwanda, miradi ya umeme hasa Mradi wa Mwalimu Nyerere na ukamilishaji wa shughuli mbalimbali hasa katika jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu tuliahidiwa kama ambavyo wenzangu wamezungumza, lami ya kilometra tatu na pale tayari kuna milioni 75 pale kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Fedha zipo pale, lakini katika ujenzi ule imepelekea mradi ule kifusi kijazwe katika barabara na

kwa maana ile hakuna shughuli za biashara zinazofanyika.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira yale hata Serikali sasa inakosa kodi, biashara haifanyiki na kwa kuwa haifanyiki wananchi wale hawawezi kulipa kodi kama inavyostahili. Niombe sana Mheshimiwa Waziri apeleke fedha za kukamilisha mradi ule ili wananchi wafanye biashara na sisi kama Serikali tuweze kupata kodi. Hii inakwenda sambamba na umalizaji wa barabara kama ambavyo nimezungumza ni umalizaji wa miradi. Kuna barabara inayotoka Kankoko kwenda Kinonko kwenda Nyakiyobe kwenda Ngwarama, kwenda Kabare na kufika kwenye mpaka wa Muhange. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo limejengwa soko kubwa, kuna millioni 585, majengo yamekamilika, lakini hatuyafaidi vizuri kwa kuwa hakuna barabara inayokwenda pale. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri katika bajeti hii kwa kuwa ndio anamalizia malizia atenye fedha za kumalizia barabara ile ili soko liweze kufanya kazi na sisi ile biashara ya mpakani tuweze kupata kodi. Kwa hiyo ni kuweka fedha, lakini wakati huo huo Serikali nayo itapata fedha kupitia mpaka ule kupitia kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo; katika nchi yetu kilimo kinatoa ajira katika eneo kubwa sana, lakini yapo mambo ya kufanya. Moja; ni kuajiri watenda kazi, hatuna Maafisa Kilimo kwenye vijiji. Naomba sana katika bajeti hii Mheshimiwa Waziri anapohitimisha aangalie makandokando, vifedha vichache vinavyobaki, basi aweze kupeleka fedha kwa ajili ya ajira ya watumishi katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inakwenda sambamba na watalaaam kupima udongo. Kwenye kilimo ni sehemu ambayo ajira inafanyika kwa ukubwa sana, lakini wananchi wetu ili mradi anaona ardhi hajui ardhi ile inafaa kwa zao gani, analima tu. Niombe taratibu zifanyike, ardhi ipimwe, ionekane inafaa kwa zao gani, ndipo wananchi waweze kulima pale. Hii iende sambamba na uongezaji wa thamani

ya mazao kwa maana ya kupeleka mashine za kuchakata mazao mbalimbali kama muhogo, mahindi na kadhalika ili mazao yetu yaweze kuongezewa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pembejeo ni muhimu sana kwenye kilimo, lakini hazi pelekwi kwa wananchi kama inavyostahili. Hii inakwenda sambamba na mbolea, lakini kuna suala la dawa, wananchi wanaanza kilimo bila mbolea, inafika muda ambao mbolea ingeweza kutumika kwa ajili ya kumfanya mwananchi alime vizuri hawezi kulima vizuri kwa sababu hana mbolea. Kwa hiyo mbolea ipelekwe, lakini dawa vilevile ziweze kupelekwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wilaya ambayo natoka Wilaya ya Kankoko ili kumbukumbu ziwepo, ni katika wilaya ambayo tunalima sana zao la alizeti. Kwa hiyo wakati inaandaliwa mipango mbalimbali kwa ajili ya kilimo cha alizeti, basi Wilaya ya Kankoko nayo iangaliwe na iwekwe kwenye mikakati. Hii inakwenda sambamba na Mkoa mzima wa Kigoma ambao zao letu ni chikichi, tuongezewe nguvu ya kutosha ili zao hili la chikichi liweze kulimwa kwa kiwango kikubwa na kujibu changamoto ya mafuta ambayo inakabili nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni pamoja na zao la miwa ambalo kwa kipindi kirefu limezungumzwa katika Mto Malagarasi, eneo lile ni zuri sana na linafaa kwa kilimo cha miwa. Niombe nalo katika mkakati wa jumla kuongeza uchumi wa nchi liweze kuwekwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la elimu, tumefanikiwa sana kwenye upande wa elimu, lakini Walimu hawatoshelezi. Kuna idadi ya Walimu imetajwa ya 6,000, hawa hawatoshi. Niombe katika mkakati wa jumla walimu waongezwe ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba za Walimu kwa sababu wanakaa mbali ikiwa ni pamoja na kujenga madarasa hasa mwishoni mwa mwaka inafika hatua sasa ni kukimbizana. Inafika hatua Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa hawawezi kwenda likizo kwa sababu wanatakiwa sasa wasimamie ujenzi wa madarasa. Naomba sana madarasa

haya yajengwe mapema ili wanafunzi nao wawe wamejiandaa vizuri kwa ajili ya kuanza masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wasichana; watoto wa kike wana changamoto nyingi pamoja na kwamba na wa kiume nao changamoto nyingi. Sasa niombe Waziri wa Elimu akisaidiana na TAMISEMI na Wizara ya Fedha kama ambao wanashikilia kihenge kikuu, waweke mkakati wa makusudi kujenga mabweni hasa maeneo ya vijijini ili watoto wetu wa kike waweze kupata sehemu ya kuishi vizuri na waweze kusoma, watumie muda mwingu kusoma badala ya kutumia muda mwingu kukimbizana na changamoto ambazo zinawakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii iende sambamba na ukamilishaji wa maboma ya maabara, maboma ya madarasa pamoja na maboma ya nyumba za Walimu. Naomba sana Serikali ichukue hatua ya makusudi ili kukabiliana na changamoto hizi na nina hakika watoto wetu watasoma vizuri na wataweza kukabiliana na changamoto ambazo zinawakabili na mwisho elimu itaweza kuwafikia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu nilitaka nichangie hayo, lakini yachukuliwe kwa ujumla wake ili kufanikisha maeneo yote kukamilisha miradi kwa wakati, lakini kuongeza nguvu katika madarasa na nyumba za Walimu ambazo zinajengwa katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa namwita Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani jiandae Vita Kawawa, jiandae Mheshimiwa Neema Mwandabila.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uzima ili niweze kusimama hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kuzungumzia Mkoa wa Ruvuma, Mkoa wa Ruvuma kwa maana ya kuugawa. Tunapozungumzia maendeleo, ukuaji wa uchumi katika nchi yetu ya Tanzania, imetosha tu kwamba tuzungumzie pia na mikoa ambayo ni mikubwa sana, mikoa ambayo kwa ukubwa wake inasababisha huduma za msingi zinashinda kufika kwa wakati na kuweza kutosheleza kwenye maeneo husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma una *population* ya watu 1,376,891 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 na sisi kule watu wa Ruvuma tunazaana sana, mpaka sasa hivi maana yake wakija kufanya sensa tunaweza tukawa tumefikia watu 2,000,000. Kwa misingi hiyo, naomba sana Mkoa wetu wa Ruvuma uwe ni miongoni mwa mikoa inayoenda kugawiwa ili tuweze kupata mikoa miwili sasa uwe Mkoa wa Ruvuma na uwe Mkoa wa Selou na vigezo viro na niseme tu kwamba hii ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alipokuja Mkoani kwetu Ruvuma alizungumzia kuugawa huu mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa huu kwa kukuthibitishia tu naomba nitoe vigezo vya mikoa mingine ambayo ina *population* ya watu wachache sana, lakini imepata mikoa. Nataka nizungumzie Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Katavi una *population* ya watu 564,000 tu, tofauti na Mkoa wa Ruvuma ambao kwa sasa una watu 1,376,891. Mkoa wa Njombe una *population* ya watu 702,000 tu, Mkoa wa Lindi una *population* ya watu 964,000 kwa hiyo ni wazi kwamba Mkoa wa Ruvuma unakidhi vigezo vya kuongeza mkoa, kwa hiyo tunaomba tupate mkoa mwingine mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Miundombinu ya barabara, lakini pia nimshukuru Waziri wa Fedha kwa namna ambavyo ametuheshimisha Wanaruvuma na niseme tu kwamba nampa *big up* sana Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Peramiho ambaye barabara hii ya Likuyufusi – Mkenda inapita kwenye jimbo lake. Kwa pamoja

ye ye akifuatilia kwa ukaribu kabisa sambamba na mimi winga machachari ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nimekuwa nikiizungumzia sana barabara hii yenye urefu wa kilometra 124 inayotoka Likuyufusi kwenda Mkenda ambayo inaunganisha Nchi ya Tanzania na Mozambique.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha akumbuke kwamba, sasa hivi hii ni bajeti yake ya kwanza akiwa Waziri wa Fedha na kikubwa kinachotakiwa ni kuendelea kujenga nchi yetu ya Tanzania iendelee kukua kiuchumi. Kwa hiyo barabara hii atakapojenga itaendelea kufungua fursa nydingi za kiuchumi na kodi italipwa na nchi yetu itaendelea kukua, wananchi watapa ajira na wananchi wetu wa Mkoa wa Ruvuma wataendelea kunufaika na rasilimali za nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mama yetu jemedari Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya, mwanamke shupavu, mwanamke mahiri, kwanza Mungu kamjalia, kwanza kabisa ukimwangalia sura yake nzuri, sura ya upole, mama mwenye upole, mama mwenye upendo. Kwa misingi hiyo mama huyu ana upendo mpaka ndani ya moyo wake, kwa bajeti hii ambayo imeletwa safari hii, ni bajeti ya kupigwa mfano, bajeti nzuri ambayo imeenda kugusa moja kwa moja kwa wananchi wanyonge na kukwamua matatizo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaombe kupitia Bunge lako Tukufu, Watanzania wote waweze kumuunga mkono Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kulipa kodi. Watakapolipa kodi ndipo hapo tutapata maendeleo kupitia ujenzi wa barabara, umeme, maji, afya na elimu. Kwa misingi hiyo kulipa kodi ndiyo maendeleo ya nchi yetu. Niseme tu, kupitia malipo mazuri ya kodi, basi maana yake itakwenda kuboresha hata sisi Wabunge hapa, amesema mama yetu Mheshimiwa Samia kwamba anaanza na kuboresha mishahara ya watumishi, maslahi ya watumishi ikiwa pamoja na kuwaongeza vyeo vyao ili waweze kuendana na wakati huu wa sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu, atakapoboresha baada ya kodi kulipwa na sisi Wabunge hapa tutakwenda vizuri, mambo yetu yatakwenda vizuri. Itoshe tu kusema kwamba ikimpendeza Mungu panapo majaliwa kama jina litarudi wakinipa hawa nafasi maana yake nitasimamia katika kamisheni ya Bunge kuhakikisha kwamba maslahi ya Wabunge kuititia safari za kwenda nje ya nchi, kwa sababu Mbunge kama Mbunge ni lazima upate *exposure*, kwa maana ya kwenda kujifunza nje ya nchi katika nchi ambazo zimefanikiwa sana kwenye miundombinu, afya, elimu na mambo mengine mengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bila Mbunge kupata *exposure* maana yake tunakuwa tuna mawazo ya kwetu tu hapa ndani ya nchi bila kwenda nje ya nchi. Hii niwaambie tu ndugu zangu kama mkinwezesha mambo hayo yakakaa vizuri maana yake nitasimama kindakindaki. Mjue kabisa kwamba uwezo ninao wa kufanya hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nizungumzie suala la namna ambavyo Mama Samia ameboresha kwenye masuala ya Madiwani. Madiwani sasa hivi wanakwenda kulipa pesa zao kuititia Serikali Kuu. Kwa msingi huo kulipwa tu kuititia Serikali Kuu haitoshi, ilitosha tu hawa Madiwani waongezewe pesa. Madiwani hawa ndio ambao wanafanya kazi asubuhi, mchana, jioni wao ndio wanakutana na wananchi kule chini kwenye *grass root* kwa hiyo hawa Madiwani katika utendaji wao wa kazi bado mzunguko wa maeneo yao waliyonayo ni mkubwa mno kiasi ambacho sasa yule Diwani, wakati mwengine unakuta Diwani ana vijiji 12, 15, vijiji nane, vijiji tisa au vijiji 20. Kwa hiyo, naomba kuititia bajeti hii itoshe tu kwamba Waheshimiwa hawa Madiwani waweze kutengenezewa utaratibu wa kupata mkopo kwa ajili ya kupata usafiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo usafiri utawasaidia kama vile ambavyo Makatibu Tarafa wameweza kusaidiwa usafiri, wakapata pikipiki, lakini pia Watendaji wa Kata wameweza kusaidiwa wanapata posho. Waheshimiwa

Wabunge mengine hatuwezi kusema hapa, mkinipa kale ka mambo kale ndio nitasema vizuri huko na nataka niwaahidi kwamba nitakuwa shujaa wenu na sisi Wangoni tulishakuwa mashujaa, kwa hiyo huu ni mwendelezo tu, tulikuwa mashujaa, tumeigana vita na Wajerumani na hata nyie mkawa mna nafuu huko mliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa aje Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, wajiandae Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimei na Mheshimiwa Felista Njau.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Narudia kumpongeza sana Waziri wetu wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba, Naibu Waziri *Engineer* Masauni. Naomba pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ndugu yangu Mheshimiwa Daniel Sillo, Iakini na Makamu Mwenyekiti *CPA* Mheshimiwa Omari Kigua kwa kutuwakilisha vyema kama Bunge kwenye Kamati ya Bajeti na hasa katika vikao vya mwisho vya majumuisho ya bajeti hii. Tunawashukuru sana Kamati ya Bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono bajeti hii na mapendekezo yake yote. Naiunga mkono bajeti hii kwa sababu inakwenda kuendelea na kukamilisha miradi ya maendeleo au miradi mkakati ambayo inafanyika sasa hivi *Stigler's Gorge*, *SGR* na mingine mikubwa. Bajeti hii inaenda kuendeleza na kukamilisha miradi hiyo, Iakini inaenda pia kuanzisha miradi mipya ambayo tumeainishiwa katika bajeti hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia bajeti hii inaelekea kwenda ku-*trickle down economic* na ku-*stimulate economic activities* zilizopo kwa wananchi wake. Kwa nini nasema hayo bajeti hii pia leo tumeambiwa inakwenda kupandisha madaraja ya wafanyakazi. Naomba niseme hapa mpaka

leo hii wafanyakazi karibu zaidi ya 86 wameshapandishwa madaraja na *automatic* wanaenda kupandisha mishahara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya upandishaji wa mishahara hii itaigharimu Serikali bilioni 300, lakini pia malimbikizo ya madeni ya wafanyakazi karibu bilioni 96 yanaenda kulipwa. Kwa hiyo ndiyo maana naipongeza Serikali na wafanyakazi maslahi yao yakinazamwa na yakipanda maana yake ni nini? Hawa ndiyo *spender* wakubwa na hawa waki-*spend* ndiyo Serikali inakusanya kodi yake. Hizi kodi zote tunazozisema hapa za simu sijui za nini tulizopendekeza watumiaji wakubwa wakiwemo pia wafanyakazi, ndiyo wanafanya miamala mikubwa, ndiyo wanaotumia hela nyingi kupeleka sehemu mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na Serikali yake wanayoiongoza. Tangu Mheshimiwa Rais ameapishwa Samia Suluhu Hassan katika wilaya yetu ya Namtumbo katika kipindi hiki toka Aprili mpaka sasa hivi ametuletea bilioni mbili na milioni mia saba sabini na saba na milioni thelathini katika miradi ya elimu, afya, *program* endelevu ya maji safi na mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametuletea pia milioni 500 za barabara kwa ajili ya *TARURA*, lakini pia tunategemea kupata milioni 600 kwa ajili ya sekondari zetu za kata, naomba sana nimpongeze Rais wetu na Serikali yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye aya ya 110 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, alizungumzia eneo la utamaduni wa kuheshimu mali na rasilimali hapa nchini; mali za Umma na binafsi. Naomba nimnukuu: “*kwa upande wa Mali za Umma lazima tutangulize uzalendo na uadilifu tunapotekeleza majukumu yetu. Serikali inapoteza fedha nyingi kwenye kutekeleza Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa kutojali thamani ya fedha kwa miradi. Watumishi wa Serikali wasio waaminifu wamekuwa wakishirikiana na*

wafanyabiashara wasio waaminifu kuongeza gharama za miradi ikilinganishwa na gharama halisi ingawa wanafuata taratibu zote za manunuzi. Taratibu za manunuzi zinapokamilika, watumishi na wafanyabishara hawa hugawana fedha na kiasi kidogo tu kilichosalia ndicho kinaelekezwa kwenye miradi husika na hatimaye miradi hiyo kuwa chini ya kiwango.” Mwisho wa kunukuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno alisema Waziri wa Fedha katika hotuba yake. Ni kweli, nakubaliana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuliona hili. Kuna haja ya kukazia eneo hili, kuheshimu kutunza Rasilimali za Umma, kwani ni kweli Serikali inapoteza fedha nyingi kwenye kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa, tumepata zaidi ya shillingi 2,700,000,000 zinakwenda katika Halmashauri zetu. Miradi hii inaongozwa na bajeti au inaongozwa na mwongozo wa kuhudumia miradi hiyo kwa *Force Account*. Mwongozo unasema, kuna Kamati ya Ujenzi, Kamati ya Manunuzi, Kamati ya Mapokezi na Kamati ya Ufuautiliaji. Kamati hizi ni za wale wananchi husika pale, lakini watumishi wa Halmashauri wanakuwa Wajumbe kama washauri na kusimamia ili shughuli iende sawa sawa kwa mujibu wa taratibu na sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo inajitokeza baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu, wao sasa ndio wanachukua majukumu yale ya kufanya ununuzi na kufanya ujenzi. Sasa hii inasumbua sana na inaleta *audit query* kwenye Halmashauri zetu. Leo hii sisi tuna *audit query* pale zaidi ya milioni 120 kwa ajili ya mradi tu ambao haukuuata taratibu hizi. Kwa hiyo, naishauri Serikali, tunaomba mumpe nguvu Mkuu wa Mkoa wawe wanasmamia miradi hii ya maendeleo. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa isimamie kama taratibu zinafuatwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni aya ya 75; Serikali katika eneo la kilimo, imependekeza katika miradi ya umwagiliaji kwamba itakuwa inatoza 5% ya mavuno katika

miradi ile ya umwagiliaji. Nia ni njema, naiunga mkono kwa ajili ya kuendeleza kufanya *service* miradi yetu ya umwagiliaji. Hata hivyo, nina mapendekezo mawili. Kwanza, kuangalia hii miradi yote. Kuna miradi ambayo fedha nyngi za umwagiliaji zimeingia kule, lakini hajakamilika miaka nenda, miaka rudi. Naamini katika kanzidata ya Serikali inaonesha kwamba kuna fedha zimepelekwa katika miradi lakini miradi ile haikukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri hapa, kwamba kwa wale wasiokuwa waaminifu, hawakukamilisha miradi, sasa tozo hii lazima yatoke maelekezo kwamba kwanza tukakamilishe ile miradi ndipo tozo zianze kuchukuliwa. Maana yake tukitoa tu tozo, miradi isipokamilika na ile ambayo *hai-perform* vizuri, tozo zitaanza kuchukuliwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima ifanyike tathmini ya miradi ambayo hajakamilika ili tuikamilishe ndiyo tozo hizi ziweze kuwapa wale wakulima wananchi kule, kuliko kupeleka tozo, wataenda kukamatwa hawajalipa tozo, wakachukuliwa tozo zao, miradi ile haikukamilika. Pili, tozo hizi tuelekeze wazi wazi zinakwenda wapi? Kama zinakwenda kwenye Tume ya Umwagiliaji, tujue; zisije kuwa tozo hizi zinakwenda kuchukuliwa tu kwenye Halmalshauri halafu zinaanza kupangiwa matumizi mengine baada ya matumizi husika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nami niungane na wenzangu, kwanza kabisa kwenye hili suala la Madiwani, Watendaji na Makatibu Tarafa kupewa na Serikali fedha zao na posho, naunga mkono kabisa. Naipongeza sana Serikali kwa kuamua kufanya jambo hili jema sana kwa ajili ya watumishi hawa. Ushauri wangu ni kwamba...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Neema Mwandabila, jiandae Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea na Mheshimiwa Felista Njau.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia bajeti hii iliyopo mbele yetu ambayo imewasilishwa ili tuweze kujidili na kuendelea kuweka mapendekezo yetu ambayo tungependa kuona Serikali inayafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa namna ambavyo ina watu makini. Naamini haya tunayoyaongea watayachukulia kwa uzito wake na kwenda kuyafanya kazi. Kipekee pia niungane na wenzangu kumpongeza Mama yetu, Mheshimiwa Samia. Mimi ni mmoja kati ya watu wanaoamini kwamba mama hajawahi kufeli. Kwa hiyo, nila matumaini makubwa kwamba mama atatuletea mambo mazuri ambayo yataenda kuleta mabadiliko katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najivunia kutoka katika Mkoa wa Songwe, mkoa ambao ndiyo unaongoza kwa ukusanyaji kodi kwa ile mikoa ya ukusanyaji kodi wa kat, Mkoa wa Songwe ndiyo unaongoza. Kwa hiyo, nilitaka nitunze hiyo kumbukumbu vizuri. Kwa hiyo, ninapokuwa nachangia haya nataka kuonyesha kwamba Mkoa wa Songwe ni katika maeneo ambayo Serikali inaweza ikapata fedha nyingi kama wataamua kuufanya mkoa wa kimkakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, nilitaka kuongea kwamba ujenzi wa *dry port* kwa Mkoa wa Songwe eneo la Mpemba pale Tunduma ni kitu kisichoepukika. Tunayasema haya tukiwa tunaamini kabisa Kariakoo na Bandari ya Dar es Salaam kumeshakuwa *busy* sana. Kama Reli ya *TAZARA* itatumika ipasavyo, ikawezeshwa na *dry port* ikajengwa Mpemba, niwaambie kabisa, Kariakoo nyingine itaenda kuota pale Tunduma. Pale itakuwa chanzo cha kuweza kutengeneza *free market* katika eneo la Tunduma. Kwa maana hiyo, uchumi unaoendelea Kariakoo utakuwa

umehamia Tunduma. Kwa hiyo, tutakuwa tumeongeza maeneo ambayo yanaipatia Taifa letu kipato. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo la *dry port* pale Tunduma, napenda pia kuongelea suala la kupunguza msongamano wa magari pale Tunduma. Ni kweli kuna mkakati wa ujenzi wa barabara, lakini ipo haja ya kufanya haraka kuhakikisha barabara ile ya pale Tunduma inayoingia mpakani inatanuliwa ili magari yasipate msongamano wa kuelekea Zambia. Kwa sababu kwa kitendo cha magari kukaa njiani muda mrefu pale, kwa namna moja au nyingine yanaiingizia hasara Taifa kwa maana ya kwamba magari hayavuki mengi kwa wakati ipasavyo; na pia hakuna barabara ya mchepuko endapo barabara ile itapata *breakage*, hakuna barabara ya kutoa magari yapite njia mbadala yaweze kwenda kuingia boda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo mambo pia naomba kama Wizara yayachukulie kwa *u-serious* wake na kuyafanya kazi haraka. Uchumi wa Taifa hili kwa upande wa Tunduma kama kweli patapewa kipaumbele, naamini kabisa Taifa litapata mapato mengi kutoka eneo la Tunduma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye suala la VAT. Sheria ya Ongezeko la Thamani inasema kwamba ili mtu aweze kusajiliwa kuwa Wakala wa kukusanya VAT, awe na mzunguko wa shilingi milioni 100. Ukijaribu kulitazama kwa kina hili jambo linakuwa ni kama ni gumu katika utekelezaji wake kwa wale Maafisa Mapato wanaokuwa wamepewa hii kazi. Unapoongelea mzunguko wa shilingi milioni 100 ni kitu cha kawaida kwa wafanyabiashara wadogo wadogo kupata mzunguko wa shilingi milioni 100. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema hiyo shilingi milioni 100, ina maana unawalenga wale watu wanaofanyabiashara ya rejareja. Unaposema ongezeko la thamani, hatuna maana kwamba bidhaa hiyo moja iweze kuongezeka thamani kila inapoenda kwa muuzaji mwingine.

Ushauri wangu ulikuwa ni kwamba, tungependa kuiona Serikali inafanya mabadiliko katika eneo hili. Kutoka shilingi milioni 100, basi iende kufanya kuwe na shilingi milioni 300. Unapomwongelea mfanyabiashara mwenye mzunguko wa shilingi milioni 300, huyu ni *stable person* ambaye ye ye kwa shilingi milioni 300 yake hiyo anakuwa ni *supplier* wa bidhaa na siyo yule mfanyabiashara wa rejareja.

Kwa hiyo, kama kweli Serikali ikiweza kuliona hili na kulifanya kazi. Ina maana kwamba kwa namna moja Serikali itapunguza mgogoro na wafanyabiashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu kule mpakani tuna mgogoro mkubwa sana kati ya *TRA* na wafanyabiashara. Wafanyabiashara wengi hao wenye mzunguko wa shilingi milioni 100 wamekuwa wanalazimika kufunga biashara zao kwa sababu tu hawawezi kulipa hilo ongezeko la thamani. Kwa kitendo cha kuwaingiza wao kwenye ongezeko la thamani, ina maana kwamba unawafanya washindwe *compete* kibiashara katika lile eneo la Tunduma, kwa sababu wapo ni *registered* wapo amba ni *un-registered*. Wale wanaokuwa *registered* ina maana kwamba sasa wanashindwa kuuza bidhaa zao kwa ile bei ambayo ipo sokoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo la kuongeza kutoka shilingi milioni 100 hadi kwenda shilingi milioni 300, kinachofanya ni kwamba, wafanyabiashara wengi pia wanafilisika, kwa sababu kinachokuja kutokea yale malimbikizo inakuwa kama wanapokwa zile fedha zao kiasi kwamba wanakuwa hawezi tena kuendesha biashara zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuongelea suala la ushuru wa forodha wa vitenge. Kuwepo kwetu mpakani tunaendelea kujifunza mengi. Kwa wastani kontena karibu milioni 500 zinapita kuelekea Zambia na Kongo pale katika mpaka wa Tunduma. Mwisho wa siku nikuhakikishie, pakifanya uchunguzi zile kontena 500 sidhani kama zote zinatumika kwa Zambia au kwa Kongo, zinarudi tena

Tanzania. Changamoto iliyopo ni kwamba kodi ya vitenge kwa Tanzania ni asilimia 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote ni mashahidi kwamba vitenge vinavyotengenezwa nchini havina *quality* hiyo ambayo tunataka kuvilinda. Vingekuwa ni vitenge vizuri, ambavyo vina mvuto, naamini kabisa ingekuwa sawa kweli kuweka hiyo kodi ambayo ipo. Mwisho wa siku ukienda Zambia unakuta wao wana kodi ya asilimia 20, ukienda Kongo ni asilimia 25. Unapopitisha kontena la *fourty fits* kwa Tanzania unalipa zaidi ya shilingi milioni 100, lakini kwa Zambia na Kongo inakuwa ni chini ya shilingi milioni 30. Katika hali ya kawaida *gap* ya shilingi milioni 70 siyo ya kitoto, ni fedha nyingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku, pale mpakani tuna watumishi 12 tu ambao wana-deal/na mpaka Maafisa Kodi, hawawezi kukimbizana na kontena 500 zote hizi kwa mwezi.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza sasa kwamba kuitia hilo ni kweli kabisa na jambo hilo limesababisha wafanyabiashara amba walikuwa wanafanya biashara Kariakoo amba walikuwa ni majirani zetu; Zambia, Malawi, Rwanda na Burundi amba walikuwa wanajaa pale Kariakoo kununua bidhaa hii ya kitenge, sasa hivi hawaji na wafanyabiashara hawa wamehama, wanaenda kwenye nchi hizo hizo kwenda kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ni kweli kabisa hata Kariakoo wamekimbia, kontena moja shilingi milioni 300. (*Makofii*)

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niseme tu, taarifa yake naipokea na hali halisi ndiyo ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema heri nusu shari kuliko shari kamili. Kitendo cha kwamba tunapoteza fedha nydingi kisa tu, kuhakikisha tunalinda viwanda vyetu vya ndani ambavyo havifanyi vizuri, tunakuwa hatujitendei haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niseme, sisi wenywewe ndiyo tunahamasisha magendo; na kwa...

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Niko hapa.

MWENYEKITI: Taarifa.

TAARIFA

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa kweli niungane na hawa waliopita kuhusiana na masuala ya vitenge. Kweli kuna jambo inhabidi tuliangalie vizuri sana. Nasema hivyo kwa sababu hata mimi nililifuatilia na nikalishughulikia suala hilo kwa muda mrefu. Kuna changamoto kubwa na wale akina mama wamekuwa wakilipa kodi ya kutosha. Tunalinda viwanda vya ndani ambavyo na vyenyewe ukivichunguza wanadai kwamba wanaenda kununua huko huko nje, halafu wanarudi wanasema wametengeneza ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliangalie hilo suala kwa umakini kwa faida ya nchi yetu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Taarifa hiyo, Mheshimiwa Neema.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Manyanya. Tunachohitaji ni pesa za kuendesha Taifa letu. Tuangalie namna zote ambazo zinazuia tusipate pesa. Suala la vitenge nimeona kwenye hotuba inasema kwamba wanamwachia

Kamishna. Tuwe wakweli, kumwachia Kamishna wa *TRA* ni kuongeza urasimu na kutengeneza mianya ya rushwa. Kwa maana hiyo, nilitamani hili wakalitafakari na waje na *percent*, ile asilimia ambayo kweli kama Taifa tutakuwa tunajua hiki tutapata na hiki kitatuongezea kitu kwenye Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme kabisa magendo kwa nchi hii tusiendelee kuhamasisha kwa kuweka kodi zisizolipika; na pale mpakani nimeshasema watumishi ni 12, sidhani kama *wata-deal* na sukari, *wata-deal* na magendo yote yanayopita pale, hawataweza. *Otherwise* iongezeke timu ya kufanya kazi katika mpaka ule. Ule mpaka ni wa faida, ule mpaka una pesa, ule mpaka unaweza ukalisadia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nirudi kusema kwamba nina maombi mengine maalum kwa Wizara. Songwe tungependa kuona kilimo cha Alizeti na Ufuta kinapewa kipaumbele. Nimeona wameitaja mikoa mitatu. Taifa hili tunahitaji mafuta, tunahitaji mbegu za mafuta zilimwe kila sehemu. Songwe tumekuwa tunalima mahindi, ndiyo yenyecheo hayauziki. Hatuna kilimo ambacho tunaweza tukajivunia kwamba hiki ni kilimo cha biashara.

Naomba watizingatie watu wa Mkoa wa Songwe kwa kuhakikisha zao la alizeti na ufuta linapewa kipaumbele na wananchi wanahamasishwa ili tuweze kuchangia uchumi wa Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuongelea suala la *TFS*. *TFS* kuna changamoto kubwa. Wanatoa vibali kwa wananchi vya uvunaji wa mkaa, mvunaji wa mkaa anapata nafasi ya kuweka watu wake wa kumvunia mkaa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia kidogo, samahani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuvuna mkaa vibali vyaa kutoa mzigo porini watu wautoe kwa wakati havitolewi kitu ambacho wafanyabiashara wengi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Neema, unaweza ukamwandikia Waziri wa Fedha kwa sababu wengine watakosa nafasi.

Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimei, jiandae Mheshimiwa Felista Njau, jiandae Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini.

MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini napenda tuweke taarifa sahihi, jina langu ni Alfred Kimea na sio Kimei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa hii nafasi, wenzangu wameongea mengi. Ukianza kufuatilia utaona kila mchango ambaa unatakiwa kwenda kwa Wizara hii kwenye hii Bajeti Kuu ya Serikali, imeshaongelewa. Napenda tu niongezee machache na sehemu nyingine niongezee ambapo palishaongelewa kwa sababu mengi yameshaongelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza napenda kumshukuru Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya. Tusiposhukuru kwa kazi kubwa anayoifanya, tutakuwa hatumtendei haki mama huyu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kichache tangu tuwepo Bungeni mambo makubwa, aidha yameshafanyika au tumepewa ahadi kubwa kwa ajili ya kuendeleza majimbo yetu. Mfano tu kwenye jimbo langu la Korogwe Mjini, kwa kipindi hiki kidogo tumeshaandaliwa zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya sekta ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu ni la Korogwe Mjini, kwa kipindi hiki kidogo tumekwisha kuandaliwa zaidi ya bilioni mbili kwa ajili ya sekta ya maji. Sekta ya barabara

ikiwemo *TARURA* tuna bajeti ya karibu 1,300,000,000 kwa hiyo, hii ni kitu kikubwa ni lazima tumshukuru Mama kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye bajeti sasa, mchango wangu utakuwa wa sehemu mbili, moja nitapongeza lakini sehemu ya pili nitashauri sehemu chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa pongezi kwa kweli tunamshukuru na tunampongeza kweli Waziri, wetu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu pamoja na kaka Mheshimiwa *Engineer Masauni* kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa kutuletea hii bajeti nzuri. Kwa kweli ni bajeti nzuri ambayo inatakiwa kupongezwa na ninazo sababu ya kupongeza hii bajeti siyo tu kama nafuata mkumbo wa watu wameipongeza bajeti na mimi nipongeze lakini ninazo sababu kabisa za msingi kwa ajili gani naipongeza hii bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza ni kweli hii bajeti imekwenda kumgusa kila mtanzania. Kila Mtanzania ameguswa kwenye hii bajeti kuanzia wafanyakazi tumeona wanakwenda kupandishwa vyeo na hii tulipigia kelele sana mimi nilikuwa mmoja wapo nilisema walimu hasa wa vyeo vikuu ambao mimi nilitoka huko nilikuwa mmoja wao walikuwa wanastahili kupandishwa madaraja lakini kwa muda mrefu hawakuwa wanapandishwa madaraja. Lakini hii bajeti sasa imekuja na dawa hiyo; walimu wa Vyuo Vikuu wanakwenda kupandishwa madaraja. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwa ajili ya kuona hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia bajeti hii imegusa au imezingatia maoni ya Wabunge na Wadau wengine wengi. Hajakaa tu chini kuandaa bajeti, hajachukua *template* za bajeti zilizopita, amekaa chini kuangalia Wabunge waliongea kitu gani, alikaa chini kuangaliwa wadau wanazungumza kitu gani akaja na bajeti nzuri ambayo imezingatia maoni ya watu hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauri juu ya *TARURA* kuongezewa bajeti na kweli *TARURA* imekwenda kuongezewa bajeti. Tulishauri Wizara ya Afya iongezewe bajeti na wamefanya hivyo. Tulishauri miradi mikubwa iende kufanyika na kweli wanakwenda kuiendeleza ile miradi mikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ndugu yangu Mheshimiwa Waziri kwa kuwa umesema unakwenda kufanya vitu hivyo, kweli tunataka hivyo vitu vikafanyike. Mfano mmojawapo; tunakwenda kushika kodi kwenye *line* za simu na tunakwenda kuchukua kodi kwenye mafuta na alisema *specific* kwenye mafuta shilingi 100 inakwenda *TATURA* na kwenye *line* inakwenda kwenye huduma za afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania siyo watu wajinga, wanakwenda kuhesabu kitu gani kinakwenda kupatikana na kitu gani kinakwenda kufanyika. Kwa kuwa ulisema *specifically* hii inakwenda kwenye afya kweli tunataka iende kwenye afya. Tumesema hii inakwenda *TARURA* kweli tunataka hii iende *TARURA*. Kwa hiyo, tunakupongeza lakini tunataka kweli ahadi yako uende kuitimiza kwa ajili tuna mwaka mmoja tu, mwakani siku kama hizi tufarudi tena tukikupitishia bajeti nyingine tunataona hiki kitu umekifanya kwa namna gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sehemu nyingine ya mwisho, kwa ajili gani naipongeza hii bajeti kama kauli mbiu ya nchi yetu ni kuinua uchumi wa viwanda ni kweli bajeti hii imeonesha dhamira yake ya kwenda kuinua uchumi wa viwanda. Tumeona wakipunguza baadhi ya ushuru wa forodha kwa bidhaa ambazo zinakwenda kutumika kwenye viwanda vyetu. Lakini pia wameongeza ushuru wa forodha kwenye bidhaa ambazo zinatengenezwa Tanzania ili kuweza kuinua sekta ya viwanda kwenye nchi yetu. Kwa hiyo, tunaipongeza bejeti hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mchango wangu utakuwa na sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni pongezi ambayo nimekwisha kutoa lakini sehemu ya pili ni

maoni yangu kwenye baadhi ya maeneo machache ambayo naona yanahitaji kufanyiwa marekebisho. Ya kwanza, nitoe maoni yangu kwenye hii sheria ya kodi ya majengo. Kweli Mheshimiwa Waziri nakupongeza kwa hii kodi mpya au namna ya utozaji wa hii kodi mpya. Kama tunavyofahamu ni kweli kodi yoyote ambayo inaanizishwa ni lazima iwe nyepesi kukusanya. Kweli nakupongeza hii kodi ambayo umeianzisha itakwenda kuwa rahidi kukusanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kodi mpya inayoanzishwa ni lazima iwe na urahisi wa kulipa. Ni kweli walipo kodi wetu itakuwa rahisi kuilipia hii kodi ya majengo kuliko mwanzo ilivyokuwa. Lakini kuna *principle* nyingine ya kodi inaitwa *principle diversity* kwamba mtu yoyote ambaye anakusudia kulipa hii kodi kweli anatakiwa kulipa hiyo kodi na kweli kodi hii itakuwa vigumu sana kwa mtu yoyote ambaye kakusudia kulipa kukwepa kodi hii. Kwa hiyo napongeza kwa jitihada hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti kodi hii inachangamoto kidogo ambazo kidogo ambazo lazima Mheshimiwa Waziri waweze kuzi-*address*. Ya kwanza tunafahamu kodi yoyote kuna *principle* muhimu sana ambayo hii kodi inakwenda kinyume na *principle* hiyo. *Principle* ya *Equity*, kwamba watu wenye kipato sawa waweze kulipa kodi sawa; lakini watu wenye vipato tofauti basi kodi iwe tofauti, mwenye kipato kikubwa alipe kodi kubwa na mwenye kipato kidogo alipe kodi ndogo. Lakini Mheshimiwa Waziri utakubaliana na mimi kabisa kwamba kodi jinsi ilivyo wewe Mheshimiwa Waziri utakwenda kulipa shilingi 1,000 kwa mwezi, na yule bibi yetu kule nyumbani kwetu kwa Mndolwa, kule nyumbani kwetu *Old Korogwe* naye atakwenda kulipa sawasawa na wewe ulivyalipa. Hii siyo sawa kabisa Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, lazima hii kodi ije itengenezwe namna kwamba mwenye kipato kikubwa atalipa kodi kubwa na mwenye kipato kidogo atalipa kodi ndogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara ya hiki, moja itawadhulumu wale watu wanyonge; lakini namba mbili

Serikali haitakusanya mapato yake sahihi kwa ajili mtu mwenye kipato kikubwa atalipa sawa na yule mwenye kipato kidogo. Nini kifanyike; maoni yangu, nadhani haya yataondo ile shida ambayo Wabunge wengi wameiongea. Maoni yangu ni kwamba kwanza *assumption* zangu ni kwamba mtu ambaye anatumia *unit* nyingi atakuwa na kipato kikubwa kuliko mtu anayetumia *unit* ndogo. Sasa kwa namna gani mtu mwenye kipato kidogo atalipa kidogo na mwenye kipato kikubwa atalipa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kusema unashika kodi shilingi 1,000 kwenye Luku achana na hiyo, shika kutokana na matumizi ya *Unit*, badala ya Luku shika hiyo kodi kwenye *unit* mtu anazotumia. Ukifanya hivyo Mheshimiwa Waziri; moja mtu mwenye kipato kidogo atalipa stahiki yake, mwenye kipato kikubwa atalipa stahiki yake. Namba mbili, ile *issue* ya maghorofa mtu ana ghorofa ngapi? Mtu ana *apartment* ngani, hiyo hutaizingatia tena kwa ajili mtu mwenye kikubwa atatumia sana na alipa kodi kubwa na mtu mwenye kanyumba kadogo atalipa kidogo. Kwa hiyo nashauri badala ya kukatwa hiyo kodi kwenye mita ikatwe kwa *Unit* jinsi mtu anavyotumia. Huo ndio ushauri wangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kodi nyingine ambayo napenda kushauri kidogo ni tozo kwenye *line* za simu. Kengele ya kwanza naamini. Tozo kwenye *line* ya simu. Mheshimiwa Waziri, hapa tozo kwenye *line* ya simu lazima uwe clear hii kodi inakwenda kushikwa kwenye nini; kwa ajili kila kodi mpya inayoanzishwa lazima tujue base ya hiyo kodi ni kitu gani? Aidha, unakwenda kushika kodi kwenye *line* ambayo siamini kwamba umiliki wa *line* unaweza kumshika mtu kodi au unakwenda kushika kodi kwenye matumizi ya muda wa maongezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama ni kwenye matumizi muda wa maongezi ile *item* uliyoisema kwa siku itakuwa siyo muhimu. Kama unakwenda shika hii kodi kwenye muda wa maongezi kuna mtu anaweza akaongeza muda wa maongezi mara kwa wiki, mwingine akawa anamiliki *line*

tu lakini haongezi muda wa maongezi. Kwa hiyo ukisema unamshika ile kodi kila siku hutakuwa umemtendea haki. Kwa hiyo, naamini watakaoshika hii kodi *permuda* wa maongezi na pia inatakiwa um-*charge* mtu kwa jinsi anavyoongeza muda wa maongezi. Kwa hiyo, hayo ndio maoni yangu, naomba kodi hizo zifanyiwe kazi ili kodi zetu ziweze kuleta tija zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha mwisho kama muda upo, naomba nishauri kwenye ushuru wa forodha kwenye mafuta. Kweli Mheshimiwa Waziri naamini kabisa kodi hii ni kwa ajili ya kulinda viwanda vyetu lakini sasa hivi Tanzania bado tuna *deficit* ya mafuta. Kwa hiyo, kodi ni nzuri lakini ninachoona *timing* bado. Tuhimize watu wetu wazalishé mbegu za alizeti pale tutakapokuwa tuna-*produce* zaidi hapo ndio tuanze ku-*protect* thatuwezi kuanza ku-*protect* kitu ambacho hatunacho bado. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kodi hii ni nzuri na ninaiunga mkono lakini nahisi *timing* bado sasa hivi mahitaji ya nchi yetu ni karibu tani za ujazo 500,000, zaidi ya 500,000 lakini tuna *produce* 200,000 tu. Kwa hiyo, tukienda ku-*protect* sasa hivi kitu ambacho hakipo bado haiingia akilini kwa hiyo naomba tuwahimize watu wetu na tutakapokuwa tunazalisha zaidi hapo ndipo tutakapokuwa na nafasi ya kuweza kulinda viwanda vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa muda huu, naunga mkono hoja, mungu awabariki sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Felista D. Njau, jiandae Mheshimiwa Jumanne Sagini, jiandae Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said.

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa pumzi alizoweza kunipa siku ya leo lakini nami niweze kuchangia katika bajeti hii. Kwa leo, nishukuru kwa kidogo, wanasema usiposhukuru kwa kidogo hata kwa

kikubwa huwezi kushukuru. Niweze kushukuru kwa mawazo haya yaliyochukuliwa kwa sababu nimekuwa ni mdau wa barabara nimekuwa nikichangia kwenye barabara katika TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi nimejikita sana kwenye barabara. Kwa hiyo, nimeona hapa mrejesho uliokuja umekwenda kuleta suluhu kama tutakwenda ipasavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza jinsi Serikali inavyopoteza wawekezaji, nikaeleza jinsi inavyoweza kufikia kukosa pato la Taifa na pato la mtu mmoja mmoja kama hatutatengeneza miundombinu thabit ya barabara. Lakini nikaeleza ni jinsi gani tutashindwa kwenda kufikia kauli mbiu ya Tanzania ya Viwanda kama hatutatengeneza miundombinu; nikaeleza ni jinsi gani hatutafanya kilimo chenye tija kama hatutatengeneza miundombinu ya barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoongea hivi narejea kwenye hotuba ya bajeti kwenye ile para ya 39. Nimeona pale kwamba Serikali inakwenda kuomba mikopo ya bei nafuu kwenye Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeainisha pale kiasi cha dola za Kimarekani milioni 120 imeelekezwa itakwenda Dar es Salaam. Ikaelekezwa kiasi cha dola za Kimarekani milioni 300 zitakwenda mikoani kwa lengo la kukuza uchumi. Lakini pale ikaelekezwa milioni 50 dola za Marekani Serikali itakwenda kuweka pale; lakini mwisho wa siku tunapata jumla ya dola za Kimarekani milioni 470. Tukienda kubadilisha kwa fedha zetu za Kitanzania kwa *rate* ya leo ni shilingi 2,300 tunapata triliuni 1.081. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukihama twende ile para ya 88 ambapo kuna tozo ya mafuta. Serikali inaendelea kutafuta fedha mbadala ili tuweze kupata suluhu ya kero ya barabara. Kwenye tozo ya mafuta ya *petrol* na *diesel* tumesema pale kila lita moja itatozwa shilingi 100. Serikali ikadadavua ikapata 322,158,000.20, ukijumlisha unapata triliuni 1.403 fedha hizi ni nyingi sana na zote zinatakiwa

zielekee *TARURA* ndio lengo la Serikali. Na ukiangalia asilimia ya barabara zetu za vumbi ni asilimia 72.4 Nchi nzima kwenye mtandao wa *TARURA*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni nyingi naomba nishauri jambo. Kwa sababu fedha hizi ni nyingi na zikiwekezwa kweli kwenye *TARURA* zitaleta tija, ninaomba fedha hizi ziwekwe kwenye *ring-fence* ili zisitumike kwenye matumizi mengine lakini jinsi ziliviyotengwa ziente eneo husika. Namba mbili, fedha hizi jinsi Mheshimiwa Waziri alikuja hapa akadadavua vizuri aje hapa wakati wa kuhitimisha fedha hizi zianishe barabara zinazokwenda kujengwa. Lakini pia zianishwe zinakwenda kujengwa kwa kiwango kipi cha lami, cha changarawe au kiwango kipi ili tuangalie thamani ya fedha zetu zinakwenda kufanya nini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikifanya hivyo ninarejea pale ambapo Serikali iliona inakwenda kukuza fursa ya kiuchumi ndio maana fedha hizi zikaelekezwa zile dola milioni 300 zikaenda mikoani. Kuna mfano wa barabara ambazo ni kwikwi tutakuwa tunaimba mapambio hapa kila siku kama hatutekelezi wajibu wetu na kutenda kile ambacho tunachokisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo barabara za mikoani ambayo mikoa inalima, inalima mazao ya biashara, inalima mazao ya mbogamboga, kwa mfano; kama Morogoro kuna barabara ile ya Bigwa – Kisaki ile barabara ni kwikwi lakini wakulima walioko kule ni wengi na barabara ile ikijengwa inaweza kuleta tija ni kwa Mheshimiwa Babu Tale. Lakini ipo barabara ile ya Iringa ambayo inapita Lujewa, Madibila mpaka Mafinga ile barabara ni ya kibashara kule wapo wakulima, wapo watu ambao wako pale wanalima mahindi ikitengenezwa vizuri inaweza kuimarisha pato la mtu mmoja mmoja lakini kuimarisha pato letu la Taifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo barabara ya Njombe – Kibena kuelekea Lupembe mpaka Madeke kule kuna wakulima wa parachichi. Tunaachaje kutengeneza barabara hizi za kimkakati. Kama lengo letu ni kukuza fursa za kiuchumi

na kibiashara twende tukaangalie hizi barabara za kimkakati.
(Makofi)

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

TAARIFA

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumpa taarifa Mheshimiwa mzungumzaji anayezungumza hivi sasa kwamba barabara ile ya Kibena *stop* Lupembe, Madeke barabara ambayo inaunganisha mkoa na mkoa. Kweli kuna umuhimu sana wa barabara hizi kujengwa kwa kiwango cha lami na Serikali ipo hatua nzuri ya kutengeneza barabara hizi kwa kiwango cha lami.
(Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa taarifa hiyo.

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa hii kwa sababu ni kati ya wadau ambao wanalalamika juu ya barabara hizo. Niendelee, naendelea kuainisha barabara za kimkakati kwenye mkoa ule wa Kagera kuna barabara ya Mulushaka, Ukwenda, Mrongo, barabara hii inaelekea mpaka mpakani mwa Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea haya sehemu hizo tumefika sisi wanasiasa tumetembea mtaa kwa mtaa, mkoa kwa mkoa, kwa hiyo tunafahamu kero za nchi hii. Barabara hii ukifika kule mpakani kuna wakulima wa ndizi, kuna wakulima wa kahawa, barabara hii ikitengenezwa tunakwenda kukuza pato la Taifa lakini pato la mtu mmoja mmoja ambayo ndio dhamira yetu ambayo Wabunge tuko hapa.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema pia bajeti hii iainishe madaraja. Kuna madaraja ambayo ni sugu watu wanaongea huku kipindi hicho cha bajeti ya Wizara ya Ujenzi

na TAMISEMI watu wengi wanaongea juu ya madaraja, vilio kwa kina mama wajawazito wanajifungulia barabarani. Tuainishiwe na madaraja haya ili tuweze kujua fedha zetu inakwenda kutumika vipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sasa naelekeea Dar es Salaam. Katika Mkoa wangu wa Dar es Salaam, Dar es Salaam ni mkoa wa kimkakati na ni mkoa wa biashara na ni kitovu cha biashara Nchi nzima. Dar es Salaam huwezi kusikia mtu anasimama hapa anaomba viatilifu, anaomba mbolea, anaomba pembejeo. Dar es Salaam tunaomba miundombinu thabiti. Tunaomba miundombinu kwa sababu mpaka Dar es Salaam inaibuka katika Majiji yote kwamba ndio Jiji ambalo linakusanya ushuru mwingi kila siku na kimkoa inashika namba moja ni kwa sababu Dar es Salaam ndio mkoa wa biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam kuna tatizo la miundombinu, nikipita kwako kwenye mitaa ile ya llala, ninaona barabara za mitaa bado haziko sawa. Pia maji taka Dar es Salaam ni asilimia 14 tu tumeunganishwa katika mfumo wa maji taka, asilimia 86 ule mfumo wa maji taka umeingiliana na maji masafi huko huko tunakutana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la mlipuko wa magonjwa ya kipindupindu na magonjwa ya homa ya matumbo. Kila mwaka kipindupindu kinaazia Dar es Salaam, siyo kwa sababu nyngine bali ni mfumo wa maji taka ambayo siyo rafiki. Niombe wakati Waziri anakuja, aje na utaratibu mzuri kwa jinsi gani maji taka yataelekezwa baharini au sehemu nyngine kuliko ilivyo hivi sasa. Dar es Salaam mvua ikinyesha ndiyo wakati wa wananchi wa kupumua na kuanza kucheulisha vyoo vyao na yale mambo yanatapaa barabarani, kwa hiyo siyo salama sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa sababu Dar es Salaam ndio Jiji la kimkakati, wawekezaji wanapokuja kitu cha kwanza wanaangalia miundombinu, kama miundombinu siyo rafiki wawekezaji wanatukimbia. Na Dar es Salaam ndipo wawekezaji wanaanza kushukia pale,

kwa hiyo wanaangalia mandhari, pia wafanyakazi wa Dar es Salaam ni uchovu kwa sababu mvua ikinyesha inakuwa ni *jam* kunakuwa na foleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe wakati Mheshimiwa Waziri unakuja kuhitimisha, uje na mkakati wa miferiji Dar es Salaam, mifereji ambayo inasababisha barabara zetu za lami zinakatika, hakuna miundombinu thabiti ya mifereji, mvua ikinyesha mafuriko watu hawapiti mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii, ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako mzuri hasa kuzungumzia Jimbo la Ilala. Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Mwanahamis nimeambiwa ushachangia jana kwa hiyo hautachangia tena leo, Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro ajiandae. (*Kicheko*)

MHE. JUMANNE A. SAGINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mchana huu, juu ya hii bajeti ya Serikali. Nami niungane na wasemaji waliokwisha tangulia kuanza kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuweka dira iliyotafsiriwa vizuri sana na Waziri wa Fedha na Mipango, siyo kutafsiri tu na hata kuiwasilisha kwa ufundi kweli kweli. Mheshimiwa Mwigulu Nchemba umejieleza vizuri na tumekuelewa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Waziri na timu yake akiwemo Naibu Waziri Mheshimiwa Masauni, Katibu Mkuu Tutuba, Naibu Makatibu wote watatu, Ndugu Amina Shaaban, Ndugu Adolf Ndunguru na Dkt. Khatibu Kazungu na Makamishna wote wa Wizara ya Fedha. Kwa kweli mimi naomba Waheshimiwa Wabunge wote tuiunge mkono bajeti hii kwa sababu ninaiona ni bajeti iliyoandaliwa kwa usikivu wa kiwango cha juu sana. Naomba kwa muda niliopangiwa nirejee maeneo machache, yanayoonesha kwamba tunastahili kuiunga mkono bajeti hii kwa asilimi 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza usikivu wa hii tozo ya shilingi mia kwa lita ya *diesel* au *petrol* ili kuhudumia barabara zilizo chini ya *TARURA*. Wabunge wote tumeonge kuhusu hali mbaya ya barabara zetu na kwa uamuzi huu, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri mwenyewe, tutapata zaidi ya shilingi bilioni 322. Fedha hizi zikiongezwa kwenye fedha iliopo ya sasa kwa mchanganuo wa asilimia 30 kwa 40 zinazokwenda *TARURA*, ambazo ni bilioni 272.5 kutakuwa na jumla ya shilingi bilioni 594.7 kwa ajili ya kuhudumia barabara za Halmashauri na za jamii. Haya ni mapinduzi makubwa kufanya, mwaka wa kwanza wakati Serikali ya Awamu ya Sita inaingia madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini fedha hizi zikitumika vizuri, zitasaidia sana kupunguza mfumko wa bei kwa sababu wataalamu wa uchumi wanatuambia mfumko wa bei unasababiswa na kupanda kwa gharama za chakula, imekuwa ni ada chakula Mpanda kule kiko chini sana maeneo mengine kipo juu kwa sababu hatuwezi kufika kutohuna na miundombinu ni mibovu. Kwa hali hii bei ya chakula kitaifa kila mtu atawezekuimudu na itakuwa ya chini vilevile hata maisha ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge aliongea kwa uchungu hapa hali ya barabara ilivyo mbaya, wagonjwa kufia njiani, madaraja yaliyokatika hayawezi kuhudumiwa, lakini kwa fedha hii nina imani hali inaweza ikawa nzuri kwenye barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu ambalo naomba nikumbushe hapa, ni iwapo fedha hizi zitatumbukizwa kwenye mfuko wa barabara zigawanywe na *Road Funds Board*, au kutakuwa na sheria maalum iliyotengwa kwa ajili ya hizi fedha. Kwa sababu kama zitaingia mfuko wa barabara basi kuna umuhimu wa ile sheria ya mfuko wa barabara irekebishwe kuondoa ile uiano wa asilimia 30 to 70, na kama itakuwa na sheria yake mahsus, zikaenda *TARURA* bila ya vikwazo itakuwa vizuri. Kwa hiyo naomba hilo Mheshimiwa Waziri alifikirie lisije likaturudisha

kwamba sheria haijabadilishwa tutaenda kwa mgao ule wa 30 kwa 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo nalionna ni mapinduzi makubwa, Waheshimiwa Wabunge wote tumelizingumza ni malipo kwa Madiwani, maeneo mengi ilikuwa ni changamoto, mbaya kabisa ilikuwa inafedhehesha. Madiwani ndiyo watunga sera kwenye vyombo vyetu vya Serikali za Mitaa, ndiyo wafanya maamuzi, ndiyo waajiri, lakini kwa kweli Halmashauri nyingi zipo chini kimapato walikuwa wanafedheheka sana na waligeuka kuwa wanyonge, wengine Mkurugenzi anaweza kuamua akasema sina hela hawalipi kwa hiyo anaweza kuwakopa ili waendelee kuwa wanyonge. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa Serikali wa kuwalipa moja kwa moja hili nalo linamapinduzi sana, Madiwani wetu watakuwa na uwezo sasa hivi wa kusimamia Halmashauri zetu bila ya kushawishiwa kwa kupewa fedha. Jambo ambalo naishauri TAMISEMI yale malipo mengine ya vikao, tumeondoa kwenye posho zao za kila mwezi Serikali kuu inatoa, sasa tena tusisikie na siyo jambo jema kusikia Wakurugenzi hawawalipi hata posho zao zile za vikao, hili ni la TAMISEMI najuwa Waziri yuko makini na wasaidizi wake litatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze kwa uamuzi wa kuwapa hawa Maofisa wa ngazi za Tarafa, na Kata posho ya kuwawezesha kusafiri kwenda kuhudumia wananchi, nilitaka niseme kitu lakini sasa ndiyo kimetoka hicho cha shilingi laki moja. Kule kwenye ngazi ya jamii ukienda kwenye Kata kuna Maafisa Elimu Kata, zamani tukiwaita waratibu wa elimu Kata, wao wanapata posho ya shilingi laki mbili kwa mwezi, na wanapewa vyombo vya usafiri pikipiki ili waweze kuzitembelea Kata zao. Sasa Afisa mwenye Tarafa nzima anapewa shilingi laki moja, lakini siyo jambo bayaa maana ndiyo tumeanza, tuone umuhimu wa kuiboresha kwa miaka ijayo ili kuwawezesha hawa watu kufanya majukumu yao vizuri zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni suala la ulipaji wa kodi ya majengo kupitia umeme. Ninajua yapo maamuzi ya kisera yalishafanywa na Serikali zetu ziliyopita na hii ya sasa, kwamba kuna watu walishasamehewa hata kulipa kodi za majengo wakiwemo watu wazima, wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huu *unless* Wizara ije na utaratibu, sheria au kanuni zake zikae vizuri. Je, watu wenye umri mkuwa ni namna gani watakaokuwa *exempted*, vinginevyo kwa vile wana nyumba za kutumia umeme ikiwa *generalized* ina maana hata hawa ambao tuliosamehe, watalazimika kulipia kodi za majengo kupitia umeme. Kwa hiyo hili nalo tumuombe Waziri kwenye sheria au kanuni ile aliweke vizuri sana, kwa sababu wananchi wameshtuka wanadhani watabanwa kwenye eneo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ambalo nataka kulisema kama ushauri kwa Serikali, ili uchumi ukue kwa kiwango tunachotaka Serikali ikubali kuajiri watumishi hasa wa kada muhimu. Muda wangu mwangi nimefanya kwenye utumishi nimeufanya kwenye sekta za Serikali za Mitaa. Ninafahamu kuna kada muhimu sana kule ambazo zinaupungufu mkubwa wa watumishi. Moja ni *Internal Auditors*, maeneo mengi *Internal Auditors* hawapo na hawa ndio wanafanya ile *preliminary audit* kabla CAG hajaingia. Hasa kama hawa hawapo na ndio wadhibiti wa mwanzo itakuwa ni changamoto, kwenye *Local Government* hakuna Wahandisi, *Quantity Surveyors* hawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilidhani Serikali ifanye kazi ya kuchambua zile kada muhimu ambazo zikiwepo zitasaidia kusimamia uchumi tunaotaka ukue, pia tutaimarisha utoaji wa huduma bora kwenye mamlaka zetu. Kwa maoni yangu nilidhani kada hizi tatu nilizozitaja tungezipa kipaumbele cha ajira ili waweze kusaidia kusukuma mbele Serikali zetu za Mitaa na Serikali Kuu kwa wale ambao hawana ajira hizi, vinginevyo naunga mkono hoja hii na tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri akafanye kazi yake kwa mwaka ujao. Ahsanteni sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti, awali ya yote napenda kuanza kumshukuru na kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi mzuri ambao ameunesha tokea awe Rais wetu na kwa kazi nzuri sana ambayo anaendelea kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya muda mfupi Mama Samia ameonyesha uongozi mzuri uliotukuka na jamii ya Kimataifa imetambua kwamba Tanzania tuna Rais kweli kweli Rais Mama. Vilevile, napenda niweze kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Naibu Waziri wake na viongozi wengine wote wa Wizara, kwa kuweza kutuletea bajeti ya kisayansi kwenye Bunge letu hili. Bajeti ambao kwa kweli imegusa maeneo mbalimbali ya vipaumbele ya nchi, imegusa makundi mbalimbali kwa kweli mimi nina washukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili bajeti hii iweze kutekelezeka, ni wazi kwamba lazima tupanue wigo wa kodi na ni lazima maeneo yote nyeti ya makusanyo ya fedha yaweze kuboreshwa ili kodi iweze kukusanywa. Kwa minajili hiyo Jimbo la Ngara ni miongoni mwa Majimbo ambayo yamekaa kimkakati, Jimbo la Ngara linapakana na nchi mbili za Rwanda na Burundi na kutoka Ngara kwenda Goma - *DRC* ni kilomita 355 na kutoka Ngara kwenda Juba ni kilomita 1,094. Hivyo, tunao mwingiliano mkubwa wa maeneo yote haya na biashara ya mpakani kwenye Jimbo la Ngara imeshamiri kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya forodha vinavyotakiwa kufanya kazi kwenye Jimbo la Ngara ni vituo vinne lakini mpaka sasa ni viwili tu vianavyofanya kazi yaani kile cha Kabanga na kile cha Rusumo. Kulikuwa na kituo cha forodha cha Mgoma ambacho kilanza kufanya kazi miaka

ya nyuma lakini baadae kituo hiki kilifungwa na *TRA* upande wa Tanzania waliondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wenzetu wa upande wa Burundi wamejenga jengo kubwa sana la kisasa, wameweka taasisi zao za mamlaka wa mapato pamoja na Uhaniaji kwa upande wa Burundi. Upande wa Tanzania, kuna mtaalamu alitoka *TRA* Makao Makuu wamekuwa wakienda pale Mgoma, kwenda kutembea, kwenda kufanya *assessment* na ripoti wanazoafanyia *assessment* hazijawahi kutoka na kinachoendelea hatujui ni kitu gani. Nimuombe Mheshimiwa Waziri atoe maelekezo *TRA*, taarfia iliyoenda kuchukuwa pale itoke na kituo hiki kiweze kunya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kamati ya kushughulikia masuala ya magendo ya Mkoa inaitwa '*fast*', kazi yake ni kwenda kukamata wafanya biashara ambao kwa kweli ule mpaka ni lazima wafanyabiashara wautumie kwa magendo, kwa maana ni ngumu mfanya biashara kusafiri zaidi ya kilomita 50, kwenda kutafuta huduma za forodha, wakati anaweza kupitisha kwenye njia za panya mzigo wake wa kilo 10 kilo 20 na akaweza kuupitisha. Hivyo badala ya kuhangaisha hawa wafanyabiashara, ninaomba sana Wizara ya Fedha na Mipango, iweze kutoa maelekezo kama zamani huduma ya forodha ilikuwepo, na kulikuwa na majengo ya kawaida yanayotumika na upande wa pili wa Burundi wapo tayari kwa ajili ya biashara mapakani sisi tunakwama wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-conclude, kwa kweli tunaombwa uwatendee haki wananchi wa Ngara na wafanyabiashara wote kwa kuruhusu kituo hiki cha forodha cha Mgoma, kiweze kuanza kutoa huduma za forodha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwengine, tuna kituo kingine cha forodha cha Murusagamba, kilijengwa mwaka 1990, baadae kikaungua, mwaka 2016 kikajengwa upya baada ya kuwa kimeungua, baada ya hapo *TRA* Mkoa na *TRA* Ngara wakaomba kupewa namba maalum ya

utambulisho wa kituo hicho yaani *Identification Code Number*. Tokea mwaka 2016 Mheshimiwa Waziri hiyo namba hatujapewa kwenye kituo chetu cha forodha cha Murusagamba. Kamishna wa *TRA* ameishikilia hiyo namba, nakuomba Mheshimiwa Waziri hiyo *identification number* ya kituo chetu cha forodha cha Murusagamba iweze kuletwala ili kituo chetu kianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na *modem*, ile *modem* ilichukuliwa kutoka kituo chetu cha forodha cha Murusagamba ikapelekwa Kerwa, ikatumika Kerwa na baadae ikachukuliwa ikapotelea hewani, mpaka sasa hivi *modem* yetu Mheshimiwa Waziri ya kituo cha forodha cha Murusagamba hatujui imepotelea wapi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, *modem* yetu irejeshwe kwenye kituo chetu cha forodha cha Murusagamba ili kituo hiki kiweze kuwa *automated*, kianze kusoma na wafanyabiashara waache kupata taabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfanyabiashara anapokwenda na gari lake la mzigo anafika Murusagamba analipaki pale, inabidi asafiri umbali wa kilomita 123 *one way*, kwenda kupeleka nyaraka zake zipigwe muhuri kwenye kituo cha forodha cha Kabanga na baadae arudi tena asafiri kilomita 123 jumla kilomita 246 kutafuta huduma ya forodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwamishwa na vitu viwili ambavyo ni *identification number* na hiyo *modem*, naomba utoe maelekezo hivi vitu viletwe ili kituo chetu cha Murusagamba kiweze kutoa huduma kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Ngara, kwa ajili ya wafanyabiashara na wakati huo huo kiweze kusaidia kukusanya mapato ya Serikali ambayo yanahitajika ili bajeti hii ulioileta Mheshimiwa Waziri iweze kutekelezeka katika kipindi chote hichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niongelee eneo la urasimu liliokuwa likiwakumba wadau wa maendeleo hasa *NGO*. Kwenye ukurasa wa 29 wa hotuba ya bajeti Mheshimiwa Waziri ameonyesha bayana kwamba kumekuwa na ukiritimba kwa wadau wa maendeleo

wanapokuwa wanaleta fedha zao kwaajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo wanakutana na figisu figisu kule Wizara ya Fedha na kulikuwa na sheria ambako inataka msaada unapokuja ndani ya nchi *on entry* ule msaada uweze kukatwa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka dunia ilikuwa inatucheka, kuna haja gani ya kukata kodi kwenye msaada unapoingia moja kwa moja pale *BOT* wakati msaada huo huo unaendelea kuukata kodi nyengine kama vile *PAYE withholding tax* na kodi nyengine baada ya msaada ule unapoingia kwenye matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulimwengu mzima ulikuwa unatushangaa Tanzania, yupo mfadhili mmoja kwenye bajeti yake anatenga zaidi ya dola milioni 500 kuzisaidia nchi zinazoendela kama Tanzania, sisi na figisu figisu zetu tunaendelea nazo Kenya mpaka wakaongezewa fedha zetu zaidi ya dola milioni 200 wakapelekewa sisi tunaendeleza figisu figisu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri umeweka vizuri sana tunaomba futilia mbali hiyo sheria ambayo inasema tutoze kodi moja kwa moja *on entry* wakati fedha hizo zinaongeza wigo wa kodi kwenye Taifa letu. Nakuomba Mheshimiwa Waziri wala usipate kigugumizi, futilia mbali hizi sheria, watu wanatushangaa ule ni msaada! Mataifa ya nje yanatenga fedha zao kuja kutusaidi nchi zinazoendelea, tunakwenda kukata kodi ya moja kwa moja, wakati tunao uwezo wa kukata kodi hivyo hivyo tukaipata baada ya fedha hiyo kuingia kwenye matumizi. Kwa kweli hapa umeitendea haki nchi na Mheshimiwa Rais tunampongeza kwenye eneo hili, nenda futilia mbali hiyo sheria inayotaka tukate kodi kwa sababu imekimbiza wadau wetu wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalonapenda kuliongelea, ni mradi wa kielelezo wa Kabanga nikel ambaao umeoneshwa ukurasa wa 16 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba yangu alipozaliwa alikuta kuna kitu kinaitwa mradi wa Kabanga Nikel, akakua akamuoa Mama yangu wakanizaa na mimi, nami nimezaliwa nimekuta kuna mradi wa huu wa Kabanga nikel, mimi pia nimekua nimeoa na nimepata mtoto wa kwanza anaitwa Ndairagije nae amekuta kuna mradi wa Kabanga Nikel. Nimekaa nimepata mtoto mwingine anaitwa Irakoze naye amekuta kuna mradi wa Kabanga Nikel. Kwa upande wa Marais, amekuja Rais wa kwanza, wa Pili, wa Tat, wa Nne, wa Tano na sasa hivi tunae Rais wa Sita naye amekuta mradi huu wa Kabanga Nikel mchakato unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa kweli Kabanga Nikel wawezeshwe umeme upelekwe, leseni ya kuchimba haya madini itoke ili uwekezaji huu sasa Mama Samia anyanyue ngoma. Hii ngoma inanyanyuka na Mama Samia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umeisha lakini ninaomba sana mradi huu hawa watu wapewe leseni ili uwekezaji uweze kuanza. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge muda wetu wa mchana umekwisha. Mheshimiwa Abubakari Asenga Mbunge wa Kilombero anaomba kuwatambulisha wageni wake Ndugu Lameck Fumbuka na Ndugu Joyce Sendama amba wanatoka Geneva Uswiss nao ni watalaam, Meneja wa Solar Africa, wamekuja Tanzania kwenye uwekezaji. Karibuni mambo sasa ni mazuri.

Mheshimiwa Gulamali ambaye ni Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga katika Bunge anaomba kuwakumbusha wapenzi na washabiki wa Klabu ya Yanga kuwa leo saa jioni mnaombwa wote kuhudhuria kikao maalum cha mabadiliko ya Katiba ya Klabu ya Yanga kuelekea kuiga Katiba za Klabu zingine ambazo zilihafanya ili na wao waweze kufikia viwango vya Kimataifa. Kwa hiyo, ninaomba wote mfike na

Mzee Mkuchika usichelewe kuja unaombwa uwahi saa mbili jioni katika hoteli ya Morena. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, jioni wachangiaji wetu tutaanza na Mheshimiwa Mohamed Monni, Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kusitisha shughuli za Bunge mpaka jioni Saa Kumi na Moja leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11:00 Jioni Bunge Lillrudia)

MWENYEKITI: Tukae. Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Ahsante. Tulishataja majina ya Wabunge wa jioni. Tunaanza na Mheshimiwa Mohamed Monni, ajiandae Robert Maboto Chacha, Bupe Mwakang'ata na Conchester Rwamlaza.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti hii muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingu wa rehema ambaye mara zote amekuwa akitupa afya njema na uhai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia kidogo sana. Lakini kwanza kabisa nishukuru Wizara na kumshukuru Waziri kwa namna ambavyo mapendelekezo yetu sisi Wabunge yamezingatiwa. Kwa hakika kila Mbunge huku nyuma amesema mambo mengi na mengi yameonekana kwenye bajeti hii. Kwa hiyo namshukuru sana lakini pia nampongeza sana ye ye mwenyewe Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wake wote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati mkuu, mpango mkuu kwenye bajeti hii unaeleza juu ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu. Hili ni jambo kubwa sana na mimi nataka nichangie ni namna gani sasa tunaweza tukafika huko ambako ndiko ambapo mkakati mkuu wa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote wengi wetu tuna Majimbo huko na tunafahamu ili tuweze kufikia mkakati huu lazima tuwe na miundombinu bora na imara. Katika hilo kwanza nimshukuru sana sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kutuwezesha, kwa kuiwezesha *TARURA* kwa kutoa milioni 500,000,000 kila jimbo. Kwa hakika ametusaidia sana sana kuhakikisha baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa hayapitiki tunaweza tukapambana nayo ili walau yaweze kupitika kwa urahisi zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo yapo mambo ambayo nataka nipendekeze. Nafahamu kila Jimbo linahitaji fedha lakini nafahamu kuna maeneo ambayo kiukweli hayapitiki. Moja ya maeneo hayani majimbo yetu sisi ya vijiji. Sisemi kwamba watu wa llala wasipewe, watu wa Kinondoni wasipewe. Hapana. Nafikiria kwamba tumepewa milioni...

MWENYEKITI: Toa mchango wako huna haja ya kutaja Majimbo mengine.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetaja llala kwa sababu wewe ndiyo Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Toa mchango wako ndugu au utakaa sasa hivi hapa. (*Kicheko*)

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni moja, nafikiria kwamba ili tuweze kufikia malengo ya bajeti hii tunafikiria ni lazima tufungue maeneo yote ili yaweze kupitika kwa urahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Kanda ya Kati, kwa mfano jimbo langu ni wazalishaji wakuu wa alizeti, na sasa hivi tunaenda kufungua viwanda nya alizeti, kama tulivyosema, kwamba mkakati namba moja ni kuhakikisha tunaweka uchumi shindani na viwanda kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu. Katika mazingira hayo yapo maeneo ambayo wamelima alizeti lakini hawana uwezo wa kuzitoa kule kuingiza sokoni. Au, kwa kufanya hivyo, unayatoa kwa gharama kubwa kweli kweli. Maana yake sasa mkulima anazalisha, anatumia fedha nyangi lakini tija yake inakuwa ni ndogo kwa sababu hana uwezo wa kuyatoa au akiyatoa, anayatoa kwa gharama kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo mimi naomba pale *TARURA* tumeongezewa fedha. Ninakushukuru sana Waziri wa Fedha namna ambavyo umefikiria na umezingatia namna ambavyo tuliongea huku nyuma. Sasa fedha zile zikipatikana naomba basi mgao ule ulenge mahitaji. Tuangalie ni wapi sasa ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie mimi nimeshindwa. Tulielekezwa zile fedha tulizopewa walau tujenga barabara au tujenge kwa kiwango cha changarawe. Lakini ni ukweli kwamba kuna maeneo ambayo hata watoto hawawezi kwenda shule wakati wa mvua. Watakushangaa sana utato amillioni 500,000,000 zile ukajenge kilometra moja ya lami wakati kuna maeneo ambayo hawapo. Mvua zikianza lazima mvua zishe ndiyo watoto waende shule. Katika kuzingatia hilo, mimi nimuombe sana Waziri wa Fedha, rafiki yangu wa muda mrefu, rafiki yangu wa muda wote. Naomba mnapotoa hizi fedha basi hebu jaribuni kuangalia ni namna gani tunaweza tukaifungua hii

nchi kila eneo walau lifaidi au kila eneo walau liweze kupidika kwa urahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, mimi nakufahamu ndugu yangu Mwigulu Nchemba, ni mtu mchapakazi, mwerevu, anaweza. Sasa tumeongeza fedha kwa ajili ya *TARURA* naomba basi zitoke, maana tunaweza tukazongeza lakini kuziongeza na kuzikusanya ni jambo lingine lakini kuzitoa ziende *TARURA* pia ni jambo lingine. Nafahamu hilo lipo ndani ya uwezo wako Mheshimiwa Waziri. Sisi ambao tuna Majimbo ambayo yapo vijiji tuna changamoto kubwa sana. Naomba sana, fedha hizo zikikusanywa zipekwe huko ili walau zitusaidie kufungua vijiji na vitongoji vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwangu peke yangu kwenye zile kilometa nyingi zinazotajwa nina kilometa zaidi ya 1,000 na zaidi za *TARURA*, lakini ambazo zinafanyiwa ukarabati au zinaweza kupidika ni asilimia 17 tu. Tafsiri yake ni kwamba maeneo mengi hayapitiki wala hayana uwezo, hata kama una biashara yako huwezi kufanya. Mimi nilitaka kuchangia hilo kuhusu barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba niongee kidodogo kuhusu kilimo. Waziri mwenyewe anakiri kwamba asilimia 65 ya Watanzania wanategemea kilimo, lakini ni ukweli kwamba hakuna namna ambavyo nchi yetu inaweza kwenda mbele bila kuwekeza kwenye kilimo ambacho ndicho kina watu wengi na hakuna *formula* zaidi ya hiyo. Ukweli ni kwamba ukitaka ku-solve quadratic equation lazima utumie *quadratic formula*, hakuna namna nyiningine.

Nimejaribu kuangalia na kufanya tafiti kote duniani, ukweli ni kwamba lazima uwekeze kwenye nguvu kubwa, lazima uwekeze kwenye shughuli kubwa ya kijamii inayofanyika. Watanzania wengi ni wakulima lakini sisi tunawekeza kidogo mno. Bajeti yetu walau tungeisogeza ikafika asilimia 10 ya bajeti tungekuwa tunaamini kwamba sasa tunaenda kusaidia watu walio wengi ili waweze kuinuka kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hilo mimi Jimbo langu asilimia 95 ni wakulima, na ukitaka kumuuliza mtu anawezaje kupata fedha lazima asubiri wakati wa mavuno ndiyo anaweza kupata fedha na akatunza kwa ajili ya kuhudumia mwaka mzima. Sasa, katika mazingira hayo kuna changamoto kubwa sana kwenye. Moja ya changamoto kubwa sana ni masoko. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri kaeleza vizuri kwenye bajeti hii. Ameeleza namna gani ambavyo anaweza ku-deal na hilo suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine kubwa, na mimi nafahamu ndugu zangu wenye majimbo hapa idadi kubwa sasa hivi ya watu vijijini ni vijana. Vijana ni wengi sana huko vijijini. Mimi nikienda vijijini nikiitisha mukutano nakutana na vijana wengi sana. Wapo vijana wenye *degree* mbili (*Masters*) wapo vijana wana *degree* moja, wapo vijana ambao hawana elimu, wako vijijini wamezubaa kule hawana cha kufanya. Tufanye nini sasa, kwa sababu tukifkiria kwamba waende kujajiri, wanajajiri vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kama alivyosema kwenye bajeti yake ninamuomba sana Waziri hili jambo alifuatilie, tuangalie namna gani tunaweza kuwekeza mitaji kwenye hawa vijana. *Otherwise* tunaweza kutengenza mazingira magumu sana kwao na kwetu sisi ambao mara zote wenyewe ndiyo wanatusaidia kutupigia kura. Nilitamani sana niyaseme hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nilitaka kuongea kidogo kuhusu elimu. Niliwahi kusema huku nyuma, kuna changamoto kubwa sana kwenye Halmashauri hizi ambazo ni changa, Halmashauri ndogo kama ya kwangu mimi ambayo ukikusanya fedha mapato yote kwa mwaka ni bilioni 1.2 na ukiangalia uwezo wa ujenzi wa madarasa ni mdogo sana. Bado narudi kwenye hoja ile ile kwamba ni lazima tuangalie ni wapi. Wakati mwingine unajiuliza maswali makubwa sana kwamba kule Wizara ya Elimu wametoa fedha kwa ajili ya maboma lakini wametoa *flat rate*. Yaani mtu ambaye anakusanya bilioni 100 unampa *flat rate* na mtu anayekusanya bilioni 1.2 kwa mwaka. Hii haiwezi kuwa sawa

na hatuwezi kuwa tunalenga sasa kuendeleza hizi halmashauri changa au watu walioko. Mimi nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, hili ulizingatie vizuri. Mimi naamini wewe unaweza na haya mambo unaweza ukayaweka vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Robert Maboto Chacha jiandae Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata na Mheshimiwa Conchester Rwamlaza.

MHE. ROBERT C. MABOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti yetu ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niwashukuru wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini kwa kuendelea kuniamini ili mimi niweze kuwatumikia lakini pia ninaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa inayofanya, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia Serikali kwa sababu imetuwezesha sisi Wabunge kwenye majimbo yetu kwa kutupatia zaidi ya shilingi 500,000,000 kwa ajili ya kushughulika na barabara ambazo zimekuwa kero kubwa sana kwa Watanzania.

Pia naipongeza Serikali kwa sababu ilisikiliza kilio cha Wabunge na mawazo yao kwa muda mrefu ambayo tumekuwa tukiyazungumza hapa. Kwa mfano mimi Jimbo langu la Bunda Mjini, takribani muda mrefu uliopita nyuma barabara zangu za mitaa zilikuwa haziwezi kupidika kwa namna yoyote ile hata kama ungeenda na trekta zilikuwa haziwezi kupidika. Lakini kwa sababu Serikali ya Awamu ya Sita ni Serikali sikuvi imetoa fedha na sasa barabara zimeanza kupidika hata kama sio zote lakini mwanzo umeshaanza kuonesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita imetufanyia mambo makubwa pale Bunda Mjini. Kwa muda mfupi huu tumeshapata taa za barabaranı pale mjini, tumeshapata fedha za kujenga shule za sekondari zaidi ya sita, na kwa muda mfupi tumeshazifungua lakini pia na shule za msingi ziko zinaendelea kujengwa. Kwa hiyo kwa bajeti hii ambayo imewasilishwa na Wizara ya Fedha Mheshimiwa Mwigulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo muhimu sana ambalo mimi ninaliona hapa ni kuhakikisha kwamba Wizara ya Fedha inasimama vizuri katika kuhakikisha kwamba makusanyo yale yanayopatikana yanatumika vizuri kwa ajili ya shughuli za maendeleo za wananchi. Wananchi wa nchi yetu tuzipowazo esha suala la kulipa kodi wakalijua, kwamba kila mfanyakibashara anayefanya biashara kulipa kodi ni wajibu wake kuna siku watakuja kudai maendeleo pasipo wao kutaka kutoa kodi. Kwa hiyo hili nilipenda niishauri Wizara ya Fedha ikasimame nalo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, kwa sababu ya makusanyo yetu tunayoyakusanya hayatoshelezi mahitaji yetu, bajeti yetu kwa mwaka ni triliuni 36 lakini makusanyo yetu yako chini. Kwa maana hiyo, fedha hii tunayoikusanya kidogo ni vizuri Wizara ya Fedha ikazilinda vizuri fedha hizi ziweze kutumika kwa shughuli mahsus. Wasipofanya hivyo, fedha tunayopata ni kidogo na matumizi yakaenda nje na utaratibu unaotakiwa, kile tunachokilenga kwenye shughuli za maendeleo hatutakifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wabunge tumesema hapa tukaiomba Wizara ya Fedha kutusaidia fedha kwenye TARURA na wametupa fedha. Lakini kama watu hawatalipa kodi fedha hizo pia tunaweza tukazungumza hapa kuanzia asubuhi mpaka jioni na fedha zisipatikane. Kwa hiyo muhimu ni kuwajenga wananchi wetu kwenye maeneo yetu ili wafahamu kwamba kulipa kodi ni sehemu ya maisha yao ni sehemu ya biashara zao. Wakilipa kodi wanarudi kuidai Serikali maendeleo. Kama hawatalipa kodi kuidai Serikali maendeleo haitawezekana. Lakini pia hatuwezi kupata

maendeleo kwenye nchi yetu tukifikiri tu kwamba tunaweza tukapewa fedha za misaada halafu zikatuletea maendeleo kwenye nchi yetu. Hiki kitu hakitawezekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuishauri Wizara ya Fedha; Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA* inafanya kazi nzuri lakini suala kubwa ambalo mimi ningewaomba wajitahidi kutoa elimu kwa wafanyabiashara. Waweke mazingira ya kodi wazi, kila yule anayetaka kulipa kodi ajue uwezo wake wa kulipa kodi na kodi anayotakiwa kulipa ni ipi. Wakishafanya hivyo, watu walio wengi wataenda kulipa kodi wao wenyewe kwa hiari yao. Lakini na wao wananchi wakishalipa kodi kwenye Serikali wanaidai Serikali maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hilo ni muhimu sana ambalo Wizara ya Fedha inapaswa kulishika vizuri ilisimamie vizuri na kwa sababu fedha yetu haitoshi shughuli zetu za maendeleo kwa mwaka, kidogo tunachokipata tuweze kukitumia vizuri. Mimi nimeshangaa kuja kuona kwamba wapo watu baadhi wanaweza kwenda kwenye bomba la mafuta la Serikali wakaenda wakachimbua kwenye bomba la mafuta ya Serikali halafu wao wakapeleka yale mafuta kwenye maeneo yao wakaenda kuuza, raia wa nchi hii. Kama tunataka maendeleo kwenye nchi hii ni lazima sisi wenyewe Watanzania tuwe wazalendo kwa mali zetu sisi wenyewe. Wale watu wanaofanya hayo kwa kuhujumu miundombinu ya Serikali, wanatuambia sisi Wabunge tunachokizungumza hapa au kile ambacho Serikali inakipanga hakitafanikiwa kwa sababu wao wanakihujumu. Kwa hiyo, lazima Serikali isimame kidete kwenye jambo hili ili kwamba wale watu wanaofanya mchezo ule wauache mara moja kwa sababu sio jambo zuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mtazamo wa nchi kwa sasa wana mpango mkubwa wa kufanya ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Uganda kuja Tanzania ambalo wao leo wakiona watu wa Dar-es-Salaam au watu walioko bandarini wanafanya vitu vyaa namna hiyo, kuna watu

watajifunza vitu viovu kupitia kwao, halafu matokeo yake kile tunachokikusudia tusikifikie kwa makusudi ya watu wachache, kundi la watu wachache wasiozidi 10 au 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mtazamo wa nchi kwa sasa wana mpango mkubwa wa kufanya ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Uganda kuja Tanzania ambalo wao leo wakiona watu wa Dar-es-Salaam au watu walioko bandarini wanafanya vitu vya namna hiyo, kuna watu watajifunza vitu viovu kupitia kwao, halafu matokeo yake kile tunachokikusudia tusikifikie kwa makusudi ya watu wachache, kundi la watu wachache wasiozidi 10 au 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara ya Fedha, leo tunazungumza na Mheshimiwa Waziri hapa, tunaipongeza sana bajeti yake ni nzuri na imekidhi vigezo vizuri vya wananchi wetu, lakini itakuwa nzuri pale yale yote tunayoyatarajia yafanyike kwa wananchi yatakapofanyika. Nje na hapo tutakaporudi mwaka kesho au kwa muhula mwingine tutaanza kumsema Waziri vibaya, lakini fedha ikipatikana bajeti itakuwa nzuri na shughuli za maendeleo za wananchi zitakwenda vizuri na kile tunachokusudia kitafikiwa. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri kudhibiti suala hilo kupitia Serikali ili kwamba, yale mapato yetu madogo tunayoyakusanya yaweze kutusaidia kwenye shughuli zetu za maendeleo. Nje na hapo Mheshimiwa Waziri, leo tutampongeza na kesho tutarudi kuja kulaumu kwake tena kwamba, mbona hakufanya yale ambayo tulikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda nichangie hayo mambo machache katika bajeti hii ili niweze kusema hilo nililoliona. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Nimeshamwita Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, ajiandae Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, atafuata Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omari.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti hii muhimu. Kwanza kabisa

namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya Wabunge wote tulioipo humu ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu kwa kazi nzuri. Bajeti aliyotuletea kwa kweli, imekidhi viwango, imegusa sehemu zote na matatizo yote ya Watanzania kwa kweli, imeweza kugusa kila nyanja. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Waziri na Naibu wake kaka yangu Mheshimiwa Masauni kwa kazi nzuri na bajeti nzuri walijotuletea. Kwa kweli, bajeti imekidhi viwango. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza kwa suala zima la kuwajali bodaboda. Bodaboda kwa kweli ilikuwa ni tatizo kubwa sana, tulikuwa na vijana wetu ambao walikuwa wanavuta bangi, wanajiunga kwenye makundi mbalimbali ambayo sio ya kimaadili, lakini sasa hivi bodaboda wameweza kujajiri wenyewe. Shida yao ilikuwa ni changamoto hizo za barabarani, za kukamatwa hovyohovsky bila mpangilio. Tunashukuru sana Serikali imeweza kuwajali kwa kuwapunguzia *fine* kutoka shilingi 30,000 mpaka shilingi 10,000. Hata hivyo, Serikali isiishie hapo tu iendelee kuwalinda hawa bodaboda maana unaweza ukampunguzia bodaboda kwamba, asilipe shilingi 30,000 lakini akaweza kukamatwa mara tano, mara tatu, ikarudi palepale shilingi 30,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali ikimkamata bodaboda kosa moja, basi kosa hilo liendelee mpaka siku nzima iishe. Sio leo asubuhi unamkamata, mchana unamkamata, jioni unamkamata, kwa hiyo, ile shilingi 30,000 itakuwa tena imerudi palepale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeweza kuishauri Serikali kwamba, hawa bodaboda wangeanzishiwa mafunzo. Bodaboda wengi wanajifunza wenyewe huko mtaani,

anajifunza siku tatu, baada ya hapo anaingia barabarani. Hajajifunza kokote, hajajua sheria anaingia barabarani. Naiomba Serikali sasa kwa sababu imewatambua bodaboda na imewapunguzia adhabu basi iwaandalie tena na mafunzo kwa ajili ya kuzijua sheria za barabarani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze tena Serikali kwa kuwakumbuka Madiwani. Madiwani kwa kweli wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana huko waliko, lakini naishukuru Serikali imeweza kuwakumbuka. Naiomba Serikali pamoja na kwamba, imewakumbuka kuwalipa posho zao kuititia Serikali Kuu, pia iwakumbuke kwa kuwaongezea posho, lakini pia kwa kuwakopesha angalau hata usafiri wa kuwafikia Watanzania popote pale walipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali kwa kuwakumbuka watumishi kuwapandisha madaraja. Hiki kilikuwa ni kilio kikubwa sana kwa watumishi Watanzania, hasa Walimu. Walimu walikuwa kwa muda mrefu hawajapandishwa madaraja na wale waliopandishwa madaraja walikuwa hawajalipwa na wala walikuwa hawapatiwi hata semina zozote za kuongezewa ujuzi, lakini kwa utaratibu huu wa Serikali kuwapandisha madaraja kwa kweli, wamefuta kilio cha Watanzania, wamewaongezea tija Walimu watakwendwa klufanya kazi vizuri na watumishi wote kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia Serikali kwa kutenga bajeti ya maji. Kwa kweli bajeti hii imekwenda kukidhi matatizo ya wananchi, kwa sababu ukimkumbuka mama kumtua ndoo kichwani, basi unakuwa umelikumbuka Taifa lote kwa ujumla, kwa sababu, hakuna kama mama. Sisi wanawake tulikuwa tunapata tabu sana wakati wa kutafuta maji, tulikuwa tunakwenda mwendo mrefu sana, ndoa zetu zilikuwa ziko hatarini, ndoa zetu zilikuwa zinavunjika, lakini bajeti hii inakwenda kutibu ugonjwa huu. Tunaishukuru sana Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, sasa niingie kwenye hoja zangu za msingi. Nilihudhuria semina

moja ya takwimu, Mkoa wa Rukwa ulatione kwa kwamba, ndio wa kwanza kwa umaskini. Nilijiuliza kwamba, Mkoa wa Rukwa unakuwaje maskini wakati sisi Mkoa wa Rukwa tuunaweza kulisha hata Tanzania nzima kwa kilimo tunacholima Wanarukwa, lakini inakuwaje tunaambibiwa sisi ndio wa kwanza kwa umaskini? Nikajiuliza ni kwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata jibu kwamba, ni kwa sababu ya miundombinu hafifu, barabara zetu hazijakaa vizuri, hasa barabara inayotoka Mkoa wa Songwe, Tunduma kuelekea Sumbawanga Mjini. Barabara ile imejengwa kwa kiwango cha lami vizuri kabisa, lakini tatizo la barabara ile ni matuta. Barabara ile ina kilometra 300, lakini matuta makubwa sana; matuta ni takribani 270, matuta hayo yametuletea matatizo makubwa sana hasa kwa wanaume wengi wanaoendesha magari Mkoa wa Rukwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipita mara tatu ile barabara kiuno chako kinakosa ushirikiano. Ukiwapima wanaume wanaoendesha magari Mkoa wa Rukwa na hasa wale wanaosafiri mwendo mrefu, mabasi na magari madogo, ukiwapima viuno havina ushirikiano kabisa. Tunaomba sana Serikali katika bajeti hii angalau itupunguzie yale matuta, matuta ni makubwa sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi wanawake tunaposafiri ukiwa mjamzito, ujauzito huwezi kufika Mbeya, unaharibika ndani ya gari. Tunaomba barabara hii ipunguzwe matuta yale, matuta yamekuwa ni mengi sana, yamezidi hata kilometra za barabara. Kilometra ni 300 matuta 270 na matuta ni makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Mkoa wa Rukwa wanasema ni maskini, lakini sisi tuna bandari, bandari ziko tatu; tuna Maziwa mawili, kuna Ziwa Tanganyika halafu na Ziwa Rukwa. Ziwa Tanganyika tuna bandari tatu, bandari hizo hazijaanza kufanya kazi mpaka sasa, naomba katika bajeti hii bandari zile zikifunguliwa tutapata usafiri wa kuvuka kwenda nchi za nje kama Kongo, Zambia, tutasafirisha mazao yetu ambayo yanakosa soko. Kwa mfano mahindi, pale

Kongo mahindi wanahitaji sana, lakini tukiwa na bandari inafanya kazi, basi tutaweza kupata soko ambalo linaweza kukidhi mahitaji ya Wanarukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni uwanja wa ndege. Uwanja wa ndege wa Mkao wa Rukwa umezungumziwa muda mrefu, lakini naiomba Serikali kwenye bajeti hii basi angalau iikumbuke mikoa hii ambayo inaitwa maskini iikumbuke kwa kujenga miundombinu kama uwanja wa ndege, kufungua hizo barabara, nadhani na sisi tutawafikia wenzetu ambao wamefikia kiwango cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante.

Sasa namwita Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, wajiandae Mheshimiwa Zulfa, Mheshimiwa Jonas Mbunda na Mheshimiwa Ahmed Ali Salum.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo katika hoja iliyio mbele yetu. Hoja ya Bajeti Kuu, Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ni tafsiri ya pesa na mipango yetu. Tumepanga mipango sasa tunatafsiri mipango yetu katika pesa. Ili tuweze kusema kwamba, hii bajeti ni nzuri, tutaangalia pale itakapowagusa watu katika kuangalia matokeo yao. Siwezi kusema bajeti ni mbaya, nitakachosema ni kwamba, hii bajeti nitaweza kuona uzuri wake pale ambapo watu watakuwa wanaguswa katika makundi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mchango wangu nitauelekeza katika ustawi wa wazee kupitia bajeti hii. Bajeti inaenda kijinsia. Kwa hiyo, tunaangalia makundi mbalimbali ambayo yameguswa na bajeti vizuri; ukitazama wanawake, ukitazama vijana, wameguswa, lakini nimekuwa na mashaka

kuhusu bajeti hii inavyowatendea wazee wa Tanzania.
(Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, Serikali hii haijafanya vizuri sana katika ustawi wa wazee katika nchi yetu. Nasema hivyo kwa sababu gani? Kwanza, Serikali hii ilitengeneza Sera ya Wazee tangu mwaka 2003. Sasa ni miaka 18 hakuna sheria yoyote ambayo imetengenezwa ili kulinda sera hii ili wazee waweze kupata huduma zao kama sera inavyosema. Ukiisoma ile sera ina mambo kama 15 ambayo yanawagusa wazee ambayo ni huduma ya afya, matunzo kwa wazee, ushirikishwaji, uzalishaji mali, hifadhi ya jamii, mahitaji ya msingi, elimu na mambo mengine yako kama 15 ambayo yamegusa sera ya wazee. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaangalia machache, kwanza nianze na huduma ya afya. Wazee wetu hawapati huduma ya afya vizuri katika nchi yetu. Katika bajeti nitajaribu kuonesha hapa kitu kilichosemwa na TAMISEMI kuhusu namna wazee wanavyohudumiwa, lakini ukitazama kwenye Bajeti Kuu n ahata kwenye bajeti ya Wizara ya Afya, hakuna mahali ambapo wametuonesha kwamba, wazee wanaweza kuingizwa katika bajeti hii ili tuweze kuangalia yaliyotajwa katika sera yao kama yanaweza kutimizwa, ili wao nao kama watu ambao wametumikia Taifa hili, kama watu ambao wamefanya uzalishaji, je, hii bajeti inawagusa ili waweze kustawi? Maana Serikali yoyote halwezi kukwepa kuangalia ustawi wa watu wake, ni kitu cha msingi. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye afya haitatekelezwa vizuri kwa sababu wazee walio vijijini hawaguswi na utaratibu mzuri wa kutibiwa kwa sababu, wao wanashindwa kutambulika kama wana miaka sitini na kuendelea. Kwa hiyo, kwao inawapa shida katika kupata matibabu na hata matibabu yanayotolewa, kwa mfano, halmashauri inawapa vitambulisho, ikiwapa vitambulisho yaani mimi niiteje, sijui niite *concession* au sijui niite nini? Labda niite ni *exemption*, inakuwa kama ni *exemption* kwa sababu hakuna sheria yoyote ambayo inamlazimisha mpeleka huduma na mtoa huduma kuhakikisha kwamba, anamsaidia

mzee, hakuna kitu ambacho kinam-*bound* mtu kwamba, mimi nitatoa huduma kwa mzee kwa sababu kuna sheria fulani inanilazimisha kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwa matunzo ya wazee. Wazee hawatunzwi vizuri katika nchi hii. Nakumbuka kipindi fulani Mheshimiwa, nani anakaa kule? Aliwahi kuchangia akasema itungwe sheria ya kulinda wazee, kama ambavyo wanawake wanatungiwa sheria, watoto wanatungiwa sheria, tunatungiwa sheria sisi wazazi kuwasomesha watoto na kuwatunza, ni kwa nini hakuna sheria ya kuwalazimisha watoto kutunza wazazi wao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Rais wetu; alikutana na wazee akawaambia na amekuwa akiendesha kampeni, mimi nasikia tangazo kwenye redlo, ambayo inasema wazee watunzwe ngazi ya jamii, ngazi ya familia, lakini kuna wakati mwengine Serikali inapaswa kuweka mkono wake pale ambapo wazee, watoto wao wanashindwa kuwatunza. Hebu tuyatazame makazi ya wazee, huwa natoa mfano mara nyingi, bahati nzuri Waziri wa Fedha anapita barabara hii ambayo tunapita kwenda Bukoba na hiyo ndio anapita kwenda kwake. Mheshimiwa Waziri aende pale Sukamahela, kuna kijiji cha wazee, lakini wazee wanashinda wamejianika juani pale wanaombaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea ni nini na awamu ya kwanza ya Serikali ya nchi hii walitengeneza kijiji ambacho kilikuwa kina-*accommodate* wazee? Sasa hivi makazi ya wazee katika nchi hii hayapendezi, hawana vyakula, hawana magari, hawana matibabu. Kwa hiyo, naomba bajeti iwaguse wazee, hawa watu tuwatambue, mjue na ninyi ambao bado ni vijana mnakwenda kulekule, njia ni moja. Kwa hiyo, msije mkafikiri kwamba, ujana wenu hamtakuwa wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ametuambia tuandae vizuri, tupange mapema namna ya kuzeeka kule mbele. Tukipanga vizuri hata ninyi ambao ni

vijana mkiisaidia wazee kupanga humu ndani ya Bunge, tutahakikisha kwamba, na ninyi mkizeeka mtakuta mazingira ya kuzeeka ni mazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka kusema ni kwamba, baadhi ya wazee ni wazalishajimali, ni watu wazima, ni watu ambaao bado wana nguvu. Kwa hiyo, wakitumika vizuri, wakasaidiwa wanaweza kusaidia na mchango wao unaweza kuendelea kuonekana. Nasema hivyo kwa sababu, wanawake, vijana, wana nafasi yao katika halmashauri. Wanawatengea pesa, lakini hakuna mahali popote katika bajeti hii walipotuonesha kwamba, wazee wanaweza kusaidiwa namna hii au wanaweza kukopesheka. Kwa hiyo, halmashauri, Serikali, imewaacha solemba, yaani imewaacha solemba huko, hawajulikani watapata wapi kipato. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeenda katika kitabu cha TAMISEMI, wamesema wametambua wazee jumla ya 366,282; wanawake wakiwa 195,771 na wanaume wakiwa 170,481. Nikajiuliza je, hii Serikali inajua idadi ya wazee katika nchi yetu? Maana katika sera waliyounda wenyewe walisema wazee ni asilimia 10 ya *population* ya nchi. Kwa hiyo, kama tunajikadiria kufika milioni 60 ina maana wazee wako kama milioni sita. Je, wamewapangia nini? Waziri atwambie, sisi wazee ametupangia nini katika bajeti yake? Tunawakaribisha na wao waje huku tuliko sisi, je, wametupangia nini ndani ya bajeti hii? Hawajatugusa kabisa, gusa wazee. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema hivi kwa sensa ya mwaka 2022 ambayo inakuja mwaka kesho watusaidie sensa hii kutuonesha wazee ni wangapi? Wazee walio katika mfumo rasmi ni wangapi? Wazee wanaopata *pension*? Wakulima wale ambaao wananyanyasika? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wazee, humu wote ni wanasiasa wameenda kwenye kampeni nyumba hadi nyumba, wameona namna gani wazee wanavyoteseka nchini, wazee wanatupwa na watoto wao, Serikali imekaa

kimya. Kwa hiyo, naomba Serikali katika jambo hili ihakikishe wazee wanapata huduma ya kutosha, wazee wanatambulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha, hata wale wanaopata *pension* ambao wametumika katika nchi hii, miaka nendarudi wakifika wakati wa kustaaafu hakuna anayewaangalia wanakaa miaka miwili, mitatu, minne, bila kulipwa mafao yao. Kwa hiyo, tunaona jinsi wazee katika nchi yetu wasivyoweza kuthaminiwa; ni kwamba, tuendelee kuwathamini na tuhakikishe wanapostaafu wapewe *pension* zao, lakini hata bajeti hii, kama sio mwaka huu basi mwaka kesho, Serikali ihakikishe kwamba wazee wanatunzwa, wanaangaliwa makazi yao, lakini pesa yao ionekane kabisa katika bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, njie kwa watoto wa mitaani. Nigusie kidogo yote; swalii ni moja au jibu ni moja kwamba watoto watunzwe kwenye familia. Nataka kuwaambia kwamba kuna familia ambazo zina matatizo kiasi cha watoto kulazimika kuingia mitaani. Kama ilivyo kwa wazee, inawezekana Serikali haijui kabisa hata watoto walioko mitaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuionya Serikali hii kwamba kutojua na kutoshughulikia watoto wa mitaani tunalea mfumo wa ujambazi. Tunaulea sisi wenyewe, tusilalamike, kwa sababu hawa wanakaa mitaani, wanabaka, wanafanya ujambazi, lakini wanazaana. *They multiply* kwa hiyo, wanajenga kizazi cha aina fulani ambacho baadaye tusije kulalamika kule ujambazi umekua aah! Ujambazi haukui ni kwamba sisi na hasa Serikali imeshindwa au imewezesha mfumo wa kulea hicho kitu ukaendelea. Kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba sasa ifike mahali, Serikali ipange kiasi fulani kwa *GDP*, kama nchi nyingine wanavyofanya. Huwezi kufanikiwa kwa mwaka mmoja, lakini tuwe na malengo, tunaweza kutoa kiasi fulani by percentage katika *GDP* yetu, tunaweza kwa ajili ya watoto

wetu na kwa ajili ya wazee. Nchi nyingine zimeweza kufanikiwa kufanya hivyo, ndiyo maana unakuta watoto wao wanalipwa na wazee wanalipwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sipendi sana na sisi Waafrika hatuko hivyo, kwamba wazee waende kulelewa katika nyumba za wazee, lakini ikilazimika kufanya hivyo, naomba Serikali isikwepe kufanya, ni wajibu wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Conchesta namwita Jonas Mbunda, halafu ajiandae Mheshimiwa Ahmed Ally Salum.

MHE. JONAS W. MBUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/2022. Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi leo kuwepo hapa kwenye Bunge lako Tukufu. Vile vile naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa utendaji wake mzuri uliotukuka ambao anasimamia na kuhakikisha kwamba kazi inaendelea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile nichukue nafasi hii nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kutupa shilingi milioni 500 kila jimbo kwa ajili ya kuondoa changamoto au kupunguza changamoto kwenye barabara zetu kuititia *TARURA*. Kwa kweli naomba nimpongeze sana.

Naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Naibu wake *Engineer Masauni*, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kuandaa taarifa ya bajeti ya mwaka 2021/2022 ambayo imetuonesha kwamba inajibu changamoto zinazotukabili katika maeneo mbalimbali hasa kwenye majimbo yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Daniel Sillo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Makamu wa Mwenyekiti Mheshimiwa Kigua pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa maandalizi mazuri ya taarifa na kwa kushirikiana bega kwa bega na Wizara ya Fedha kuandaa na kukamilisha bajeti ya mwaka 2021/2022. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Mawaziri kupitia Wizara zote na Manaibu pamoja na Makatibu Wakuu kwa sababu bajeti hii ya Serikali ya mwaka 2021/2022 inajumuisha Wizara zote ili kuhakikisha kwamba sasa tunasonga mbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kusema kwamba kwa ujumla bajeti ya mwaka 2021/2022 imejibu changamoto nyingi na sehemu kubwa ya changamoto ambazo Waheshimiwa Wabunge tulikuwa tunachangia katika Wizara mbalimbali itatusaidia sana sisi kuonekana kwamba mwaka huu tumefanya kazi ya maana na tumejitahidi kushirikiana na Serikali; na kama Serikali itatekeleza bajeti hiyo kama ilivyoandaliwa, nina uhakika kwamba tutakuwa tumefanya jambo la maana sana kwenye majimbo yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Wizara ya Fedha kwa maono ya kuhakikisha kwamba tunakusanya kodi za kutosha ili kuweza kukidhi bajeti ambayo ipo mbele yetu. Binafsi naunga mkono mapendekezo yote ya makusanyo ya kodi yaliyopendekezwa, nina uhakika kwamba hatutaweza kufanya masuala ya maendeleo bila ya kuwa na fedha za kutosha. Kwa hiyo, lazima tupate maumivu lakini tutakuja kufurahia baada ya changamoto nyingi kuondolewa kwenye maeneo yetu ya majimbo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima ya utaratibu wetu wote tulioupanga, lengo kubwa ni kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu na kuondoa umasikini. Suala hilo haliwezi kutekelezwa kama mambo yale

yanayohusu jamii na shughuli zote zinaohusu maendeleo yetu hazitasimamiwa na kutekelezwa kwa wakati. Tunaweza tukafanikisha tu kukamilisha dhima hiyo na siku ya mwisho lengo letu, tunachohitaji ni kuona kwamba wananchi wote tumeondokana na umaskini ambao umeenea kwenye maeneo mengi ya vijijini. Siku ya mwisho tutakapopima sasa kama malengo yetu tumefikia ni kuhakikisha kwamba huyu mwananchi sasa ameondokana na umasikini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuimarisha viwanda vyetu, naipongeza sana Serikali kwa kuondoa tozo kwenye maeneo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba viwanda vyetu sasa vinaimarika. Vile vile naomba niipongeze Serikali kwa sababu imeweka tozo kwenye bidhaa mbalimbali zinazoingia ndani ya nchi zikiwa na lengo kubwa la kuhakikisha tunalinda viwanda vya ndani. Tusipolinda viwanda vya ndani ina maana hatutaweza kufikia lile lengo ambalo tumelipanga la kuondoa umasikini na kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande huo wa viwanda naomba sana Serikali kuweka mazingira bora ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanafanya biashara katika mazingira yanayokubalika. Kwa mfano kuna vikwazo vidogo vidogo, unaweza kukuta mwananchi wa kawaida anataka kuanzisha biashara ndogo, lakini mchakato anaotakiwa apitie mpaka aanzishe hiyo biashara, unamkatisha tamaa. Kwa mfano mtu leo ana mtaji wake mdogo, anataka aanze biashara, masharti anayopewa kama anahitaji leseni, lazima aende *TRA* akafanyiwe *assessment*. Kwa hiyo, ina maana mwananchi huyu anaanza kulipa kodi kabla hata hajaanza kufanya biashara yoyote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe Serikali ingeweza kutengeneza mazingira ya kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanaweza kufanya biashara na baada ya kuanza kufanya biashara ndipo waanze kufikiriwa kwamba wanatakiwa wachangie kwenye pato la Taifa. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali yangu, kwa sababu ni Serikali Sikivu,

imetusikiliza kwa mambo mengi, nina uhakika kwamba hilo mtalifanya kazi ili kutengeneza mazingira mazuri kwa wananchi wetu waweze kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika maeneo hayo ya viwanda naishauri Serikali isimamie miundombinu ambayo ipo katika maeneo haya yaliyotengwa ya viwanda yawe katika hali nzuri. Kwa mfano barabara, umeme, maji kwenye maeneo haya yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda naiomba Serikali iweke mazingira mazuri ili tuhakikishe kwamba shughuli zetu zinaenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo mambo yote hayawez
kufanyika kama kuna nyanja nyingine za kiuchumi pamoja
na kijamii hazitatendewa kazi. Kwa mfano, ukiangalia kwenye
suala la afya, ili hawa wananchi baadaye tuweze kuwapima
maisha yao kwamba yako bora au yanaenda vizuri lazima
kwenye afya wawe kwenye hali nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali
kwa kuhakikisha kwamba inaendelea kujenga hospitali, vituo
vya afya pamoja na zahanati na kupeleka dawa na vifaa
tiba kwenye hospitali hizo. Yote hiyo lengo lake ni kuhakikisha
kwamba wananchi wetu wanakuwa kwenye hali nzuri kiafya.

Kwa hiyo, naipongeza Serikali na ninaomba sasa
tuendelee na juhudhi hizo kwa sababu bajeti tayari imetengwa
na itekelezwe ili tuhakikishe kwamba wananchi hawa
wanaishi katika maisha mazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni elimu.
Naipongeza Serikali kwa kusimamia sana kutengeneza
miundombinu kwenye suala la elimu, kujenga madarasa na
sasa hivi tunategemea kupata fedha nyingine kwa ajili ya
kujenga Shule za Sekondari kwenye kila Jimbo. Hiyo itatusaidia
kwanza ku- *rescue situation* ya wanafunzi wengi ambaao
walianza kuingia kuititia mfumo wa Elimu Bila Malipo
ambao wanaanza kutoka mwakani, kwa hiyo, hii
itatusaidia kupunguza changamoto kwenye suala hili la elimu.
(*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze mama yetu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Prof. Ndalichako kwa kutusikiliza sisi Wabunge, tulikuwa tunapiga kelele na kusema kwamba mitaala yetu irekebishwe. Tayari nimeona tangazo tarehe 18 wadau wameitwa kwa ajili ya kuanza kuchangia mawazo kwenye masuala ya mitaala ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naipongeza sana Serikali, naomba tuendelee ili tuhakikishe kwamba tunafikia malengo. Kuna suala lingine la umeme. Unakuta kwenye Majimbo yetu, kwa mfano mimi kwenye Jimbo langu kuna vijiji 27 havijapata umeme, lakini katika hivi vijiji 27 kuna kata mbili hazijapata kabisa umeme. Kwa hiyo, naomba sana baada ya bajeti hii Serikali isimamie wananchi wale wapate umeme na vijiji vile vyote vipate umeme ili tuweze kuhakikisha kwamba tunafikia maendeleo ya kweli. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni maji. Naiomba sana Serikali, kwa sababu tutapitisha hapa bajeti; na ninaomba Wabunge wenzangu tushirikiane kuipitisha hii bajeti, ili sasa ile miundombinu ya maji na mambo mengine yasaidie tuweze kumtua mama ndoo kichwani. Kwa hiyo, naomba niishukuru sana Serikali kwa jitihada hizi, lakini naiomba sasa kutekeleza haya kwa wakati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kilimo. Naiomba sana Serikali izingatie kilimo ambacho kinaleta tija. Tuangalie kwanza kwenye uzalishaji amba o unaleta tija. Vile vile naomba Wizara ya Kilimo watumie vituo vya utafiti ili sasa tuweze kufanya kilimo ambacho kitaleta tija kwenye wananchi watu. Kwa mfano, kuna mashirika ya utafiti kama *TARI*, *TIRDO*, *TEMDO*, *CAMARTEC*, Serikali ihakikishwe kwamba mashirika hayo yanapata bajeti ya kutosha ili sasa utafiti utakaofanyika na majibu yale ya utafiti yaweze kuwafikia wananchi kwa ajili ya kuendeleza kilimo chetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la UVIKO 19. Kwenye suala la UVIKO 19 tumeathirika sana kwenye upande wa utalii na usafiri hasa kwa upande wa ndege, lakini kwenye taarifa ya bajeti ambayo imetolewa na Mheshimiwa Waziri

wa Fedha, sijaona kama Serikali imeweka mikakati ya dhati na kutenga fedha za kutosha kuhakikisha kwamba inatibu majeraha hayo yaliyotokana na UVIKO 19. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Serikali ifikirie kwa upande wa ndani tunafanya nini? Badala ya kutegemea mikopo kutoka nje au na misaada, sisi wenyewe tumejidhatiti namna gani kuhakikisha kwamba tunasimamia na kudhibiti suala hili la UVIKO 19? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwenye suala la sensa, kwa sababu sensa ni suala la msingi sana kwenye maendeleo ya jamii na ili baadaye tuweze kupata taarifa sahihi za idadi ya watu na makazi, ningeomba sana Serikali iweke nguvu za kutosha katika kusimamia na kuhakikisha kwamba tunapata sensa ya idadi inayokubalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Anton Mwantona, wajiandae Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum.

MHE. ANTON A. MWANTONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa kunipatia nafasi nami kuchangia katika Hotuba hii ya Bajeti ya mwaka 2021/2022 katika Bunge lako Tukufu. Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu kutupatia afya ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea kwa kifupi sana. Kwanza nianze kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nilipokuwa nakwenda kwa mara ya kwanza kwenye kampeni, nimezunguka kwenye vijiji vyote 99 vya Rungwe, nimezunguka kwenye kata 29 zote za Rungwe, matatizo makubwa ya wananchi katika Jimbo langu ilikuwa ni barabara, maji, umeme na matatizo mengine madogo madogo. Matatizo makubwa ambayo wale wananchi walikuwa wakiniambia ukienda Bungeni ukatusemee ilikuwa ni hayo makubwa matatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza na barabara za vijijini. Tumerekebisha Mfuko wa TARURA, Serikali imerekebisha; tunakwenda kupata shilingi 100/= kwenye mafuta, kwa hiyo, tatizo la barabara nina uhakika linaenda kutatuliwa na hivyo kunirahisilia mimi maisha kama Mbunge wa Jimbo, kuwaambia na kuwanyooshea vidole kwamba Serikali yetu imefanya mambo haya, haya na haya. Pia nashukuru kwa kiasi kikubwa, kwa shilingi milioni 500 ambayo imepatikana kwa kila Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kampeni zangu nilizunguka nikakuta kuna kijiji ambacho hakina barabara ya kuunganisha. Nilipanda pipipiki mpaka kwenda kupiga kampeni kwenye Kijiji hicho; kinaitwa Kijiji cha Kikole. Ni kilometa 12 kutoka kwenye mji amba unapitika unaitwa Masukuru mpaka Kikole mpakani na Kyela. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu hilli kwamba hiyo fedha tumeielekeza huko na wananchi wa Kikole niwaambie, mama amesikia kilio chenu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba amesikia kilio chenu na Serikali ya Chama cha Mapinduzi imesikia kilio chenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali, namshukuru sana Waziri wa Fedha, nashukuru sana Baraza la Mawaziri ambalo limefikiria kupeleka hii shilingi milioni 500 kwenda kuwasaidia wananchi katika maeneo ambayo yapo katika taabu kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maji, pia tulikuwa na tatizo kubwa katika mji wetu mkuu pale Tukuyu katika Jimbo letu la Rungwe, lakini Serikali pia ilituletea shilingi milioni 500 mwezi uliopita na miradi mbalimbali inaendelea kutekelezwa katika Jimbo hilo. Wananchi wamefurahi sana na wanasema Mwantona tupelekee salamu kwamba wameiamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa umeme, sisi tuna vijiji 99. Vijiji ambavyo vilikuwa na umeme ilikuwa ni vijiji 66 na vijiji 33 vilikuwa havina umeme. Niwaambie wananchi wa Jimbo la Rungwe kwamba vijiji vyote 36 kwa mujibu wa

bajeti hii, vinakwenda kupata umeme na wananchi wanaenda kufurahia matunda ya uhuru wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitashukuru Wizara ya Ardhi ambayo imekwenda kupunguza tozo au kiasi cha *premium* ambayo ilikuwa inalipwa katika upimaji wa viwanja vipyta. Wametoa kutoka asilimia 2.5 hadi 0.5; lakini pia kwenye uhalalishaji wametoa kutoka 1% hadi 0.5%. Naona kabisa kwamba tunapokwenda, wananchi wengi watapima ardhi kwa sababu gharama imepungua, itakuwa ni ukombozi katika maisha yao kwa sababu ardhi ni mwanzo wa kujipatia mitaji na kufanya biashara zao ambazo zitawasaidia katika maisha yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni shukrani pekee pia. Vile vile nashukuru kwa bajeti hii imekwenda kuangalia *Property Tax*. Nilimsikia mama kipindi fulani anasema kwamba tutumie akili zaidi kuliko kutumia nguvu katika ukusanyaji wa kodi za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba Waziri wa Fedha ametumia akili zaidi katika ukusanyaji wa *Property Tax* kuliko ilivyokuwa hapo awali. Kodi hii inakwenda kuongeza walipa kodi wengi zaidi (*tax base*) wanakwenda kuongezeka. Pia gharama za ukusanyaji wa kodi zinakwenda kupungua. Mara ya kwanza tulikuwa tunatumia Watendaji wa Kata, watu mbalimbali walikuwa wanaenda katika maeneo mbalimbali, gharama zilikuwa kubwa, lakini kwa kutumia utaratibu ambao umeshawekwa, gharama za ukusanyaji wa kodi zitapungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu wazi kwamba kama kuna changamoto ambazo zipo, zishughulikiwe lakini utaratibu huu ni mzuri ambazo utasaidia sana kukuza mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nitoe ushauri kidogo kwa Serikali na nitaomba Waziri wa Fedha anisikilize especially kwenye halmashauri zetu. Halmashauri zetu

ukiangalia kuanzia mwaka 2016/2017, 2017/2018, 2018/2019, 2019/2020 uwezo wa kujitegemea kwa halmashauri zetu uko chini 2016/2017 halmashauri ilikuwa na uwezo wa kujitegemea halmashauri zote kwa wastani ilikuwa ni asilimia 11, 2017/2018 uwezo wa halmashauri zetu kujitegemea nchini ulikuwa ni asilimia 13, 2018/2019 uwezo wa halmashauri zetu kujitegemea nchini kote ilikuwa ni asilimia 15 na mwaka huu kwa mujibu wa taarifa ya CAG uwezo wa halmashauri zetu kujitegemea umefikia asilimia 15 ina maanisha nini? inamaanisha kwamba mapato ya ndani ya halmashauri ukagawanya na matumizi mengineyo pamoja na mishahara ndiyo uwezo wa halmashauri kujitegemea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme kwa dhati kabisa kama Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo ni sikivu waangalie kwa jinsi gani kubadilisha *mindset* kuziwezesha halmashauri zetu kuongeza uwezo wa kujitegemea. Si vizuri sana kuonekana kwamba Serikali Kuu inaongeza uwezo wa halmashauri kutokujitegemea ili tuweze kuwasaidia tumekuja Wabunge wote hapa tumeshangilia sana madiwani wetu kupewa posho zao tumeshangilia sana watendaji wa kata kupewa posho zao. Lakini nishauri kwa Serikali yangu tukufu kwamba tuwasaidie halmashauri zetu kuendeleza kukusanya mapato kuliko kuapelekea pesa kwa ajili ya kuwalipa madiwani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikatoa mfano mmoja tu ambao unaweza ukasaidia kuongeza mapato ya halmashauri *service levy* ambayo ni mapato makubwa sana chanzo kikubwa halmashauri zetu haikusanyi sheria ya fedha *Local Government Finance Act* ya Mwaka 1982 ambayo imekuwa *advanced* 2002 inasema kabisa kwamba halmashauri itakusanya *service levy* kwa mtu ye yeyote ambaye ana leseni ya biashara yoyote lakini utafiti mdogo nilioufanya halmashauri nydingi hazikusanyi *service levy* mtu ye yeyote mwenye biashara ana leseni ya biashara anatakiwa ali pe *service levy* lakini hawalipi na ndiyo maana unakuta mapato ya halmashauri yanakuwa chini na hivyo uwezo wa kujitegemea unazidi kushuka mwaka hadi mwaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tufanye utafiti kwenye *service levy* tuzisaidie halmashauri zetu ziweze kukusanya *service levy* ili kuongeza mapato yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niliseme hilo kwa sababu siyo picha nzuri sana kwa Serikali kuonekana halmashauri nydingi sana zinategemea Serikali Kuu kuendesha shughuli zake siyo picha nzuri sana *financial statement* tunazidi kuzi-spoil za halmashauri. Kwa mfano nimeangalia haraka haraka hapa kwenye taarifa ya CAG kuna majiji yetu Matano. Jiji la kwanza ambalo liliongoza lilikuwa na uwezo mzuri wa kujitegemea lilikuwa ni Jiji la Dar es Salaam ambalo limeshavunjwa lilikuwa na asilimia 484 walikuwa na mapato ya bilioni 16 wakapokea mapato kutoka Serikali Kuu bilioni 3.6 ilikuwa ni milioni 484 ilikuwa ni asilimia 484 uwezo wake wa kujitegemea ulikuwa siyo mbaya ni mzuri lakini jiji la pili ilikuwa ni Dodoma walikuwa na asilimia 45 ya kujitegemea, jiji la tatu ilikuwa ni Arusha walikuwa na asilimia 32 ya kujitegemea. Jiji la nne ilikuwa ni Mbeya asilimia 20 ya kujitegemea Jiji la tano na la mwisho ilikuwa ni Tanga asilimia 6 ya kujitegemea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tusione fahari sana sisi kama Serikali kuwawezesha kuwapelekea hela za ruzuku kwenye halmashauri vinginevyo tuwatafutie mapato mengine ambayo yatawasaidia wao kuwawezesha kwenye *financial statement* zao kwamba uwezo wao wa kujitegemea unazidi kupanda mwaka hadi mwaka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anton ahsante

MHE. ANTON A. MWANTONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Sasa namuita Mheshimiwa Zulfa Omar, jiandae Mheshimiwa Ahmed Salum, Mheshimiwa Daimu Mpakate.

MHE. ZULFA MMAKA OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi jioni hii kuchangia katika bajeti

yetu hii ambayo iko mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataala kwa kutujaalia uzima wake na uhai wake na pumzi zake ambazo hatulipii kiasi chochote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza mama yetu mama Samia Suluhu Hassan kwa utendaji wake mzuri na umahiri wake na njia nzuri ambayo wametuonesha sisi wanawake kama tunaweza kuongoza bila ya kusaidiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka kwa mama angu mama Samia nimpongeze Mheshimiwa Rais wangu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kule Zanzibar na bajeti nzuri ambayo imesomwa tu hivi juzi ambayo imeleta matumaini makubwa na imeleta chachu kubwa ya maendeleo hasa katika uchumi wa blue. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kaka yangu Naibu Waziri na Mawaziri wote kwa ushirikiano wao wa kutuletea bajeti hii iliyojaa matumaini ya watanzania hususan wazanzibar katika zile sehemu ambazo wametutaja na wametusema na wametuherumia na kutuonyesha kwamba muungano huu tunazidi kuunganisha kwa mambo mazuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kuzungumzia masuala ya nyanja za kodi katika sekta ya kilimo. Nimpongeze sana Mheshimiwa mama yetu kwa kuona kwamba iko haja ya kupunguza kodi hizi katika sehemu ya kilimo pamoja na pembejego. Wakulima hawa wataweza kulima na kupata pembejego kwa njia nzuri na kufanya kilimo hiki bila matatizo yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hapo niipongeze kwa kuondoa katika kodi za masuala mazima ya uchimbaji wa madini suala hili litachangia sana uchimbaji mzuri wa madini katika nchi yetu na madini haya yataweza

kuongeza pato katika nchi yetu na uchumi wetu utazidi kuimarika kwa hali ya juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo naomba nichangie katika suala la biashara la Tanzania Bara na Zanzibar. Tuseme wazanzibar tumeefarijika sana kutokana na imani yao ambayo tumeonyeshwa. Kulikuwa na changamoto kidogo ambazo zilikuwa zinaikabili katika suala zima la biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaumia sana pale biashara zetu Zanzibar tunapolipia mara mbili ushuru huu lakini sasa hivi tumeona kwamba bajeti hii ambayo iko katika meza zetu imeondosha changamoto hii kwa hali nzuri sana. Jambo zuri husifiwa na tunaona kwamba imani kubwa ambayo tumeoneshwaa sisi wazanzibar tunaahidi kwamba tutailipa imani hii kwa kushirikiana na kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli suala hili ni zuri na sisi twaahidi kwamba tutashirikiana ila tumuombe Mheshimiwa Waziri suala hili aliangalie vizuri hasa katika bandari zetu. Watu wa bandari wanausumbufu sana katika suala hili kwa hiyo tusiichukulie tu kwamba tayari limeshawekwa lakini Mheshimiwa Waziri usimamie watendaji wako ulifatilie ili suala hili liweze kuenda sambamba na nia ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende katika miradi ya Muungano tuna miradi mingi sana Zanzibar ambayo fedha zake zinatoka katika Serikali ya Muungano wa Tanzania kuna baadhi ya miradi hii inachelewa kutendeka kutokana na ucheleweshaji wa kusaini mikataba ama pesa wakati mwingine kusuasua katika miradi hii tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri suala hili akae tena na watendaji wake washauriane vizuri na wasimamie vizuri ili fedha hizi ziweze kupelekwa kwa wakati na miradi ile iweze kutendeka na Zanzibar ifaidike ilivyo katika mgao huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa watanzania mjenga nchi ni mwananchi kwa hiyo niwashauri sana watanzania wenzangu tuungane kwa Pamoja kulipa kodi kusimamia rasilimali za Tanzania ili ziweze kutuongezea pato katika nchi yetu. Mambo mazuri yanaletwa na mwananchi mwenyewe, tukianza kusuasua katika ulipaji wa kodi naamini kwamba yale mazuri ambayo yamekusudiwa katika bajeti hii hayatoweza kutendeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa ushauri wangu kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mama yetu katuonyesha njia nzuri sana ya kuifata. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge bajeti hii ambayo ipo katika meza yetu inataka kumshusha mwanamke ndoo kichwani, bajeti inaenda kumaliza vifo vyta mama na Watoto, bajeti hii inaenda kuleta madawa hospitalini, bajeti hii inasimamia wamachinga waweze kufanya kazi zao vizuri, bajeti imewasema wamama waweze kujiwezesha na wao watasaidiwa katika Serikali hii, bajeti hii inaenda kujenga barabara zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tuipitishe kwa moyo mmoja na tuwe na nia moja na tuungane kwamba watanzania wajue kwamba Wabunge tumekusudia kupitisha bajeti yenye mambo mazuri bajeti ya kimapinduzi ambayo imetengenezwa kwa umahiri mkubwa na umakini mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Sasa namuita Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, jiandae Mheshimiwa Daimu Mpakate.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu kuchangia kwenye hoja ya bajeti yetu hii nzuri bajeti ya kwanza ya Mheshimiwa Rais wetu mama yetu Samia Suluhu na bajeti

ya kwanza kwa Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Waziri wa Fedha. Naomba tu niwasalimie Waheshimiwa Wabunge kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof!*)

WABUNGE FULANI: Kazi iendelee!

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri bajeti hii inakwenda kumaliza matatizo mengi sana na hasa hasa kwenye maeneo yetu ya vijiji na hasa hasa kwa wananchi na wakulima wanaoishi maeneo ya mbali na miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni awamu yangu hii ya tatu nakwenda ya nne nimekuwa nikisema mara nyangi sana tupate fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma bajeti hii inakwenda kukamilisha maboma. Katika Jimbo la Solwa lina mabomba zaidi ya 150 ukichukua katika zahanati nina maboma 39 sasa hivi ukienda kwenye elimu ya msingi nina maboma zaidi ya 53, ukienda kwenye Sekondari nina maboma zaidi ya 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishukuru sana Serikali ya Samia kwamba kweli kabisa tunakwenda kutatua matatizo haya ya maboma yetu. Lakini vilevile inakwenda kumaliza kabisa matatizo ya barabara zetu, nina barabara zenye urefu wa kilometra 743 *TARURA* lakini hakuna barabara hata moja ambayo ilikuwa inanisumbua kama barabara ya kutoka Didia kuja Solwa. Fedha hizi tulizopata Mheshimiwa Dkt. Mwigulu pamoja na Mheshimiwa Rais wetu nikushukuru sana tunakwenda kumaliza matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na barabara ilikuwa ni muhimu kweli kwenye kata zaidi ya sita zenye kulima mpunga zinalima mazao mengi sana mpaka watu wa Burundi na Rwanda wanakuja kununua mazao katika Jimbo la Solwa. Kwa hiyo, kwa kweli hapa sasa hivi wakulima pamoja na wafugaji wa Jimbo la Solwa wamekusikia na wamefurahi sana kwa Serikali yao hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha tarehe 25 Februari, tulisaini mkataba wa maji Tinde pale kwa agizo la Hayati aliyekuwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli mradi huu ulisainiwa Tinde kwa maana mradi mzima unaitwa Tinde *package* ni mradi wa maji wa vijiji zaidi ya 15 Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tangu tumesaini mradi huu mpaka sasa hivi mkandarasi ameshindwa kuendelea kwa sababu ya suala zima ya VAT kwa maana ya GN. Nkuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha lishughulikie hili haraka ili mkandarasi aanze kazi aanze kazi mara moja, na mimi nimelisema hivi ili wananchi kwanza wa Jimbo la Solwa wasikie wakusikie wewe waisikie na Serikali yao kwamba tatizo hili sasa limekwisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda nikushukuru Mheshimiwa Waziri umeigusia sana *blue print* umeigusia sana sana na nikushukuru sana tu umeondoa ile asilimia 15 kwa suala zima la sukari nakadhalika tunakwenda vizuri sasa lakini kuna VAT *refund on export* hii bado inazuia *export* ya bidhaa zetu zinazozalishwa ndani ya nchi yetu matokeo yake nini? Biashara yoyote bidhaa yoyote inayozalishwa ndani ya nchi yetu hii unapokwenda kuuza nchi Jirani au nchi za SADC lazima ulipe VAT unapokwenda kwenda kuomba VAT hii na bidhaa tayari imeshatoka bidhaa ikishatoka unatakiwa urudishiwe ile ili uendelee kuzalisha na kwenda kuuza bidhaa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii sisi ni tatizo kubwa wafanyabiashara wengi wamekuwa hawafanyi hawa *export* na hii tatizo kubwa sana inadumaza *export* leo ninavyokwambia Mheshimiwa Waziri wa Fedha wafanyabiashara wanaokwenda Rwanda kuwekeza waki-target soko la Zaire. Leo wafanyabiashara wengi wanakwenda kuwekeza Uganda waki-target soko la Tanzania na nchi za Zambia kwa sababu hizo nchi ni nchi nzuri sana na ziko mstari wa mbele ku-refund VAT on export product kutokana na manufacturing. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hili lichukue lifanyie kazi linadumaza *export* na

ukishadumaza *export* maana yake unadumaza *foreign currencies* ndani ya nchi yetu utaona kuna tatizo kubwa sana kwenye suala hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitizama Djibouti leo wana *free zone* kubwa sana inaweza ikawa *the second largest au third largest in Africa* baada ya Afrika Kusini wamejenga bandari kubwa wamejenga eneo kubwa kweli kwa ajili ya wawekezaji wa viwanda wanaokwenda kuwekeza pale wanataka sasa kuwa katika Afrika wao wawe kama vile Hong Kong kama vile Dubai wanataka kuifanya Djibouti iwe hivyo na Serikali ya China imeisaidia 3.5 bilioni katika mradi mzima ule. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuwe makini na hapa nikushauri Mheshimiwa Waziri atenge fedha kwa ajili ya *research development* katika Wizara yake. Tenga fedha kwa ajili ya *research and development* tusiende kichwa kichwa lazima tuwajue wenzetu na nchi Jirani wa Kenya wanafanya nini, Waganda wanafanya nini, Rwanda wanafanya nini Burundi wanafanya nini, Zambia hawa nchi zote zinazotuzunguka ni wapinzani wetu na usifikiri wanafurahia maendeleo yetu kwa namna moja au nyingine wanatizama sera, wanatizama sheria zetu, wanaziweka mezani wanazifanya kazi ili wawe *advantage Zaidi* ya sisi Tanzania ndio wanavyofanya tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Kenya hapa wanajenga bandari hapa Lamu bandari kubwa sana ambayo tayari inakuwa *competitor* ya bandari yetu ya Dar es Salaam na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo nilitaka tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha lichukue na ikiwezekana tufanye kama wenzetu Ethiopia wamekuwa na maeneo maalum kabisa yaani na wanavyotenga maeneo kwa ajili ya viwanda wawekezaji wa nje na wa ndani ya nchi kwa mfano wanakuwa na *strategic* zao tunataka kwenda kumaliza matatizo ya masoko ya pamba katika Mkoa wa Shinyanga na Simiyu tunataka kwenda kumaliza masoko kwa mfano ya

mazao ya mawese Singida sijui, Singida hapo tunataka kwenda wanakuwa na *strategic* wanatenga maeneo, wanajenga maeneo wanaweka barabara wanaweka lami, wanaweka umeme wanandaa hili kwa ajili ya viwanda kwa wawekezaji wa viwanda tu atoke nje akija anataka kuwekeza mafuta anaambiwa bwana mafuta ya kula nenda Singida, nenda Kigoma kiwanja hiki hapa na hati hii hapa biashara imeisha nenda kawekeze ndiyo wanavyofanya wenzetu ukienda Thailand hivyo hivyo, ukienda Ethiopia hivyo hivyo yaani hupati shida kabisa kwenye uwekezaji wa nchi kama hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ukishakuwa na *East Africa Development* haya yote yataangukia kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine Mheshimiwa Waziri wa Fedha hii *blue print* ipige *overall* yote mnaigusa gusa hivi sawa kabisa mimi nakushukuru kwa namna ambavyo hata haya uliyoyachukua umeyafanyiakazi. Lakini ichukue ipige *overall* yote kabisa tuimalize ili sasa Tanzania iwe katika nafasi nzuri ya uwekezaji Tanzania tuweze kuwavutia wawekezaji wote wa ndani na nje ya nchi. Tanzania tuna jiografia nzuri bandari yetu iko katikati karibu na nchi zote za *SADC* Tanzania kuna amani tuna *advantage* nyingi mno ya watu kuja kuwekeza hapa Tanzania tuna *resources* nyingi tuna mali nyingi ambayo wawekezaji wanaweza wakaja kuwekeza katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa Shinyanga Simiyu peke yake inazalisha asilimia 60 ya pamba inayozalishwa Tanzania hii na mnajua pamba inaa jiri watu Zaidi ya milioni 21 lakini hakuna kiwanda kikubwa cha nguo Tanzania hii haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kimoja tu India kinanunua pamba yote ya Tanzania hii, hivi tunashindwaje kuwa na *Strategic Plan, TPDC, NDC* tukamwambia sikiliza chukua hii bilioni 100 jenga kiwanda kikubwa cha pamba hapa, chukua hii bilioni 100 jenga kiwanda cha mafuta hapa,

ukishajenga tangaza, uza watakuja wawekezaji, yaani ukishajenga kiwanda ikakaa vizuri Menejimenti kila kitu tangaza uza, chukua fedha jenga kiwanda kingine, tunakuwa na *strategic* tu, viwanda vikubwa 10 ndani ya nchi hii, nchi inainuka inakwenda vizuri sana katika maendeleo yetu. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ahmed ni kengele ya pili.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwigulu hili suala la viwanda nya pamba ni muhimu sana, ziko taarifa labda uzithibitishe kuwa *TANESCO* wanachaji viwanda hivi *capacity charge* hata kama havifanyi kazi, ndiyo maana wanashindwa kuviedesha, hebu tazama ili kuweza kujaribu *ku-cure* hili tatizo.

Mheshimiwa Daimu Mpakate, Mheshimiwa Dennis Londo, Noah Saputu Lemburis, ajiandae.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataala aliye niwezesha kusimama leo hii na kuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini, nimshukuru kipekee Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kukubali hisia za Wabunge wengi ambacho ndicho kilikuwa kilio cha muda mrefu kuanzia Bunge la Kumi na Moja na Bunge hili la Kumi na Mbili kuhusu suala la maji pamoja na *TARURA* nashurukuru sana, naamini ametoa heshima kwa Wabunge leo tunajisikia furaha sana, kuona namana ambavyo Rais ameyachukua yale yote ambayo tulikuwa tulikuwa tunayazungumzia katika kipindi chote na kuyaweka katika bajeti na katika utekelezaji halisi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuchambua bajeti hii kwa makusanyo yaliyopita ya Mwaka 2020/2021niwapongeze sana Wizara ya Fedha na wale wote waliohusika kukusanya fedha kwa kutumia mipango mbalimbali na kufikia asilimia 86 ya makusanyo yetu ya bajeti iliypita. Kwa kweli hili jambo ni likubwa tunatakiwa tuwape pongezi hasa Wizara ya Fedha na wengine wote kwenye idara mbalimbali waliohakikisha kwamba fedha hizi asilimia 86 ya makisio ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 yamefikiwa naomba sana Jambo hili tuliangalie na tuwape moyo hawa watu waendelee kufanya vuzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo nikirejea kwenye bajeti zilizopita za kisekta za Wizara mbalimbali sioni *reflation* hii ya asilimia 86 kwenye shughuli za maendeleo katika Wizara zingine, inaonekana kwamba kuna Wizara ambazo zimepata fedha za maendeleo chini ya asilimia 30 ambacho kwa kweli kwa hali ya kawaida hawasemi lakini inaonekana kama kuna Wizara zimekuwa ni muhimu zaidi kuliko Wizara zingine kwa kupewa fedha ya maendeleo ambayo iko chini ya asilimia 30

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama makusanyo yamekua asilimia 86 kwa tuliosoma hesabu tulitegemea na shughuli za maendeleo kwenye Wizara mbalimbali zifiki zaidi ya asilimia 50 lakini haikuwa hivyo, ina maana kwamba kuna Wizara ambazo zimependelewa zaidi kwa makisio yake kutekelezwa ya maendeleo zaidi kuliko vile ambavyo vimekisiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa hali ilivyokuwa kwa miezi miwilli iliyobaki makusanyo yanaweza yakafika asilimia 90 au 92 kwa mwenendo huu, kwa hiyo naomba zile Wizara ambazo hazijafikia angalau asilimia 50 nazo ziangaliwe zipewe fedha za maendeleo ili haja ile ya mipango yao iweze kufanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia na hili kuna jambo lingine naomba Wizara nalo uliangalie kwenye miradi hii ya maendeleo nashukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa milioni 500 kwa kila Jimbo. Siku zote huwa tunazungumza

majimbo yetu yanatofautiana wote tuna furaha kila Jimbo limepata milioni 500, lakini kwa maeneo mengine ni kilio! Kwa sababu hiyo milioni 500 namna ya kuitumia na kilometra tulizo nazo ni kizungumkuti, tunaona kwamba hili jambo mlione mbele ya safari mnavyogawa hivi vipaumbele vya maendeleo angalieni na ukubwa wa Majimbo kama tunavyolia siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ugawaji wa fedha za majengo, majengo ya zahanati, shule za msingi na sekondari ni vizuri basi muangalie na ukubwa wa majimbo, wingi wa shule na Kata jinsi ilivyo kubwa *ratio* ni muhimu sana. Kwa sababu inaonekana mwisho wa siku kuna Majimbo yataenda mbele Zaidi kuliko Majimbo mengine kutokana na ukubwa wa Majimbo ulivyo. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri wakati unagawa mipango hii ya miradi muangalie na ukubwa wa Majimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano; Tunduru tuna Kata 39 Jimbo langu lina Kata 15 napata shule moja, mwingine ana Kata Nane anapata shule moja, hayo majengo kila mmoja anapata matano matano ina maana mwenye kata nane atamaliza mapema kujenga majengo kuliko wenye Kata 15 na 39. Kwa maana hiyo tunaomba *ratios* iangaliwe wakati wa kugawa miradi ya maendeleo ili kila mmoja afikie ile *standard* ambayo inatkiwa kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana kulizungumza suala la kilimo, kwa watu wa Kusini, kilimo cha Korosho ni uti wa mgongo. Mkutano wa 18 uliona sakata la korosho liliyokuwa, natamani sana ile sheria ya *export levy* iangaliwe upya ili kuhakikisha kwamba aidha ifutwe ili kile kiwango kinachotozwa kwenye *export levy* ambacho ni sehemu ya gharama ya nunuzi kirudi kwa mkulima au irudishwe yale yote yaliyokubaliwa na wadau na kuanzisha *export levy* basi yafuatiliwe ili sekta ya korosho iweze kusonga mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili mwaka 2018 lilipotokea uzalishaji wa korosho umeshuka kwa asilimia kubwa. Mara ya mwisho tumezalisha tani 330,000, lakini msimu uliopita tumepata tani 206,000 ni kwa sababu kwamba yale yote ambayo yalikuweko kwenye *export levy* yalitakiwa yarudi kwenye kutekeleza sera ile ya Bodi ya Korosho na makubaliano ya wakulima pamoja na wadau wa korosho hayakuweza kutekelezeka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ahadi ya Serikali kwamba yote yale Serikali itatekeleza lakini kwa masikitiko makubwa napenda kusema ndani ya miaka mitatu misimu mitatu, Serikali imetoa billioni tatu kwenye kituo cha Naliendele na bilioni 10 kwa ajili ya kununua *sulphur*, yale mengine yote hayakuweza kutekelezeka.

Kwa hiyo, naiomba Serikali langalie kwa namna moja aidha wafute *export levy* kwenye korosho kwa sababu hakuna zao lingine lolote la biashara ambalo linatozwa *export levy*, hii tulianzisha wenyewe kwa ajili ya kuona namna ambavyo zao letu la korosho linadumaa na tukaanzisha ili kutafuta fedha la kusaida zao liweze kusonga mbele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyeikiti, jambo hili kwa kweli Serikali inahangaika sana inatafuta kila aina, nawaonea huruma Wizara ya Kilimo wanatafuta kila aina na sasa hivi kuna mgogoro wa *sulphur* huko kwa sababu wakulima wetu wameshindwa kupata *sulphur* ili waweze kuhudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa nizungumzie ni suala la hili *property tax*. Niishukuru Serikali na niipongeze Serikali kwa kubuni jambo hili, lakini kuna changamoto ambazo mnatakiwa mzifanyie kazi hasa tunaotoka Majimbo ya Vijijini, Naibu Waziri wetu wa Nishati anasema wekeni umeme hata kwenye nyumba za matembe. Leo nyumba nyingi za matembe zina umeme, zina Luku tuna zi-*charge* shilingi 1,000 maana yake tunaongeza gharama kwenye zile nyumba za tembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wakati wa utekelezaji muangalie hizi nyumba ambazo kwa kweli hadhi yake hazistahili kulipa hii *property tax* kwa kutumia *LUKU* na hasa zile nyumba za ibada. Nyumba za ibada ni kweli vijijini zina umeme lakini hizo ni nyumba za ibada kwa hiyo mfanye chini juu muweze kutambua nyumba hizi za ibada mtambue nyumba hizi za matembe ambazo hazistahili kulipa hii *property tax* ili kuleta maendeleo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka kuzungumza suala la Linganga na Mchuchuma. Namshukuru Rais ametoa mwanga wa kuendelea na mradi huu wa Linganga na Mchuchuma. Kwenye Linganga kwa maana ya makaa ya mawe kuna matatizo, naomba turejee mkataba ule, turejee sheria mpya ya Madini, Ngaka pale tunachima madini ya makaa ya mawe, lakini Serikali haipati chochote, hata *NDC* yenye we hawapati chochote kutokana jinsi mikataba ilivyokaa na hawa wawekezaji ambao tumeingia nao mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili Serikali ifanyie kazi ipitie ile mikataba yote Ngaka, ipitie mikataba ya Kiwira, ipitie mikataba ya Mchuchuma ili kuhakikisha kwamba Serikali inapata mapato kutokana na makaa ya mawe ili kuendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja kwa asilimia 100. (*Makof*)

MWENYETIKI: Ahsante. Mheshimiwa Dennis Londo, atafuatiwa Mheshimiwa Noah Saputu, Mheshimiwa Haji Makame Mlenga, ajiandae.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya bajeti na ninaomba niazé kwa kuchangia bajeti kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa yale yote ambayo yametokea tangu Bunge hili lilipoanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niishukuru Serikali ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kipindi hiki kifupi lakini kubwa kuliko yote ni kuendelea kutunza imani ya Watanzania kwa Chama cha Mapinduzi, kutunza imani ya Watanzania kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamefanywa katika kipindi hiki kifupi lakini kwa uchache suala la kupeleka fedha za ujenzi wa miundombinu ya shule hasa maabara na kuongeza vyumba vyaya madarasa katika Halmashauri mbalimbali wananchi wa wanashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia upelekaji wa shilingi milioni 500 kwa kila Jimbo kimsingi imeweza kwenda kujibu kero nyingi hasa za miundombinu ya barabara na Mikumi tumeamua kupeleka milioni hizi 500 kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Mto wa Ruhembe, mto ambao umeuwa watu wengi, wananchi wengi katika lile eneo lakini ni daraja ambalo kimsingi ni la kimkakati katika uzalishaji wa miwa na usafirishaji katika kiwanda cha Illovo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja hili linaenda kupunguza gharama ya uzalishaji kwa wakulima pia usafirishaji wa mazao yao kutoka mashambani katika Kata za Mikumi, Kidodi, Ruhembe, Ruaha na hata vidunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hotuba nzuri ya bajeti ambayo imejaa ubunifu mkubwa lakini pia inaongozwa na uzalendo wa hali ya juu, hotuba ambayo imechukua maoni ya Wabunge kikamilifu ni hotuba ya bajetiimeonesha uzalendo katika kulinda viwanda vyetu nya ndani na bidhaa ambazo zinazalishwa na viwanda vyetu nya ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupunguza tozo na kodi mbalimbali hili siyo tu kwamba linavutia wawekezaji kuja kuzalishia hapa ndani lakini linaenda kuongeza ajira na linaenda kuamsha uwekezaji wa ndani na hivyo kuboresha uchumi wetu katika namna mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii pia kuipongeza Serikali kwa ubunifu na kubuni njia bora zaidi ambazo hazimsumbui mwananchi lakini ni katika kuongeza *tax base* hasa kupitia kukusanya kodi ya majengo na viwanja kupitia simu lakini pia kupitia *LUKU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya *principal* za kodi ni kupunguza gharama ya ukusanyaji pia kuongeza kiasi cha ukusanyaji, shida kubwa ya makusanyo yetu ya kodi ni kwamba tunatumia gharama kubwa kukusanya kodi ndogo lakini pia kumsumbuu yule mlipa kodi kiasi ambacho mlipa kodi anatakiwa kutumia mara nyingine shilingi 5,000 ama Shilingi 10,000 kwa ajili ya kwenda kulipa shilingi 7,000.

Kwa hiyo, hali hii inapelekea wananchi wetu wengi kutojitoa kikamilifu katika kutimiza majukumu yao ya kiraia hasa katika eneo hili la kulipa kodi. Kwa ubunifu huu naamini kabisa wananchi watajitoa kimasomaso katika kuunga mkono jitihada za Serikali katika kutimiza wajibu wao wa kizalendo katika kulipa kodi ambayo ndio msingi wa ujenzi wa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii pia kuishukuru Serikali kwa maamuzi ya upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Kilombero, upanuzi huu siyo kwamba unaenda kutatua tatizo la soko la miwa kwa wakulima wa Kilombero, unaenda kutatua tatizo la sukari katika nchi yetu ya Tanzania. Uwekezaji huu mkubwa ambao haujapata kutokea katika ukanda huu wa Afrika siyo tu ni mfano wa kuigwa kwa sababu unaenda kuongeza ajira ya wananchi wetu lakini unaenda kupanua soko la ajira la vijana wetu ambao wanamaliza shule hawana kazi ya kufanya ama ajira ambayo ina tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo linaenda kuongeza kipato cha vijana wetu lakini inaenda kuwawezesha wananchi wetu uwezo wao wa kuweka akiba ambayo inaweza kuwasaidia katika kuwekeza katika maeneo mbalimbali na hivyo kupambana na jitihada za kupiga vita umaskini, haya yote yatachochea uchumi wetu ili ukuwe kwa kasi, hata hivyo naomba maboresho machache yafanyike:

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; wananchi wetu hasa wa pembezoni siyo tu wanatumia simu kama chombo cha mawasiliano lakini kwao ni muhimu sana, wengi siyo kwamba wanatumia kwa sababu wana fedha, kwa hiyo hii tozo kwa wananchi naomba tuwe na kima cha chini. Kwa mfano, unaweza kusema mwananchi yoyote *consumption* yake ama matumizi yake ya simu hayazidi shilingi 5,000 huyo hatakiwi kutozwa, lakini zaidi ya 5000 pengine ndiyo atozwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litasaidia sana wananchi wetu hasa wenye kipato cha chini kuendelea kuhamasika kutumia mawasiliano kwa ajili ya jithada za kupambana na hali yao. Pia naomba Wizara ya Fedha iangalie njia bora za kupanua wigo wa kodi (*tax base*) katika kuangalia haya makampuni ambayo yanafanya biashara kimtandao wanaita *e-commerce*. Biashara nyingi sasa hivi zimeamia katika mfumo wa biashara mtandao, biashara hizi zinafanywa kwa kiasi kikubwa lakini hatujui *VAT* wanalipia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni makubwa yanafanya biashara hizi za mitandaoni tunaona *Amazon*, tunaona *Alibaba* na wengine, mtu anaponunua bidhaa kutoka kwenye makampuni haya *VAT* analipa wapi, lakini hata *corporate tax* inaenda wapi? Nani anatoza? Kama tunaweza kuangalia eneo hili tunaweza kuongeza uwezo wetu mkubwa wa ukusanyaji wa kodi na hivyo *ku-contribute* katika miradi yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba nizungumzie Tanzania kwa Geografia lakini kwa historia *hegemonic power*, *hegemonic power* katika ukanda wetu, lakini *hegemonic power* katika siasa za Afrika. Ni wakati sasa umefika kwa Serikali yetu, Wizara zetu kuzungumza kwa pamoja kuangalia nafasi yetu, *influence* yetu katika Ukanda wa Maziwa Makuu lakini katka Ukanda wa Kusini na Bara zima la Afrika. Katika hilo tuangalie ushiriki wetu katika mashirika ya Kikanda Kama *SADC*, kama *East Afrika, Cooperation* lakini pia katika *African Union*. Je, nafasi yetu ni

ile ile kama tumelegalega ni wapi? Nini kifanyike ili Tanzania irudi katika nafasi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ni lazima tutumie fedha, Wizara ya Fedha lazima tushirikiane na Wizara ya Mambo ya Nje kuhakikisha kwamba zile *business center* ambazo tulikuwa nazo lazima zirudi na tuzitangaze kikweli kweli. Pia túsitengemee sana watumishi wa Mambo ya Nje katika Balozi zetu kunadi vivutio vyetu, kunadi sekta mbalimbali za uwekezaji. Wakati umefika sasa wa kampuni mashirika na taasisi nyingine kuanza kuajiri watu wao na kuwa *station* katika Balozi zetu, Wizara ya Mambo ya Nje iwe ni *coordinatorama* mratibu wa hawa watu kutoka Bodi ya Utalii na kituo cha uwekezaji lakini pia Taasisi mbalimbali ambazo zinapaswa kutangazwa huko nje. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilivyo sasa wanadiplomasia wetu ambao wanaenda kwenye Balozi zetu ndio tunawatumia kufanya kazi zote ikiwemo kutanganza utalii wetu kitu ambacho naamini tumeona matokeo yake na hatuhitaji mwalimu wa kutueleza wapi ambapo tumeangukia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kilimo ni uti wa mgongo na Bunge hili limejipa jukumu la ajenda la kufanya mapinduzi ya Kilimo. Kilimo hiki ambacho tunasema ni uti wa mgongo tunakichukulia poa kwa kiasi kikubwa, kilimo ni sayansi na kilimo kinagusa kuanzia *natural, social* na hata *economics* na ndio maana uwezi kuzungumzia uzalishaji bila kuzungumzia kilimo. Nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua ndugu yetu Prof. Mkenda kuwa Waziri wa Kilimo, ye ye ni Mchumi na kwa sababu kilimo ni uchumi basi tunaamini kabisa anaenda kufanya mageuzi makubwa na mapinduzi katika eneo hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuona ni jinsi gani kilimo chetu bado hatujakitendea haki kwa sababu hata sera zetu za maliasili, sera zetu za ardhi, za uwekezaji bado zinajji-*contradict* unapozungumzia sera yetu ya kilimo. Kwa hiyo nilikuwa naomba kuwe na mafungamano kati ya sekta ya

kilimo na sekta nyingine, tatizo hapa unakuta ile *concept* ya *ceteris paribus* kwa Wachumi, ambayo inaanzia kuangalia kilimo na kuangalia uchumi wetu kutokea kwenye jicho la viwanda na huduma. Lile linatuonesha ni jinsi gani tunakosea ni lazima hiyo *concept* ya *ceteris paribus* ianzie kuangalia kilimo na kuangalia kwa sababu kilimo ni uzalishaji lakini kilimo kinaenda mpaka kwenye ulaji. Tuangalie sheria zetu zinaangalia vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuona kwamba hata mikopo ya benki inatolewa katika *rate* ambazo mtu anatakiwa kulipa kila mwezi, mkulima wa miwa ambaye anavuna kwa *season* anawezaje kulipa kila mwezi? Lakini mkulima huyu ukimwambia alipe baada ya msimu wa mauzo anaweza akafanya. Unaweza ukampa *mortgage* ya nyumba unaweza ukampa *mortgage* ya mashine na anaweza akatumia vitu hivyo na akalipa kwa msimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja nashukuru sana (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, sasa namwita Mheshimiwa Noah Saputu, jiandae Haji Makame Mlenga.

MHE. NOAH L. S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangi kwenye bajeti hii ya 2021/2022 katika Bunge lako Tukufu. Na mimi nitakuwa mwizi wa fadhila nisipoishukuru sana Serikali ya mama Samia Suluhu Hassan ya awamu ya sita pamoja na Waziri wa Fedha na Mawaziri wote kwa ujumla kwa jinsi ambavyo wameshirikiana kutengeneza bajeti hii na kuiwasilisha kwenye Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo ninaenda kuchangia katika maeneo kadhaa, nikianzia kwenye eneo la ukusanyaji. Ili tuweze kutekeleza bajeti hii na bajeti hii iwe salama lazima Wizara yetu ya Fedha pamoja na taasisi zake zote, zikiongozwa pia na TRA, kuhakikisha kwamba mapato yakutosha yamekusanya kulingana na bajeti yetu. Kwa sababu bajeti hii inategemea makusanyo

ndipo tuweze kuteleza. Kama makusanyo hayatasimamiwa vizuri kama ambavyo wamejitahidi kusimamia ya 2021 malengo yetu haya yote tuliyoyategemea yatashindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, kwa jinsi ambavyo Waziri amewasilisha, na alivyoyipanga, ninaamini kazi itaendelea vizuri. Katika bajeti hii kama hatutakusanya vizuri hatutapata maji, barabara zile barabara zetu za kwenye majimbo, ukosefu wa maji, vituo vya afya na zahanati haitatelezwa. Lakini naamini Waziri akisimama vizuri, na Mawaziri wote wa idara zote bajeti itatekelezwa na hatimaye makisio haya ya trioni 36 ambayo tumekadiria kukusanya yatakusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri ahakikishe kwamba ameweza mifumo rahisi na itakayowavutia walipa ili kodi walipe kodi kwa utaratibu mzuri kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na masharti yasiwe mengi katika kulipa kodi. Kuna watu ambao wanataka kulipa kodi lakini wanapoona huo mlolongo mrefu na vikwazo mbalimbali basi wanashindwa na wanachoka kwenda kulipa kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukiweka urahisi katika kulipa kodi, tuweke usawa, kwa mfano mtu anapokwenda kupeleka fedha benki mlolongo unakuwa ni rahisi kwa sababu anaweka fedha benki lakini anapotoa inakuwa ngumu. Sisi katika kulipa kodi tunaweka mlolongo mrefu. Ningemba milolongo hiyo ipunguzwe ili walipa kodi walipe kodi ili miradi yetu iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya kukusanya kuna suala la upelekaji wa fedha kwenye majimbo na halmashauri. Hili nalo Mheshimiwa Waziri tunawapongeza kwa kipindi hiki cha 2020/2021 kwa sababu mmejitahidi kwa kweli. Kwa mfano kwenye jimbo langu mmetuletea bilioni mbili na *point* juu, mmetupa tena milioni 500 ambayo imetolewa na Mama Samia Suluhu Hassan Rais wetu wa awamu ya sita kwa kweli mmejitahidi. Lakini tunaomba basi tutakapokwenda kukusanya tujitahidi tena mara dufu kwa

sababu wananchi wetu wanategemea na wanaamini kwamba pale ambapo tutapeleka fedha za kutosha kwenye miradi tulyopanga, hiyo ndiyo ahueni na furaha; na utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi itatimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hata tutakapokwenda mbele ya wananchi tutakwenda kifua mbele kwa sababu tumetekeleza ilani ya 2021/2022 bila shida yoyote na watatuelewa vizuri. Kwahiyo naomba hili la upelekaji wa fedha tuhakikishe kwamba tunajitahidi kama tulivyojitatihidi 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kupeleka fedha pia nzungumzie suala la uhaminifu na uhadilifu, kwa maana ya nidhamu katika matumizi. Hili suala la nidhamu na uadilifu katika matumizi ni suala muhimu na nyeti kwa sababu kama tutapeleka fedha lakini bila usimamizi tutakwenda kupata panya wanaotoboa magunia, watatoboa miradi yetu mara tutakapopeleka fedha itakuwa hatujatekeleza vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lazima tuhakikishe kwamba tumewazuia panya wasiharibu bajeti hii, tumewazua waharibifu, kwa sababu inashangaza sana na inasikitisha pale ambapo watu wanaofanya wizi, ujambazi, ujisadi na ulafi ni wale watu ambao wanalipwa mishahara, wanakaa lakini bado wanatamaa ya kuharibu bajeti hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta mtumishi amepewa gari, ofisi, watumishi, wasaidizi, kila kitu lakini bado anaungana na njama za kufanya ujisadi kwenye maeneo ya miradi naomba.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa

TAARIFA

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji kaka yangu anayechangia kiukweli anaongea ukweli kabisa, kwamba hii bajeti imekaa vizuri sana. Kama haitapata panya wakazitafuna hizo pesa tunazopitisha hapa Serikali yetu itakuwa juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilikuwa nataka nimpe taarifa tumchangiaji. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Pokea taarifa hiyo Mheshimiwa

MHE. NOAH L. S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusema, watu hawa ambao ni waharibifu tukiwaachia wakienda kukondesha bajeti hii, bajeti hii ikakonda kwa sababu panya, hatutaweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Mawaziri wote, kwa sababu watatelekeza bajeti hii, wahakikishe kwamba bajeti hii haitakonda, haitakondeshwa, ili hatimaye malengo, nia na madhumuni ya kutelekeza ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika sekta za maji, barabara, elimu, afya na miundombinu vyote kwa ujumla viweze kufikiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo panya hawa tukiwaruhusu; na inashangaza, kama nilivyosema, mtu analipwa mishahara lakini bado ni mwizi na fisadi, yeye ndiye anaanzisha timu ya kufanya uhalifu. Ifike mahali sisi wote kwa ujumla wetu tupige vita rushwa, tutosheke na mishahara yetu. Kwa sababu hata ukikusanya dunia nzima, hata ukikusanya mali ngapi utakufa utaacha lakini huku umewatesa wa akina mama, hawana dawa, umewatesa akina mama wajawazito pamoja na wagonjwa wengine wakakosa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali hata milango yote ya ofisi za Serikali milangoni tuweke acha kupokea rushwa, acha kutoa rushwa. Tukienda kule msalani iwepo acha kutoa rushwa acha kupokea rushwa. Kwenye magari ya Serikali tuweke acha kutoa rushwa acha kupokea rushwa. Kila mlango wa Serikali iweke na popote pale panapotolewa huduma; hata mezani pale kama ni kwa Waziri liwekwe bango linalosema acha rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ya pili nizungumzie suala la posho ya madiwani. Ninaishukuru sana Serikali kwa sababu imewakumbuka madiwani wetu na kuwaweka kwenye sehemu ya kulipa posho zao kutoka wizarani moja kwa moja. Hilo ni jambo jema sana na ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita. Hata hivyo kwa mshahara huu wa madiwani bado tunaomba Serikali iendelee kuangalia, kwa sababu kimekuwa ni kilio cha muda mrefu. Diwani huyu ndiye anayehangaika na kila kitu katika kata. Vilevile tusiwasahau wenyewe viti wa vijiji na vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuyaangalie maeneo hayo kwa sababu nao wanateseka sana, wenyewe viti wa vitongoji na vijiji na hata watendaji wetu wa vijiji ni wachapakazi kule na tunawakabidhi majukumu ya aina mbalimbali. Sehemu hii Serikali yetu imekaa vizuri sana katika masuala ya utawala, lakini naomba basi ikaangalie maeneo hayo kwa kuwa tumetoa fedha hizo za madiwani, na kama zinalipwa na Serikali Kuu naomba Shilingi 250,000 iliyobaki ikawaangalie wenye viti wetu wa vijiji, watendaji wetu wa vijiji pamoja na wenye viti wetu wa vitongoji ili nao waweze kuneemeka na Serikali yao ya Chama Cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri atakapokuwa ku-*windupwajaribu* kutoa waraka maalum wa kuhakikisha kwamba huu utaratibu wa kuwalipa Maafisa Tarafa iko Serikali Kuu lakini hii ya halmashauri itoe waraka unaosema Watendaji wa Kata walipwe kulingana na waraka huu kwenye vituo vya vitongoji kwenye vituo vya vijiji na Watendaji wa Viji. Hii itasaidia sana katika kuhakikisha

kwamba utaratibu huo uliopangwa kwenye bajeti hii kwa watumishi wetu hawa wa chini inafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *property tax*, kwa maana ya kodi ya majengo. Nilikuwa nasema naipongeza Serikali kwa sababu imekuja na utaratibu mzuri wa ukusanyaji wa kodi hii; na muendelee na huo utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningeomba muangalie sana hizi nyumba za tembe, kwa maana ya nyumba za udongo. Unakuta nyumba nyingine ni ya udongo na ina umeme. Je, nayo ni mionganoni mwa zinazoolipa *property tax*? Hilo ni suala ambalo Waziri kama ni mionganoni au kama si mionganoni basi uhakikishe kwamba umeweka utaratibu wa kufanya *analysis* ya kutosha ili wananchi wetu wasiumie. Ukusanyaji wa kodi ni muhimu ili bajeti hii iweze kufikiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na kazi iendelee. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Haji Makame nilishakuwa ajiandae Mheshimiwa Edwini Swalle na Mheshimiwa Samwelii Hhayuma.

MHE. HAJI MAKAME MILENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kupata fursa hii ya kuweza kuchangia jioni hii. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa nikwa katika hali ya uzima. Pili, ninakishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuweza kusimamia mpaka ikafika hapa kuletwa bajeti ambayo kila mtu anaiangalia kwa mtazamo chanya. Nakishukuru sana chama changu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninaipongeza sana bajeti hii hasa kwa sababu imeweza kutaja maeneo mengi ambayo yanaenda kuwagusa wananchi wa nchi hii. Mfano wa maeneo hayo ni kama vile elimu, barabara, maji michezo, wafanyakazi, bodaboda, nakadhalika. Haya yote inaonekana kwamba Serikali imekusudia kufanya na kuleta maendeleo makubwa katika kipindi hiki cha awamu ya sita.

Kwa hiyo na mimi nitatoa mchango wangu mdogo ili tuweze kuona namna gani tunaenda kuboresha zaidi ili kuweza kufikia yale malengo ambayo tumeyakusudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa mwanzo nitaanza kugusa kupitia mifugo. Najua kwamba Serikali imeshajidhatiti hasa kupitia Waziri anayehusika na sekta hii. Wakati bajeti yake ilipopitishwa alijidhatiti na kuona kwamba anaenda kuleta mabadiliko makubwa ili kuweza kutimiza zile haja za wananchi na Bunge hili ambalo michango yao wameitoa. Lakini niweze kusema kuna maeneo ambayo yanaweza yakagusa wananchi hasa wale wa chini, kama vile ambavyo tumesema katika mpango wetu, kwamba tunaenda kuangalia maendeleo ya watu. Niseme kwamba Serikali ikasimame zile benki zetu ili ziweze kurejesha riba za mikopo, kama ambavyo mama ameshauri, kwamba mikopo ipunguzwe riba.

Kwa hiyo ikipunguzwa riba kuna makundi ya vijana kina mama, wale mavu tunaweza tukawapa elimu na wakaweza kusomeshwa ili kuweza kutimiza haja zao kwa kupitia mifugo kama vile kuku. Inaonekana kwamba soko la mifugo hii ya kuku bado lipo kwa sababu soko hili bado linaku kutoka nje, kuna *import* kupitia kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama tutaweza kufanya vizuri maana yake sisi tunaenda kujiwekeza zaidi ili tufanye *export* badala ku-*import*. Watu wana *import* kutoka mfano Brazil na maeneo mengine kuleta kuku nchini ilhali sisi tuna uwezo mkubwa wa kufanya ufugaji huu na baadaye sisi tukaweza ku-*export*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika dhana nyingine ambayo katika kichwa changu inaniambia kwamba tukiweza kuifanya basi ile adhma yetu ya bajeti nzuri tunaweza tukaifikia. Watu wengi wanazungumzia miundombinu, lakini nataka kuzungumza kuhusu jambo kubwa la huduma ambalo linaweza likasababisha kuona yale matakwa yetu yanaweza kufikia kwa urahisi. Kwa sababu inaonekana tukishindwa kulitilia mkazo suala la huduma basi

tunaweza kutapanga mambo mazuri lakini yakashindwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano niseme tu, bajeti hii kila mtu anayekuja hapa anaisifu; lakini si hapa tu hata kwenye mitandao watu wote wanaisifu bajeti hii kutohana na uzuri wake. Sasa tukishindwa kutoa huduma iliyokuwa sahihi maana yake hii bajeti haitakuja na majibu; na kama itakuja bila majibu basi tutabakia na vitabu vyetu kuwa vizuri, lakini hatutapata kile ambacho tulikikusudia kukipata katika jambo hili. Kwa hivyo niseme kwamba tuboreshe huduma hili yale ambayo tumeyakusudia yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano *TRA* timesema kwamba tunaenda kujenga viwanda vingi, lakini baada ya kujengwa kuna watu ambao tumewapa kazi kwa kila mwezi kuweza kuvipitia na kupata huduma katika maeneo haya. Kama huduma hizi hazitakuwa stahiki maana yake tunaweza tukapelekea wawekezaji kutokuridhika na kuweza kuondoka, yapo maeneo ambayo tulipita tukaona kwamba wawekezaji waliondoka kutohana na huduma tu kuwa si nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jambo hili la kuweza kutoa huduma bora tulitilie mkazo mkubwa sana; na nipayendekeze kwamba katika eneo hili tuwape elimu, hasa *TRA* ambao wanaenda kukutana na wafanyabiashara katika muda wote ambao wanakutana na wanazungumza na wanapanga ili wafanyabiashara waweze kulipa kodi. Kodi hii bila kulipa katika hali ya kirafiki maana yake tutaendelea kuhesabu kusema kwamba tuna watu milioni zaidi ya hamsini lakini wanaolipa kodi ni watu milioni 5. Lakini iwapo kama dhana hii ya kutoa huduma itakuwa ni rafiki maana yake tunaenda kuongeza walipa kodi, kwa sababu kila mtu atakuwa anaania ya kwenda kuwekeza lakini pia kulipa kodi kwa sababu huduma anayoipata ni rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme jambo lingine; mfano wa bandarini. Tukiiona bandari yetu maana yake ina hudumia nchi nydingi lakini bado hatujafikia viwango. Watu wanalamika kwa kuona kwamba watu wanaondoka

kutoka bandari yetu wanaenda katika sehemu nyingine lakini ukizingatia mbali ya miundombinu je, huduma yetu tunayoitoa watu wanairidhia? Na kama hwawataridhika maana yake wataondoka. Kwa hivyo lazima tuboreshe suala la huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini sana Serikali kwa namna ambavyo imejidhazititi na suala hili litapewa kipaumbele kikubwa hili kuweza kufikia malengo ambayo tunayataka. Sasa nije katika suala ambalo mimi mwenyewe linanipata mtihani mkubwa, suala la ubinafsishwaji wa benki ya *FBME*. Kwanza hapa ni-*declare interest*. Miongoni mwa waathirika na mimi ni mmoja wao. Kwa kweli jambo hili tukishindwa kuliangalia vizuri, Serikali na kwa sababu Serikali ndiye mdhibiti wa benki hizi za biashara ambazo zinakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo wanastahiki kuangalia zile dhima ambazo Serikali wamebeba kwa ajili ya kuwafanya Watanzania ambao wameathirika. Mimi mwenyewe tarehe 8 Mei 2017 wakati naondoka zangu naenda benki nikiwa sina pesa mfukoni, naenda benki mlangoni nakutana na polisi. Lakini kwa sababu sikuwa jambazi wala sikwenda pale kwa jambo baya sikujishughulisha nao. Nataka kuingia ndani benki wakaniambia soma hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikakuta kwamba benki imezuiwa huduma. Pale bado kidogo nichanganyikiwe kwa sababu mfukoni nilishamaliza na pesa zangu zote zilikuwa ziko benki. Kwa kweli nimeondoka pale nimejikaza, lakini niko barabarani akili nilikuwa sina. Kwa hiyo jambo hili ni kubwa sana, na hapa limezungumzwa mara nyingi lakini ufumbuzi wake unakuwa mgumu. Mimi mwenyewe nimeenda *BOT* mara mbili kusikiliza jambo hili. Cha kusikitisha sana ninapoenda *BOT* nakutana na wanani bemebeleza na kuniambia usiwe na shaka. Pesa benki hii inayoza kutosha mtalipwa nyote na pesa nyingine zitabakia lakini mpaka leo hatujalipwa. Kwa hiyo hata wakibebeleza inakuwa ni bure tu lakini kama mimi niliumia nikiwa mfanyakazi wa Serikali baada ya mwezi mmoja nikalipwa pesa zangu angalau nikapata

kujizuiwa je, wale wengine ambao walikuwa si wafanyakazi wakoje

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hapa kuna watu wamepoteza maisha yao kutokana tu na kuathirika na kukosa haki yao na benki hii kama tumeambiwa ina fedha za kutosha kwa nini atulipwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha ndiye msimamizi mkuu kupitia *BOT*. Wale wadau kama kule Zanzibar walikaa pamoja kutafuta njia na kuona namna gani tufanye na wakajikusanya wakachagua viongozi na wakaona namna gani tufanye. Wakaandika barua ya kuweza kuonana na Wakuu wa *BOT*. Barua hii hapa, Waziri naomba hii barua nimkabidhi aone namna gani, lakini majibu yake mpaka leo hayajapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo tunayozungumza ili huduma, kwamba kama hatutatoa huduma inayostahiki, basi watu wengine wanaweza wakapata taabu kwa sababu ni jambo dogo tu hili la kuwajibu na kukaa nao, kuzungumza nao wakawabembeleza kama ambavyo nimebembelezwa mimi, lakini lilikosekana. Kwa hiyo naomba mhudumu aje uichukue barua hii umpe Waziri ilia one namna njema...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mlenge.

Sasa namwita Mheshimiwa Edwin Swalle, ajiandae Mheshimiwa Samweli Hhayuma.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa ajili ya nafasi ya kuchangia bajeti hii muhimu sana ya Serikali. Nianze kwa kunukuu maneno ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameyasema kwenye ukurasa ule wa 116 wakati akiwasilisha bajeti yake ndani ya Bunge lako Tukufu. Pengine kabla sijanukuu maneno hayo, niseme tu kwamba napenda kumpongeza sana Mheshimiwa

Rais na Amiri Jeshi Mkoo wa Nchi yetu, Samia Suluhu Hassan. Pia nawapongeza sana Waziri wetu wa Fedha, Naibu wake pamoja na timu nzima ya Wizara hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza, kwanza kwa kusikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge, lakini pia nawapongeza sana kwa sababu wamekuwa ni wasikivu na kujibu kilio cha wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia bajeti hii, ukiitazama sura nzima inaanishi kauli mbiu ya Rais wetu, kwamba kazi iendelee. Hii ni kwa sababu bajeti hii ya kwanza imizingatia kuendeleza miradi yote mikubwa ambayo ndiyo imekuwa moyo wa Watanzania katika kupata maendeleo yao. Kwa hiyo kauli mbiu ya kazi iendelee imeakisiwa vizuri sana katika hotuba hii ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea kwenye ukurasa wa 116, Mheshimiwa Waziri alisema, naomba kumnunguu: "*Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amenituma niwahakikishie Watanzania kupitia hotuba hii kuwa, tunaendelea kuijenga nchi, ije mvua, ilje sua, tunaendelea kuijenga nchi, uwe usiku au mchana, tunaendelea kuijenga nchi.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lupembe, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba sisi wananchi wa Jimbo la Lupembe, iwe usiku, iwe mchana, tutaendelea kumuunga mkono kwa kazi nzuri ambayo ameanza kuifanya inayoleta matumaini makubwa sana kwa Watanzania wa nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Lupembe wamenituma nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwamba zile milioni 500 kwa ajili ya barabara za vijijini zimewafikia na kazi inaendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Wizara hii kuhusu kutoza fedha kwenye mafuta kwa ajili ya barabara za vijijini, wananchi wa Jimbo la Lupembe wanayo matumaini

makubwa, kwamba barabara ambazo kwa muda mrefu zimekuwa na shida; Barabara kama ya Nyombo – Ikuna – Kichiwa – Mtwango – Welela sasa itakwenda kupata ufumbuzi. Pia barabara ambayo imekuwa na kero ya muda mrefu ya kutoka Ninga – Lima – Ikondo, kwa bajeti hii itakwenda kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo machache ambayo nataka sasa niishauri Wizara hii. Sehemu ya kwanza ni kuhusu sehemu ya *TRA*. Nilizungumza na Mheshimiwa Waziri wiki mbili zilizopita, kwamba wananchi wa Mkoa wa Njombe, hasa wajasiriamali wadogo wa biashara ya mbaao kumekuwa na biashara kubwa sana kwenye biashara ya miti ya mbaao. Siyo Njombe tu, mikoa mingi ya Nyanda za Juu Kusini kumekuwa na kero kubwa kwa wasafirishaji wa biashara ya mbaao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa, nilimwambia Waziri hapa, kwamba kumekuwa na hitaji la kisheria la watu ambaao wanafanya biashara ya mbaao kusajiliwa kwenye *VAT*. Mfanyakabiashara wa mbaao akisajiliwa kwenye *VAT* anakwenda kununua mbaao kwa wakulima wadogowadogo kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko babu yangu, au mtu ambaye ana msitu, ameufuga kwa zaidi ya miaka kumi, anauza mbaao mara moja tu kwa miaka kumi au 15, lakini kwa mujibu wa sheria hii, inamtaka huyu mkulima mdogo anavyouza huo msitu wa mbaao awe na mashine ya *EFD*. Kwa hiyo huyu mfanyakabiashara aliyesajiliwa kwenye *VAT* takienda kwa yule mwananchi wa kule chini hana risiti ya *EFD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake hapa ni nini? Kumekuwa na udanganyifu mkubwa wa wafanyakabiashara na kukwepa kodi ya Serikali. Pia Maafisa wa *TRA* ambaao siyo waaminifu wamejenga mazingira ya kuchukua fedha kwa wafanyakabiashara wa mbaao. Kwa hiyo biashara ya mbaao Mkoani Njombe imeshuka na baadhi ya wafanyakabiashara wameamua kuacha kabisa hii biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, nilimwomba Waziri na leo namwomba tena, tukimaliza Bunge hili la Bajeti afike Mkoani Njombe akazungumze na wafanyabiashara hawa ili kutatua changamoto ya VAT na biashara ya mbao ambayo kimsingi imekuwa na shida sana. Wafanyabiashara wako tayari kulipa kodi lakini wanahitaji uwekwe mfumo mzuri ambao utakadiriwa na wakajua kwamba ukipakia mbao kiasi fulani, malipo yake ni kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda kuishauri Serikali ni kuhusu elimu kwa mlipakodi. Nimesoma kwenye bajeti hii kuna suala ambalo halijasemwa vizuri. Makamu wa Rais akiwa Waziri wa Fedha aliongea ndani ya Bunge hili kwamba alipokwenda kugombea jimboni aligundua wananchi wengi ni maskini na aligundua kuna ukwepaji mkubwa sana wa kodi na ubadhirifu wa fedha za umma kwenye miradi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hajawa Makamu wa Rais, aliahidi Bunge hili kwamba angetoa elimu kwa Wabunge tujue mianya ya upotevu wa fedha za umma. Naomba nimshauri Waziri; kwa sababu ahadi hii aliitoa Makamu wa Rais wa sasa, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atoe semina kwa Wabunge na Madiwani ambao ni wasimamizi wa shughuli za maendeleo kwenye majimbo haya, wapate semina kujua mianya ya ubadhirifu wa fedha za umma kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia sana kudhibiti upotevu wa fedha ambao Serikali kwa siku za karibuni wanapeleka fedha nyingi sana kwenye halmashauri, lakini bila kuwa na usimamizi fedha hizi zitakwenda kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo napenda kusema ni kwamba, naishukuru sana pia Serikali kwa kutupia macho Mradi wa Liganga na Mchuchuma kule Njombe. Ninachomwomba Waziri wa Fedha, kwa kuwa Rais ameonesha mwelekeo wa mradi huu ukamilike mapema, Mkoa wa Njombe hauna uwanja wa ndege, na nilishauri kwenye mpango wa Serikali kwamba ni vizuri vipaumbele

vya Serikali vikaendana na maeneo muhimu ambayo Serikali imekusudia kuweka fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mkoa wa Njombe ambao sasa unafungua uchumi mkubwa kwenye Mradi wa Liganga na Mchuchuma na ule mkoa una biashara kubwa ya matunda ya parachichi na ni mkoa wa tatu kwa uchumi nchini, hauna uwanja wa ndege. Kwa hiyo namwomba sana Waziri kwenye bajeti yake hii basi aendelee kutazama maeneo ambayo kuna mambo mengi ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba pia kulisema ni kuhusu suala zima la kuwasaidia wananchi kuwa na uelewa wa kudai risiti baada ya kupata huduma. Siku za karibuni kumekuwa na kujisahau kwa Watanzania wengi kudai risiti. Ukienda kwenye sheli sasa hivi, sheli nyingi hawatoli risiti kwa wanaoweka mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na bajeti hii kuwa nzuri ni vizuri akajielekeza kutoa elimu kwa Watanzania ili wajue kodi wanayolipa ndiyo kodi ambayo inawafanya wao kupata maji safi na salama; kodi wanayolipa wanapata elimu bora; kodi wanayolipa ndiyo wanapata maji na kadhalika. Bila kutoa elimu hii kwa Watanzania wakawa sehemu ya kusimamia uchangiaji wa fedha hizi hakutakuwa na maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata Waheshimiwa Wabunge sisi kama sehemu ya kiungo muhimu kati ya Serikali na wananchi ni vizuri pia tukawa na sehemu kubwa ya kuwaelimisha wananchi wetu waone furaha kulipa kodi kwa sababu kodi ni maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Samwelii Hhayuma, wajiandae Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga na Mheshimiwa Kavejuru Felix.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nitumie nafasi hii awali ya yote kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu ya usikivu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani bajeti hii kwa sehemu kubwa imechukua mawazo yetu sisi Wabunge wakati tunachangia Mpango wa Taifa wa 2021/2022 - 2025/2026. Yote ambayo yameletwa mbele yetu ni yale ambayo sisi tumeyaweka Mezani. Bajeti hii ni ya kwetu sisi Wabunge wa Bunge hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, mtani wangu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Naibu wake na wataalam wote kwa jinsi walivyochakata yale mawazo yetu tuliyoyaweka kitaalam na kuakisi mahitaji halisi ya Watanzania kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulilalamikia sana eneo la fedha ndogo inayopelekwa *TARURA* ili iweze kuhudumia barabara zetu za vijjjini. Eneo hilo limeangaliwa vizuri sana. Tulikuwa tunalia vyanzo vingine vipatikane ili tupate fedha zaidi; hilo limeangaliwa, lakini zaidi sana tumepewaa shilingi milioni 500 kwa kila jimbo. Huu ni usikivu wa hali ya juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelia sana eneo la maji. Wakati wa kampeni sisi Hanang hatukuwa na ajenda nyingine; ajenda ya kwanza kwetu sisi ilikuwa maji, ya pili ilikuwa maji na ya tatu ilikuwa maji. Eneo hilo nalo limeangaliwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa tuna changamoto bado zipo, naamini nalo litakwenda kukamilishwa vizuri kwani wapo watu wataalam, wabunifu ambao wanaipenda kazi yao na wanaifanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la umeme; wakati tunajinadi ili tupate kura tulikuwa tunafanya *reference* ya jinsi umeme ulivyokwenda vijiji kupitia REA, lakini kabla ya bajeti ya Nishati kusomwa tulipewa jinsi wakandarasi watakavyokwenda kutekeleza miradi mbalimbali ya REA kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwenye eneo hili, kwamba ni nyeti zaidi, bado kuna maeneo mengi hatuna umeme. Tunatarajia kukusanya fedha kwenye eneo la kodi za nyumba, kwenye LUKU na hasa kuwapelekea watu wengi zaidi, wapate umeme ili tupate kodi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ambao tumepelekewa wa nyumba 20 na kuendelea kwenye vijiji vyetu hautatusaidia sana kukusanya kodi za kutosha kwenye kodi za nyumba. Tupeleke umeme kwa watu wengi zaidi ili tupate kodi zaidi kwenye nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hilo pia nashauri sana tuwashirikishe na viongozi wa chini ili tuwaangalie watu tunaowachaji ni watu halisi ambao wanapaswa kulipa kodi. Inaweza ikatokea kwamba tunapeleka kodi kwenye nyumba na nyumba zina wapangaji. Nao ndio wameanza kulalamika kwenye mitandao ya kijamii, kwamba wao hawamiliki nyumba lakini wanapelekewa kodi. Eneo hilo tuwashirikishe viongozi wa chini kwa sababu Serikali ipo mpaka chini. Tuwatambue wale Wenyeviti wa Vitongoji, Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji, tuwatambue na wenzetu walioko kwenye Kata ili tuwashirikishe vizuri wanaofahamu maeneo hayo vizuri ili tukusanye kodi bila kuleta kelele kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanahanang ni wakulima na wafugaji. Naishukuru sana Serikali yetu ya Awamu ya Sita, eneo la kilimo imeliangalia vizuri sana. Sisi tunategemea kilimo cha ngano na kilimo cha alizeti; maeneo haya yote yameangaliwa vizuri. Naomba mwendo huo twende nao ili angalau wananchi wetu waendelee kunufaika, tupate manufaa kwenye kilimo tunachokilima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliongea sana wakati wa nyuma kuhusu mwekezaji ambaye tunaye kwenye shamba ille lilloluwa la *NAFCO* zamaani, kwamba tupate mwekezaji ambaye yuko makini; naona juhudzi zinaonekana, kazi zinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la mifugo wafugaji wanachohitaji, mifugo yao tuwasaidie kitaaluma. Tuboreshe mifugo, tujenge majosho na malambo, tipeleke chanjo na dawa za uhakika ili hatimaye waweze kufuga kisasa na tupate tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeongelewa mara nyingi sana; maeneo kwa sasa yamekuwa finyu, Serikali iache kufuga. Serikali iache kuchunga ng'ombe. Kazi ya kuchunga watuachie sisi ambao tuna uzoefu wa kuchunga. Yale maeneo, Ranchi za Serikali zile wapewe watu ambao wana asili ya ufugaji, watu wenye nia ya kufuga, ili tupate tija ya kutosha kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba niongelee kidogo eneo la utafiti. Mara zote tumekuwa tukisema kama hujafanya utafiti huna haki ya kusema. Sisi tuna mashirika yetu; *TIRDO*, *TEMDO* na *CAMARTEC*. Ili haya mashirika yawefe kutusaidia, Kamati imesema fedha ambazo wametengewa, bilioni 3.5, ni kidogo sana na ni kweli ni kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutawekeza kwenye utafiti maana yake tutategemea fedha za wafadhili na mfadhili akileta fedha zake maana yake atataka yale anayoyataka yeye ndiyo yasemwe. Serikali iamue sasa kuwekeza kwenye eneo la utafiti ili utafiti utakaofanyika uwe kwa manufaa yetu sisi na uweze kutusaidia katika kutatua changamoto tulizonazo sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na eneo la ardhi. Kwenye eneo la ardhi tumekuwa tukiongea suala la kupima ardhi yote ya Tanzania ili angalau tuweze kupata mapato kwenye ardhi, lakini unakuta kuna ardhi maeneo mengine

tumeyapima tumemilikisha watu. Baada ya kumilikisha ardhi ile utakuta ina kodi zaidi ya miaka 10, 15 hajjawahi kulipiwa. Ina malimbikizo kibao, mtu yule akitaka kuuza ardhi ile hawezি kuuza kwa sababu tayari ina madeni ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba tuangalie eneo hilo; je, yale madeni ambayo tunayo katika ile ardhi tuyatafutie namna, ama kufuta yale madeni ili tuanze upya, tuwape watu wapya ambao wako *serious* na kuendeleza yale maeneo ambayo tumewapatia watu. Au vinginevyo...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako mzuri.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, wajiandae Mheshimiwa Kavejuru Felix na Mheshimiwa Genzabuke.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii niliyopewa ya kuchangia. Nianze kwa kumshukuru Mungu kwa nafasi hii kwa kusoma mstari wa Zaburi ya 136:1 katika Biblia, unasema; "*Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema, kwa maana Fadhilli zake ni za milele.*" (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ninapenda sana kuipongeza Serikali kwa ujumla, hasa Mheshimiwa Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoiifanya pamoja na Mawaziri wote, pamoja na Waziri wa Fedha kwa bajeti nzuri sana ambayo imewekwa mezani petu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii inatoa matumaini makubwa kwa Watanzania pamoja na Wanakilolo ambao kwa kuiangalia tu tayari tumeshaanza kupata matunda ya

Awamu ya Sita kwa zile milioni 500, tumeshazipokea kwa ajili ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunajua tunakaribia kupokea shilingi milioni 600 kwa ajili ya shule za sekondari. Yote hayo tunajua ni juhudini ambazo zinafanyika katika kulikwamua Taifa letu, likiwemo Jimbo la Kilolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais, nami nikaitafakari wakati alipokuwa akiongea na vijana. Tafakari yangu hasa ililenga kwenye kuwawezesha vijana kimitaji. Mheshimiwa Rais amekuja na wazo zuri sana la kuanzisha benki ya vijana. Hapa niliona ni vema nikatoa ushauri wangu. Ushauri huu unatokana na haya yafuatayo:- (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo benki mbalimbali zilizoanzishwa kwa malengo maalum. *National Microfinance Bank (NMB)*, hata kwa maneno yake, ni benki ya mikopo midogo midogo (*microfinance*). Tunayo Mwalimu *Commercial Bank* iliyoanzishwa kwa ajili ya walimu. Vile vile tulikuwa na *Tanzania Women Bank*. Kinachozitesa hizi benki ni riba. Kama riba ingekuwa ndogo, hatuhitaji kuanzisha benki nyiningine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu, tuna benki zenye mtandao nchi nzima. Hizi benki nilizozitaja zote zilikuwa Dar es Salaam, kama zimeenda mbali sana, zitakuwa Arusha au mahali pengine katikati ya miji. Tunazo benki zilizosambaa mahali pote. Pendekezo langu na ambalo nafikiri ningeweza kushauri ni kuanzisha madirisha maalum kwenye benki ambazo hata Kilolo zipo, lakini riba isiwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba kama kuna fedha kwa ajili ya kuanzisha hii benki, hatutawekeza kwenye kodi ya majengo, hatutawekeza kwenye miundombinu, hata wafanyakazi hatutawekeza, tayari wapo. Tuangalie benki ambazo tayari zina mitandao ili vijana hata kesho kama hiyo hela ipo ikiwekwa, wafundishwe hao

wafanyakazi kwenye hizo benki ambazo zipo tayari ili vijana waweze kupata mikopo na waweze kufanyakazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti katika benki pia yakipunguzwa, hawa vijana hata hii benki ikianzishwa kama wataambiwa wapeleke *collateral* ya nyumba, hawana. Kama wataambiwa wapeleke *collateral* ya viwanja, hawana. Kwa hiyo, kinachowatesa siyo benki, ni riba na masharti ya hizo benki. Kama likianzishwa dirisha maalum na hilo dirisha likaondoa hayo masharti, basi kazi itakuwa rahisi sana kuwawezesha vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuongelea suala zima la Madiwani. Tunashukuru Madiwani sasa watalipwa kwa kupitia Serikali Kuu, lakini sisi wote tunafahamu, nami nafahamu hata Mheshimiwa Waziri, nawe ni Mbunge, kuna Madiwani kule Jimboni kwako. Hawa Madiwani wote wanafanya kazi kubwa sana katika kuwashudumia wananchi. Hii posho inayolipwa, bado ni ndogo sana. Napendekeza kwamba kuwe na nyongeza pia ya posho yao licha ya kulipwa kutoka Serikali Kuu. Ikongezwa tutawasaidia sana ili waweze kufanya kazi vizuri na kutimiza majukumu yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee hapo hapo, hizi Halmashauri zilikuwa zinalipa hii posho, tumewapa hiyo nafuu. Hii hela ambayo tumeiokoa ningependekeza yatolewe maelekezo maalum ielekezwe kwenye nini? Nafahamu kwenye Jimbo langu kwa mfano itaokolewa karibu shilingi milioni 10 kwa mwezi au zaidi. Hii fedha inatosha darasa moja la Shule ya Msingi, inatosha kupaua majengo yale ambayo ni maboma. Tusipotoa maelekezo maalum au wasipokuja na mpango maalum wa kuzitumia zile fedha ambazo tumeziokoa kwa Serikali Kuu kulipa, matumizi haya hayataeleweka na huku kuokoa hakutakuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza TAMISEMI itoe maelekezo maalum kwa fedha zilizookolewa kutokana na Serikari Kuu kulipa posho za Madiwani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuzungumzia misamaha ya kodi kwa taasisi za dini. Ninakushukuru kwanza Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali mmeju na msamaha mzuri. Napenda nikwambie kwamba kuna kigezo kilichowekwa cha kusema kuwe na mkataba kati ya Serikali na mtoaji msaada ndipo msahama utolewe. Kuna taasisi ndogo nyingi za dini ambazo zinatoa misaada na nitakupa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye Jimbo langu Kilolo kuna *container* lenye dawa, lenye vitanda kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Kilolo, lina miaka mitatu pale bandarini na lilitolewa na Kanisa na suala ilikuwa ni msahama ambao ulichukua zaidi ya miaka miwili kupatikana. Sasa hivi tunashughulikia *storage* na mpaka sasa sijui itatolewa lini? Ni kwa sababu ile ni taasisi ndogo, lakini imetoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaweza pengine kufanikiwa kuingia mikataba na taasisi zote, lakini zile taasisi ambazo zimesajiliwa na tunajua zinatoa msaada, tukisema kwamba lazima tuingie mikataba, tutachelewa. Hapa sisi wote kwenye maeneo yetu tuna taasisi za dini ambazo zinasaidia na mara nyingi zinakwama kwenye misamaha na wakati huo huo zinachelewesha na kama nilivyozungumza hapa, lile ni kontena la dawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kuna nchi hapa kuna kontena liliupuka na moto ukaunguza nusu ya mji, lakini tumeacha kontena lenye dawa ambazo najua zime-expire lipo bandarini na halijapatiwa msamaha hadi leo. Sasa ni *storage*, wakati huo huo tunajua lina viashiria vyatari kwa sababu hatujui zile dawa ziki-expire zitafanya nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa huo mfano ili kuona umuhimu wa kuharakisha misamaha hasa tunapopokea misaada ambayo tunaihitaji. Kwa sababu sasa pale Kilolo vitanda na dawa tunanunua, Serikali inatoa hela. Kama tungepokea vile, tungekuwa tumeokoa hela nyingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango mzuri sana.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nashukuru. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Sylvester Kavejuru, ajiandae Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

MHE. KAVEJURU E. FELIX: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hili adhimu kwanza kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia kwa kutuletea bajeti nzuri. Nampongeza na Makamu wake Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Nampongeza Waziri wa Fedha, Naibu wake, Katibu na watumishi wote wa Wizara ya Fedha. Bajeti waliyoandaa hakika inatibu kiu ya Watanzania. Mungu awabariki sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru kwa namna ya pekee Waziri Mkuu kwa Mkoa wetu wa Kigoma jinsi anavyosimamia zao la kimkakati la Mchikichi, Mungu ambariki sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie kwenye hoja ya bajeti. Nimeipitia bajeti, nikaangalia Tanzania sasa hivi inakadiriwa kuwa na idadi ya watu milioni 60. Katika milioni 60, ni 5% tu ndio ambao ni *direct tax payer*, wanaolipa kodi moja kwa moja. Asilimia tano katika milioni 60 ni sawa na milioni tatu. Ukitoa kwenye milioni 60 unabakiza milioni 57 ambao sio walipaji wa kodi wa moja kwa moja. Nikaijuliza swali: Je, upo uwezekano wa watu milioni tatu kulipa kodi ambazo zitatosheleza Serikali itoe huduma kwa watu milioni 57? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri wa Fedha anisikilize kwa makini tuna kila haja ya kutafuta na kuangalia ni kwa namna gani tunaweza tukapanua wigo wa kodi. Wigo wa kodi ni lazima utokane na kupanua wingi wa shughuli za kiuchumi ndani ya nchi yetu, naomba nishauri, Tanzania tumejaliwa vyanzo vingi. Mungu ametujalia, lakini hatujavifanyia kazi. Mathalani Mkao wetu wa Kigoma, Mungu ametupa ardhi nzuri, inastawi kila aina ya mazao, lakini ndani ya ardhi hiyo Mungu ametupa madini ya *Dolomite* ambayo ndiyo malighafi haswa ya mbolea ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atambue kwamba katika Mkao wa Kigoma tuna madini ya *Dolomite* ambayo mimi mwenyewe niliwhi kuhusika kwenye kampuni iliyokuwa ya Kimarekani wakapita wa *Anglo American* walikuwa kwenye utafiti wa madini, walisema maeneo yafuatayo; Ilagara, Kazuramimba, Basanza, Makere na Kitagata ni maeneo ambayo yana malighafi ya kutengeneza mbolea ya kusaidia nchi hii na tunaweza tukafanya mapinduzi ya kilimo kwa kupata mbolea ambayo inaweza ikatengenezwa ndani ya nchi yetu. Naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa jicho la pekee. Wakati wale wa Ngara wanasaidiwa kile kiwanda cha Nikeli na Liganga tuangalie uwezekano wa kuwa na kiwanda cha kutengeneza mbolea katika Mkao wa Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikijuliza, kwa nini tunaagiza chumvi kutoka nje wakati sisi kwenye ukanda wa ziwa wa bahari tuna vyanzo vingi vya kutengeneza chumvi? Ukienda kule kwenye Ziwa Eyasi upande Meatu Mkao wa Simiyu, tuna *deposit* kubwa ya chumvi. Ukija Kigoma, ile miamba yote ya Uvinza ni chumvi. Kwa nini tusiweke uwekezaji mkubwa na tukazalisha ya kutosheleza na ile fedha ambayo tunaagiza bidhaa ya chumvi nje tukaitumia kwa mahitaji mengine na badala yake tukauza sisi wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuangalie mahali hapo kama sehemu mpya ambapo itakuwa ni chanzo cha mapato ya fedha ya Serikali na chanzo cha ajira kwa waliokosa ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuendelea, ni lazima tufunge mkanda kwa kufanya mapinduzi katika kilimo chetu. Hata Ulaya waliendelea baada ya kufanya mapinduzi katika kilimo. Tunahitaji sekta ya umwagiliaji ipewe fedha. Zaidi ya hapo kwenye tafiti papewe kipaumbele. Hatuwezi tukasonga mbele kama hatuna tafiti. Tunaomba tafiti kwenye kilimo zipewe kipaumbele, kwenye madini zipewe kipaumbele na kwenye uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwenye uvuvi nayo ni sehemu ambapo tunaweza tukapata fedha.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri, mengine unaweza ukamwandikia Waziri, umechangia vizuri sana.

MHE. KAVEJURU E. FELIX: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makof)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Genzabuke, jiandae Mheshimiwa Dkt. Alice Kajage.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya ya kuweza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu na ninaomba nianze kwa kuunga mkono hoja. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Naibu wake Mheshimiwa *Engineer Masauni* pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu kwa jinsi anavyoendelea kuwapigania Watanzania wa rika zote. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila nikimwangalia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu pamoja na Mama Samia ninakumbuka mbali sana. Mwaka 2015 wakati wakitafuta kura walikuwa wanatembea Pamoja; mama na mtoto wote walikuwa wakiruka kwa chopaa kuhakikisha Serikali ya CCM inashinda. Sasa ninaiangalia bajeti yao ya kwanza Mheshimiwa Mama Samia akiwa Rais wa Awamu ya Sita jinsi gani wanavyofanya kazi mama na mtoto, hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mama Samia kwa namna alivyoshusha *pressure* ya wafanyabiashara kwa kuwahamasisha kulipa kodi bila shuruti. Namshukuru sana Mheshimiwa Mama Samia na wananchi wamelipokea kwa furaha kubwa sana na *pressure* zao zimeshuka kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni uwezeshaji wa wanawake na vijana. Serikali ya Chama cha Mapinduzi kupitia Halmashauri zetu imehamasisha wanawake na vijana kuwezeshwa ili waweze kujajiri hatimaye waweze kupata kipato na kuchangia kodi katika Taifa letu pale watakapokuwa wameweza kusimama vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee kuhusu wanawake wafanyabiashara wa Kariakoo. Soko la Kariakoo la vitenge limekamatwa na wanawake. Wanawake hawa walihangaika kutafuta mitaji, hatimaye wakasimama na wakaweza kuagiza mizigo kutoka nchi za nje na wamekuwa wakifanya vizuri na wamekuwa wakilipa kodi vizuri sana, lakini kutokana na kodi kutokuwa Rafiki, wamefika mahali wanashindwa kufanya biashara zao kwa sababu kodi inakuwa hailipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sisi tumezungukwa na nchi za *DRC*, Zambia, Uganda na nchi zote ambazo zimetuzunguka zimekuwa zikija kuchukua biashara Tanzania, lakini baada ya kuwa kodi siyo rafiki kwa wafanyabiashara wa Tanzania wale wote waliokuwa wakija Tanzania kununua vitenge wamehamia nchi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma walikuwa wakilipa kodi 0.4 na wakati huo walipokuwa wakilipa namna hiyo walikuwa wanaweza kuchangia kwa mwezi shilingi bilioni 9.7 mpaka shilingi bilioni 10. Kwa maana hiyo, wafanyabiashara wa Kariakoo kila mwezi walikuwa na uwezo wa kushusha makontena kuanzia 90 mpaka 120; na kontena moja limekuwa likilipwa kwa shilingi milioni 128. Nchi jirani ya Zambia kontena hilo ambalo Tanzania wanalipa shilingi milioni 128 wao wanalipa shilingi milioni 30. Angalia tofauti iliyopo, ni karibia shilingi milioni 100 nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kugundua hivyo, nchi jirani zilizotuzunguka wameteka masoko ya Watanzania, wanaagiza biashara wao wenye we na biashara zile zinapita kwenye bandari ya Tanzania. Wanapitisha nchini mwetu, wanazipeleka nchini kwao, baadaye zinarudi nchini mwetu kwa sababu vitenge viliwyopo Tanzania, vya kwetu sisi havina... (*Makofi*)

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki anachokizungumza mzungumzaji, kwanza nimpongeze kwa sababu ni kweli kwamba soko la vitenge la Kariakoo limeingia mchanga. Kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maua ambayo yanatengenezwa kwenye vitenge vya Tanzania ndiyo yanaongoza kwa ubora katika *East Africa* na Afrika nzima, lakini kutokana na kupanda kwa kodi kutoka 0.4 na kwenda kwenye 0.6 tumepeoteza kabisa soko kwa Watanzania wengi, wamekuwa *stranded*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Kenya, Uganda, Zambia... (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sanga usichangie. Karibu Mheshimiwa Genzabuke, malizia.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa yake. Kwa maana hiyo, wapo wafanyabiashara ambao tayari wameshahama Tanzania wameenda kuwekeza nchi za nje, lakini wanawake wameshindwa kuhama kwa sababu mama ni mlezi. Mama hawezi kuhama akamwacha baba, mama hawezi akahama akawaacha watoto. Kwa hiyo, wale wameshindwa kuhama wamebaki hapa hapa. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Nina mchangiaji mmoja. Kwa hiyo, naomba amalize. Hizi taarifa zote najua mnataka kumuunga mkono. Kwa hiyo, mengine mwandikleni Waziri wa Fedha. Endelea Mheshimiwa Genzabuke. (*Kicheko*)

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kilio hiki kimfikie Mheshimiwa Rais, Mama yetu Mpendwa, Mama Samia Suluhu aangalie jinsi ya kuwasaidia wanawake hawa ambao ni walipa kodi wazuri, wamekuwa wakiipigania Tanzania ili biashara hii iendelee kubaki Tanzania, Tanzania iendelee kupata kodi kuitia wafanyabiashara wa Tanzania kuliko nchi jirani kuendelea kunufaika na bandari yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara zinapita kwenye bandari yetu zinaenda nchi za Jirani, baadaye zinarudi Tanzania. Tanzania inakuwa haiingizi mapato, mapato yanapotea, hatupati wa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Kengele imelia, husikii shangwe ya makofi mengi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage. (*Makofi*)

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja. Pia namshukuru sana Mwenyezi Mungu kupata nafasi ya kuchangia bajeti hii muhimu sana katika uongozi huu wa Awamu ya Sita na pia katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ikiwa ni bajeti ya kwanza ya miaka mitano 2021/2022 na 2025/2026. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kumpongeza mama yetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Tunamwangalia kiongozi siyo katika maono tu na katika /level/ya usikivu, huyu mama ni msikivu pamoja na Serikali yake yote wamekuja na bajeti ambayo imejibu matamanio mengi makubwa ya Watanzania, pia imejibu hoja mbalimbali ambazo kwa umoja wetu Wabunge tumekuwa tukichangia na tukiishauri Serikali katika Wizara zote ambazo tumechangia, imejibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuipongeza pia Wizara yote, Waziri wetu, Naibu Waziri, Kamati pamoja na Watendaji wa Wizara hii kwa umakini mkubwa kutetea bajeti hii njema. Napongeza vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo vimetufanya kuendelea kuwa na amani mpaka tumefanya mambo yote haya kwa utaratibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali yetu kuendelea kutambua na kuthamini mchango muhimu sana wa watumishi katika kuchangia pato la Taifa. Tumeona jinsi ambavyo Serikali imejibu kwa ujumla wake, kwa mwavuli wake kuhusu maslahi ya wafanyakazi. Sitachambua moja moja, yapo dhahiri kwenye bajeti na wenzangu wameyachangia, lakini kuna suala zima la utengaji wa karibu shilingi bilioni 449 kwa ajili ya upandashaji wa madaraja. Ni jambo jema sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali, katika upandishaji wa madaraja haya; natoa mfano, unakuta kuna kada moja ya taaluma na /level/ sawa ya elimu, lakini unakuta mmoja ameajiriwa mwaka 2014 mwingine 2020 lakini

wamekuja kupandishwa daraja pamoja 2020, wanakuwa *level* moja ya daraja. Hii inavunja morali kwa kwa yule aliyetangulia. Kwa hiyo, naomba nishauri, mnapopandisha madaraja kwa hizi bilioni zilizotengwa, karibia watumishi 92,000 wameshahakikiwa, lakini suala la *seniority* tulizingatie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo Halmashauri zisizopungua 184 na tafiti zinaonesha karibia asilimia 80, Halmashauri zetu tunategemea ruzuku ya Serikali Kuu. Hata hivyo, naomba niipongeze Wizara ya Fedha na Mipango, mwaka 2018 mlikuja na miongozo ya uandaaji wa miradi ya kimkakati katika Halmashauri zetu ili kujijenga kimapato na baada ya kujijenga kimapato Halmashauri zetu ziweze kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi wetu kule kwenye *grassroot*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa napongeza kwamba katika miradi ya kimkakati yote iliyowekwa, miradi sita imekamilika, miradi 32 bado ipo kwenye hatua ya ukamilishaji. Hata hivyo, tafiti zinaonesha miradi hii ya kimkakati ina changamoto nyingi sana. Mojawapo ni changamoto za kiutendaji ambayo ni pamoja na ukosefu wa wataalam wa kuandika yale maandiko. Ukosefu wa hatimiliki za ardi na changamoto za kimuundo nyingine na kitaaluma na taasisi, ni ukosefu wa watalaam husika wa kusimamia miradi ile kwa maana ya ma-*engineer* na wazabuni na vitu vya namna hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwamba imeendelea kuajiri walimu na watumishi wa afya, tunashukuru sana. Naomba nishauri, kada nyingine nazo mzajiri kwa sababu nia njema ya dhima ya bajeti hii ya kujenga uchumi na viwanda kwa maendeleo ya watu, ni kule kwenye watu chini kwenye Halmashauri. Nia yenu njema ya kuja na mikakati hiyo ya kuboresha na kujenga kimapato Halmashauri zetu, changamoto hizi tuziangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wadau wanaohusika na utekelezaji wa miradi hii ya kimkakati

mkiwemo ninyi Wizara ya Fedha na Mipango, ikiwepo TAMISEMI, Sekretariati za Mikoa na Halmashauri, mkae kwa Pamoja. Kuna vigezo vimewekwa ambavyo siyo rafiki na siyo halsia na uwezo wa baadhi ya Halmashauri. Nia ni njema, lakini nashauri mkae mziangalie tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Serikali imekuja na mpango mzuri sana wa afya kwa wote, nia na makusudi ni kwamba kaya zisizopungua 12,000 zipate bima ya afya, lakini pia katika hizo kaya 12,000 asilimia 20 ndiyo kaya za watu ambaao hawana uwezo kabisa na Serikali inasema kila mwaka itakuwa inatakiwa ipate zaidi ya shilingi bilioni 140 na kila mwaka ili angalau katika miaka hii ambayo lengo lake ni katika 2034/2035 kila Mtanzania awe amefikiwa na Mfuko wa Bima ya Afya, yaani kila mwaka iwe inapata zaidi ya shilingi bilioni 149. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna changamoto ya mfuko huu, lazima uwe unapata michango kutoka sekta binafsi, sekta zisizo rasmi na sekta rasmi, najua changamoto ipo kwenye sekta ambazo siyo rasmi. Kwa hiyo, naishauri Serikali itafute mbinu nzuri sana za kuhakikisha kwamba sekta zisizo rasmi zinashiriki kikamilifu katika kuchangia mfuko huu ambaao una nia njema sana ya kwamba kila Mtanzania apate bima ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa michango mizuri sana. Hongereni sana. Kuna mtu amesahau miwani yake, iliachwa hapa kwenye maeneo ya Mawaziri. Kama kuna mtu alikuja, basi aonane na watalaaam wetu wa humu ndani, watampatia.

Mwenyekiti wa Club ya Yanga anatangaza tena kwa umuhimu wa kikao hiki, kuwa leo saa 2.00 usiku kwenye Hoteli ya Morena wanachama wapenzi watapokea Rasimu ya Katiba ya Yanga ambayo inapendekezwa ambayo

itawasilishwa na viongozi wa Yanga amba ni Mjumbe wa Kamati ya Utendaji Ndugu Albinus, Ndugu Senzo Mbatha Mtaalam, Mwenyekiti Kamati ya Mabadiliko Ndugu Raymond na Ndugu *Engineer* Hersi. Tangazo hili limeletwa kwenu na Mheshimiwa Gulamali, Kiongozi wa *Club* ya Yanga kwenye Bunge.

Nichukue nafasi hii vilevile kumshukuru Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, mama yetu Mheshimiwa Jenista na Waziri wa Fedha. Kiti hiki bajeti ya mwaka 2020 na 2019 hakikaliki. Ukiambiwa ukaendeshe kikao cha bajeti, unajuliza mara mbili mbili, unamwomba Mungu kwanza, pilika za humu ndani; Iakini *this time* viongozi wetu mmetuletea bajeti, hongera sana Waziri wa Fedha, hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, mmeefanya kazi ya kuwagusa wananchi kuitia Wabunge wao. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mmeefanya kazi na bajeti hii *for the first time* kila Mbunge wa Jimbo anapewa shilingi milioni 500, wapi tumeona haya mambo? Tupelekeeni salamu zetu kwa mama na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Mungu aendelee kukuongoza uendelee na kazi nzuri, fanya bidii ya kazi nzuri, ibua vyanzo vingine vipyta ili watu waweze kuona maendeleo ya Taifa letu. (*Makofi*)

Baada ya maneno haya naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi,
Tarehe 17 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*